

**USAWIRI WA MWANASIASA WA AFRIKA KATIKA USHAIRI WA
KISWAHILI**

TIMOTHY KINOTI M'NGARUTHI

**Tasnifu Iliyowasilishwa katika Shule ya Mafuzu kwa Madhumuni ya
Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamifu katika Kiswahili ya
Chuo Kikuu Cha Chuka**

**CHUO KIKUU CHA CHUKA
APRILI 2015**

UNGAMO NA IDHINI

Ungamo

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine chochote.

Sahihi
Timothy Kinoti M'Ngaruthi
AD12/07820/12

Tarehe 30/04/2015.....

Idhini

Tasnifu hii imewasilishwa, ikatahiniwa na kupitishwa katika Chuo Kikuu cha Chuka kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamifu katika Kiswahili kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu.

Sahihi.....
Prof. Mwenda Mukuthuria
Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika
Chuo Kikuu cha Mount Kenya

Tarehe 30/4/2015.....

Sahihi.....
Prof. John M. Kobia
Idara ya Sanaa na Fani
Chuo Kikuu cha Chuka

Tarehe 30/04/2015.....

HATILINZI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuchapisha, kuhifadhi kwa mfumo wowote au kutoa sehemu yoyote ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Chuka.

IKISIRI

Utafiti huu ulishughulikia usawiri wa mwanasiasa wa Afrika katika ushairi wa Kiswahili. Kimsingi, mtafiti alichunguza jinsi washairi mbalimbali walivyowasawiri wanasiasa wa Afrika kiubunifu kwa lengo la kudhihirisha walivyobadilika kisiasa na kimaadili kutoka enzi za ukoloni hadi kipindi cha siasa za vyama vingi. Utafiti huu ulichukulia kuwa wanasiasa hawa hutekeleza wajibu mkubwa katika maendeleo ya mataifa yao na bara la Afrika kwa jumla. Uafikiaji wa malengo mbalimbali ya maendeleo kama vile Ruwaza ya 2030 nchini Kenya na uimarishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kiasi kikubwa utategemea maamuzi ya kisiasa. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza nafasi ya ushairi wa Kiswahili katika uhifadhi wa historia ya mwanasiasa wa Afrika; kubainisha sifa za mwanasiasa wa Afrika kabla ya uhuru na kutathmini mabadiliko ya mwanasiasa wa Afrika baada ya uhuru kwa mujibu wa washairi wa Kiswahili. Mtafiti aliichukulia sauti ya mshairi kuwa sauti ya mwananchi ambaye ndiye huathiriwa na maamuzi na vitendo vya wanasiasa. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Ulimbende iliyoasisiwa na William Wordsworth na Samuel Taylor Coleridge na Nadharia ya Baada-Ukoloni ambayo inahusishwa na kazi za Edward W. Said, Gayatri Chakravorty Spivak na Homi K. Bhabha. Utafiti huu ulifanyiwa maktabani ambapo mbinu ya sampuli ya kudhamiria ilitumiwa kuteua data kutoka kwa diwani teule. Uchanganuzi wa kimaelezo ulizingatiwa ambapo mashairi yaliyoteuliwa yalihakikiwa kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti. Tasnifu hii imegawanywa katika sura sita. Sura ya kwanza imejumuisha utangulizi. Katika sura ya pili pana mwauo wa maandishi yanayohusiana na utafiti huu pamoja na misingi ya kinadharia. Sura ya tatu imeshughulikia mbinu za utafiti zilizotumiwa katika utafiti huu. Katika sura ya nne na tano, data imechanganuliwa, kuwasilishwa na matokeo kujadiliwa. Hatimaye, sura ya sita inatoa mahitimisho na mapendekezo kutokana na utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa ushairi wa Kiswahili ni utanzu wa fasihi ulio na umuhimu mkubwa katika kuhifadhi matukio mbalimbali ya kihistoria. Kupitia uhifadhi huu, sifa na vitendo vya mwanasiasa wa Afrika vimebainika katika vipindi mbalimbali vya kisiasa. Imebainika kuwa mwanasiasa wa Afrika aliyeonekana kuwa mzalendo kabla ya uhuru alibadilika ghafla uhuru ulipopatikana na kuwa mkandamizaji wa umma alioapa kulinda. Aidha, wanasiasa walioonekana kutetea upatikanaji wa demokrasia ya vyama vingi hawajatekeleza demokrasia hiyo. Licha ya dosari zilizobainishwa na utafiti huu, ni dhahiri kuwa bara la Afrika bado lina wanasiasa wachache vielelezo ambao wanaweza kuigwa na wanasiasa wa wakati huu na wale wa baadaye. Matokeo ya utafiti huu yatawanufaisha wasomi wa Kiswahili, waandishi na washikadau wote wa masuala ya kisiasa barani Afrika na kwingineko ulimwenguni.

ABSTRACT

This research investigated the portrayal of the African politician in Kiswahili poetry. Basically, this research intended to shed light on how different poets have portrayed African politicians creatively with a purpose of revealing how these leaders have changed since colonial times to the multi-party period. The research assumed that political leaders played a great role in the development of their individual countries and Africa as a whole. The attainment of various developmental goals such as Kenya's Vision 2030 and strengthening of the East African Community is to a large extent pegged on political decisions. The objectives of this research were to investigate the role of Kiswahili poetry in preserving the history of the African politician, to examine the traits of pre-independence African politician according to Kiswahili poets and to evaluate the changes that the African politician has undergone since independence according to Kiswahili poets. The researcher assumed that the poet speaks for the citizen who gets adversely affected by decisions and actions taken by politicians. The study was guided by Romanticism theory developed by William Wordsworth and Samuel Taylor Coleridge and Post-colonial Theory which is associated with the works of Edward W. Said, Gayatri Chakravorty Spivak and Homi K. Bhabha. The study was carried out in the library where purposive sampling method was used to collect data from selected anthologies. Qualitative analysis of the selected poems was done guided by the research objectives. This thesis is divided into six chapters. Chapter one gives the introduction to the study. In chapter two there is a review of related literature which also covers theoretical framework. Chapter three comprises of the research methodology. In chapter four and five, data is analyzed, presented and research findings discussed. Finally, chapter six summarizes the findings of the study and gives recommendations for further research. The findings of this study revealed that the seemingly royal pre-independence African politician changed drastically after independence was attained and became a tormentor of the very people he had sworn to protect. Likewise, politicians who appeared to champion the struggle for multi-party democracy are yet to live to the letter and spirit of that democracy. Despite these shortcomings, it is evident that the African continent has a few political role models whom the current and future politicians can emulate. The findings of this research will benefit Kiswahili scholars, writers and all political stakeholders in Africa and beyond.

TABARUKU

Kwa wazazi wangu wapendwa, Mzee Isaac M’Ngaruthi M’Kirigia na Mama Grace Kaguri, kwa kujitoa mhangana na kunielimisha licha ya changamoto nyingi maishani.

SHUKRANI

Kukamilika kwa tasnifu hii kumethibitisha kuwa imani na matendo ni muhimu katika mradi wowote. Namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia uzima wa mwili na mawazo na kuniwezesha kuianza, kuiendeleza na hatimaye kuikamilisha kazi hii. Hakika Mungu ndiye mpaji asiyechagua wala kubagua kama wafanyavyo binadamu.

Shukrani za dhati pia ziwaendee wasimamizi wa utafiti huu, Prof. Mwenda Mukuthuria na Prof. John M. Kobia kwa kunishauri, kunikosa na kunipa mwongozo wa kitaaluma. Juhudi walizotia tangu nilipopiga hatua za mwanzo za maandalizi ya pendekezo la utafiti hadi kukamilika kwa tasnifu hii haziwezi kupuuzwa kamwe.

Fedha nyingi zilihitalijika katika kuuendeleza na kuukamilisha utafiti huu. Naishukuru Tume ya Taifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI) kwa kuufadhili utafiti huu kifedha. Hatua hii ilithibitisha kuwa lugha ya Kiswahili inatambuliwa rasmi kama chombo mwafaka cha kuendeleza utafiti na kusambaza matokeo yake nchini.

Familia yangu iliniombea na kunipa moyo tangu mwanzo hadi mwisho wa masomo yangu. Mke wangu mpendwa Hellen Kinoti anastahiki shukrani za pekee kwa kunifadhili licha ya majukumu mengi yaliyomkabili, yeye pia akiwa mzamili katika Chuo Kikuu cha Chuka. Binti zangu Karwitha, Kajuju, Kawira na Rehema waliwajibika kila nilipowahitaji.

Wahadhiri wenzangu katika Chuo Kikuu cha Kimethodisti Prof. Simon Thurania, Rev. Dr. John Kobia Ataya na Dkt. John Mariene pia walinihimiza kuukamilisha utafiti huu. Ushauri wa kitaaluma nilioupata kutoka kwa Dkt. Tarsilla Kibaara, Dkt. Catherine Thuita, Dkt. Pamela Muriungi, Bw. Bundi Marete, Bw. Mwaki Arimi na marehemu Gitobu Emaitah hauwezi kupuuzwa kamwe. Nilipokaribia kuvunjika moyo nilipata mawaidha yaliyonirejeshea matumaini kutoka kwa Prof. Nephath Kathuri, Rev. Dr. Isaac Kaberia, Dr. Mercy Thurania na Doreen Katiba miongoni mwa marafiki wengine. Hakika ni vigumu kumtaja kila mmoja aliyehusika katika mradi huu. Nawatambua nyote mlionisaidia kwa njia yoyote, iwe ndogo au kubwa; asante sana!

YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI	Error! Bookmark not defined.
HATILINZI	ii
IKISIRI	iv
ABSTRACT	v
TABARUKU	vi
SHUKRANI	vii
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI	1
1.1 Usuli wa Mada ya Utafiti	1
1.2 Mada ya Utafiti.....	3
1.3 Madhumuni ya Utafiti.....	4
1.4 Maswali ya Utafiti	4
1.5 Sababu za Kuchagua Mada	4
1.6 Upeo wa Utafiti	6
1.7 Maelezo ya Istilahi.....	8
SURA YA PILI: MWAUO WA MAANDISHI	9
2.1 Utangulizi	9
2.2 Ushairi wa Kisiasa	9
2.3 Sifa za Mwanasiasa wa Afrika	14
2.4 Usawiri wa Wahusika wa Kishairi	21
2.5 Misingi ya Kinadharia.....	25
2.6 Hitimisho	30
SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI	31
3.1 Utangulizi	31
3.2 Eneo la Utafiti.....	31
3.3 Uteuzi wa Sampuli.....	31
3.4 Uchanganuzi wa Data	32
3.5 Uwasilishaji wa Data	33
SURA YA NNE: TASWIRA YA MWANASIASA WA AFRIKAKABLA YA UHURU	34
4.1 Utangulizi	34

4.2 Uhifadhi wa Historia Kupitia Ushairi	34
4.3 Taswira ya Viongozi Wazalendo.....	35
4.3.1 Uwajibikaji kwa Umma.....	37
4.3.2 Uongozi wa Kidemokrasia.....	40
4.3.4 Ujasiri.....	41
4.3.5 Uangalifu na Kuheshimika.....	42
4.3.6 Uadilifu	47
4.4 Mashujaa Wengine wa Ukombozi wa Kenya	48
4.5 Upinzani Kabla ya Uhuru.....	62
4.6 Hitimisho.....	67

SURA YA TANO: MABADILIKO YA MWANASIASA WA AFRIKA BAADA

YA UHURU	69
5.1 Utangulizi	69
5.2 Mabadiliko ya Ghafla	69
5.2.1 Wazungu Weusi.....	70
5.2.2 Usawiri wa Wanasiasa Kijazanda	73
5.2.2.1 Wakatili	73
5.2.2.2 Wenye Kiburi.....	76
5.2.2.3 Wenye Wivu na Ujeuri.....	77
5.2.2.4 Mwalimu Julius Nyerere: Mwanasiasa Kielelezo.....	82
5.3 Vuguvugu la Vyama Vingi	84
5.3.1 Vibaraka.....	85
5.3.2 Wapinga Demokrasia.....	87
5.3.3 Wenye Ubinafsi.....	88
5.3.4 Wanyonyaji	89
5.3.5 Wadhalimu	91
5.3.6 Watovu wa Maadili	93
5.4 Kinaya cha Mabadiliko	95
5.4.1 Walafi.....	95
5.4.2 Waharibifu.....	97
5.4.3 Wazembe.....	99
5.4.4 Waendelezaji wa Tabaka	101
5.4.5 Wapenda Vyeo na Pesa.....	104

5.4.6 Wanyakuzi wa Ardhi	107
5.4.7 Wachochezi na Waenezaji Chuki.....	108
5.4.8 Wauaji na Wabakaji.....	110
5.4.9 Wasaliti na Wajanja.....	111
5.4.10 Wanafiki.....	114
5.5. Hitimisho.....	117
SURA YA SITA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	119
6.1 Muhtasari.....	119
6.2 Hitimisho.....	120
6.3 Mapendekezo.....	123
MAREJELEO.....	124
KIAMBATISHO 1: SAUTI YA DHIKI (ABDALLA, 1973)	130
KIAMBATISHO 2: CHEMBE CHA MOYO (MAZRUI, 1988)	140
KIAMBATISHO 3: DIWANI YA KARNE MPYA (WALIBORA, MH. 2007)	147
KIAMBATISHO 4: MSIMU WA TISA (KITHAKA WA MBERIA, 2007)	152

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada ya Utafiti

Mabadiliko mengi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yameshuhudiwa katika bara la Afrika tangu enzi za ukoloni hadi kufikia sasa. Kabla ya majilio ya wakoloni jamii nyingi za Afrika zilijigawa katika vikundi kwa kuzingatia misingi kama vile koo, kabila au vijiji. Hali hii ilibadilika wakati wakoloni walivamia bara la Afrika na kulikalia eneo hili kwa muda mrefu. Wakoloni hawa walibadilisha mifumo ya kiutawala ya wenyeji na kuanza kutawala wakizingatia misingi na mifumo ya kigeni. Kwa mujibu wa Kinyatti (1992), mfumo wa serikali ya kikoloni haukuwa na nia yoyote ya kuwafaidi Waafrika bali uliendeleza unyakuzi wa rasilimali wa hali ya juu. Ili kutekeleza nia hii, wakoloni walitumia sheria kali za kuwakandamiza Waafrika na kupambana na juhudi zozote za kupinga ukoloni. Katika utawala wao, wakoloni hawakujali kamwe tamaduni za wenyeji zilizosisitiza umoja wa wanajamii na ugawanyaji bora wa rasilimali. Badala yake wakoloni hawa walinyakua rasilimali za wenyeji kama vile ardhi yenye rutuba na kuwatumikisha wenyeji katika mashamba na nyumba zao. Ukandamizwaji huu uliwafanya wadhulumiwa kutafuta mikakati ya kujikomboa kutokana na minyororo ya ukoloni. Harakati hizi ziliza kizazi kipya cha mashujaa waliotambuliwa, sio tu katika mataifa yao bali katika bara zima la Afrika.

Washairi wa Kiswahili walitambua juhudi hizi za wapiganiaji uhuru; hivyo wakatunga tendi zilizowasifu mashujaa hawa. Baadhi ya watunzi maarufu walionakili kumbukumbu hizi ni Mohamed (1967), Kibao (1972) na Khatibu (1975). Watunzi hawa waliwasifu wapiganiaji uhuru kwa juhudi zao za kulikomboa bara la Afrika kutoka kwa utumwa wa ukoloni. Aidha, washairi hawa waliwasifu wapiganiaji uhuru kwa kujaribu kuleta uongozi bora chini ya Waafrika wenyewe. Tungo zao vilevile zinaonyesha changamoto nyingi walizokumbana nazo mashujaa hao katika juhudi za ukombozi na jinsi walivyokabiliana nazo bila kuchelea upinzani kutoka kwa wakoloni na vibaraka wao.

Kutokana na hadhi kuu waliyopewa wapiganiaji uhuru pamoja na wanasiasa waliochukua hatamu za uongozi baada ya uhuru, wananchi wengi waliwatukuza hasa marais na wabunge na kukosa kuzihakiki tabia na vitendo vyao. Mrikaria (2010) anasema kuwa hali hii ya kuwatukuza wanasiasa ililifanya kundi dogo la viongozi wa

wakati huo kuanza kupotosha mwelekeo uliokuwa umeanzishwa na wananchi wakati wa kupigania uhuru. Viongozi wa kisiasa wa wakati huo pamoja na vibaraka wao walianza kupinga vikali maoni yoyote yaliyowapinga. Viongozi hawa walifanya kila juhudi kuhakikisha kuwa watu waliotofautiana nao kimawazo walinyimwa nafasi ya kutolea maoni yao. Baadhi ya wakosoaji walioathirika ni washairi kama vile Abdalla (1973) ambaye aliyatungia baadhi ya mashairi yaliyohakikiwa katika utafiti katika jela la Shimo la Tewa. Mshairi huyu alitiwa kizuizini kati ya Disemba 1968 na Machi 1972 baada ya kudaiwa kuwa alinuia kuipindua serikali ya Kenya kwa kutumia silaha.

Unyakuzi wa mali ya umma uliendelezwa na baadhi ya viongozi walioingia uongozini mara tu baada ya uhuru, kama ilivyoshuhudiwa nchini Tanzania kabla ya Azimio la Arusha (Havnevik na Isinika, 2010). Kitendo hiki kiliwakera watunzi mbalimbali wa Kiswahili na kuwatia ari ya kukikashifu vikali kupitia tungo zao. Washairi kama vile Kezilahabi (1974) katika diwani ya *Kichomi* wanawakashifu wanasisia kwa unyakuzi na pia ujilimbikiziaji mali kama vile mashamba makubwa makubwa, viwanja, majumba na magari ya kifahari.

Uhusiano wa ushairi na siasa haukudhihirika tu baada ya uhuru. Historia ya ushairi wa Kiswahili inaonyesha kuwa washairi wa kale kama vile Muyaka bin Haji (1776-1840) na Zahindi bin Mngumi (1758-1828) walishiriki kwa kiasi kikubwa katika siasa za karne ya kumi na tisa. Nabhany (1987) anaeleza kuwa Zahidi bin Mngumi ndiye aliyekuwa rais wa mwisho wa Uswahilini. Kushiriki kwake katika siasa kuliathiri utunzi wake kama inavyodhihirika katika shairi lake liitwalo 'Watu wa Mombasa' (uk. 15) ambapo anawaonya viongozi wa Mvita dhidi ya kuuchezea uongozi wake. Hii inathibitisha kuwa ushairi wa Kiswahili ni utanzu ulio na utajiri mkubwa kama chombo cha kuhifadha historia ya siasa za Afrika na hivyo kuupa uzito utafiti huu.

Ushairi pia unatambuliwa kihistoria kama utanzu ambao umeitumikia jamii zaidi ya tanzu zingine zote za fasihi. Senkoro (1988) anadokeza umuhimu wa ushairi katika harakati za kupigania uhuru katika mataifa kadha ya Kiafrika. Anatoa mfano wa nchi za Tanzania, Angola, Msumbiji na Gine ambapo ushairi ulitumiwa kama silaha ya kifasihi kwani uliweza kupitishwa, kuandikwa, kusambazwa na kuimbwa au kusomwa na wananchi haraka na kwa urahisi zaidi kuliko tanzu za nathari kama vile riwaya na tamthilia. Maoni haya yanaupa utafiti huu nguvu kwani mtaalamu huyu

anatambua dhima ya ushairi katika uhifadhi wa historia ya mwanasiasa wa Afrika kama ulivyofanya utafiti wetu.

Aidha, Mazrui na Syambo (1992) wanaonyesha uhusiano wa ushairi na siasa kwa kurejelea kadhia ya visiwani Pemba, Unguja, Mombasa na Lamu ambako mashairi ya kisiasa yalitumiwa kupambana na Wajerumani; hivyo kuzaa ushairi wa kipekee. Ushairi wa aina hii haukukomea hapo bali uliendelezwa na watunzi waliouona kama chombo muhimu cha kuwasawiria viongozi wa kisiasa waliopigania uhuru na pia walioshikilia hatamu za uongozi baada ya uhuru. Mashairi ya Abdalla (1973), Mazrui (1988) na yale ya Mberia (2007) ambayo yalihakikiwa katika utafiti huu yalilenga kuuzindua umma ili ujikomoe kutokana na dhuluma zilizoendelezwa na wanasiasa wa Afrika waliogeuka na kuwa wakoloni mamboleo.

Utafiti wetu ulichunguza ushairi wa Kiswahili kwa undani zaidi ili kupata taswira kamili ya matatizo yanayoikabili jamii ya kisasa. Baadhi ya mambo yaliyoshughulikiwa ni jinsi wanasiasa wanavyoiathiri jamii kupitia hatua wanazozichukua, ziwe nzuri au mbaya, na jinsi zinavyoiathiri jamii kwa jumla.

1.2 Mada ya Utafiti

Ushairi wa Kiswahili umetumiwa kwa muda mrefu kuwasilisha maudhui mbalimbali. Dhima ya ushairi kama chombo cha kuburudisha, kuelimisha, kuzindua na kuikosoa jamii imetambuliwa tangu mashairi yalipoanza kutungwa. Ushairi umetumika pia kuendeleza masuala ya kidini, kijamii na kisiasa pamoja na kuhifadhi utamaduni wa Waswahili na Waafrika kwa jumla. Licha ya juhudi zilizofanywa na washairi wengi katika kusawiri aina mbalimbali za wahusika, utafiti kuhusiana na ushairi wa Kiswahili umekuwa ukijikita zaidi katika uhakiki wa maudhui na umbo la shairi. Ili kupanua mawanda ya kuuhakikia ushairi, kuna haja ya kutilia maanani uhusiano kati ya ushairi na taaluma nyinginezo kama vile historia na siasa. Hatua hii itausaidia utanzu huu wa fasihi kukua zaidi kupitia uhakiki wake katika mikabala ya taaluma nyinginezo. Utafiti huu uliangazia nafasi ya ushairi wa Kiswahili katika uhifadhi wa historia ya mwanasiasa wa Afrika na mabadiliko aliyopitia tangu kipindi cha kabla ya uhuru, baada ya uhuru na kipindi cha siasa za vyama vingi. Iilitiwa maanani kuwa kwa muda mrefu ushairi wa Kiswahili umekuwa chombo muhimu cha kupigania

mabadiliko ya kisiasa na kusawiria matukio ya kisiasa katika uhalisia wake; hivyo, kuufanya chombo muhimu cha kusaidia kumfahamu zaidi mwanasiasa wa Afrika.

1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo:

- i) Kuchunguza nafasi ya ushairi wa Kiswahili katika uhifadhi wa historia ya mwanasiasa wa Afrika.
- ii) Kubainisha sifa za mwanasiasa wa Afrika kabla ya uhuru kwa mujibu wa ushairi wa Kiswahili.
- iii) Kutathmini mabadiliko ya mwanasiasa wa Afrikabaada ya uhuru kwa mujibu wa ushairi wa Kiswahili.

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulizingatia maswali yafuatayo:

- i) Ushairi wa Kiswahili una nafasi gani katika uhifadhi wa historia ya mwanasiasa wa Afrika?
- ii) Mwanasiasa wa Afrika alikuwa na sifa gani kabla ya uhuru kwa mujibu wa ushairi wa Kiswahili?
- iii) Mwanasiasa wa Afrika alibadilika vipi kisiasa na kimaadili baada ya uhuru kwa mujibu wa ushairi wa Kiswahili?

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Uchaguzi wa mada hii uliongozwa na ukweli kwamba ushairi wa Kiswahili una uwezo wa kuangazia mambo yaliyopita, yaliyopo na yajayo. Kezilahabi (1983) anasema kuwa shairi linaweza kuhakiki wakati uliopita na uliopo na pia kutabiri juu ya wakati ujao. Utafiti huu uliutambua ushairi kama kurunzi ya kumulikia historia ya mwanasiasa wa Afrika, na kuangazia sifa na vitendo vyake kabla ya uhuru, baada ya uhuru na katika kipindi cha siasa za vyama vingi. Vipindi hivi vitatu ni muhimu mno katika historia ya Afrika kwani wakati huu mabadiliko makubwa ya kisiasa yalishuhudiwa katika eneo hili. Mabadiliko haya ni pamoja na upiganiaji na upatikanaji wa uhuru, utawala wa viongozi wa Kiafrika chini ya siasa za chama kimoja na juhudi za kuuondoa utawala huu na hatimaye kuibuka kwa siasa za vyama vingi.

Katika mukatadha wa siasa, utafiti huu utamsaidia mwenyeji wa bara la Afrika kuyatambua mabadiliko ambayo wanasiasa wa eneo hili wamekuwa wakipitia. Mwanasiasa, kama binadamu mwingine yeyote, anatarajiwa kubadilika kutegemea hali za kisiasa, kijamii na kiuchumi za wakati anapoishi. Utafiti huu ulihakiki sifa na vitendo mbalimbali vya mwanasiasa wa Afrika kama vilivyoshughulikiwa katika ushairi wa Kiswahili kwa mujibu wa vipindi vitatu vilivyotajwa hapo juu.

Kuhusiana na masuala ya kijamii, utafiti huu utamsaidia mwanajamii kuichunguza jamii yake kwa kina kupitia jicho la mshairi wa Kiswahili. Jambo hili lingeusaidia umma kuwafahamu vyema viongozi wake na kuzitambua sifa zao na jinsi walivyaothiriwa na tabia za waliokuwa wakoloni kama inavyobainishwa na nadharia ya Baada-Ukoloni. Nadharia hii inashikilia kuwa ingawa wakoloni waliondoka na kuwaachia uongozi wanasiasa wa Kiafrika, ukoloni mamboleo umeathiri pakubwa maendeleo ya bara la Afrika. Hii ni kwa sababu wanasiasawa Afrika waliendeleza matabaka yaliyoanzishwa na mkoloni. Utafiti huu ulibainisha kuwa tabaka la juu, ambalo linajumuisha wanasiasa na matajiri wengine wa kipindi cha baada ya uhuru, linaendeleza unyanyasaji ulioanzishwa na mkoloni.

Kisera, utafiti huu ulinuiwa kuitambulisha lugha ya Kiswahili kama chombo muhimu cha kuendeleza utafiti. Aidha, serikali ya Jamhuri ya Kenya, katika Ruwaza ya 2030 inatambua umuhimu wa utafiti katika maendeleo ya taifa. Lugha hii vilevile inatambulika rasmi kama lugha ya taifa na pia lugha rasmi nchini Kenya. Kiswahili pia ni chombo muhimu cha kuunganisha mataifa ya Afrika na ulimwengu kwa jumla.

Kuhusiana na elimu, utafiti wetu ulilenga kuwachochea watunzi kuzingatia wahusika, kama zilivyo tanzu nyingine za fasihi. Kwa miaka mingi, ushairi wa Kiswahili umejikita zaidi katika masuala ya urari wa vina na mizani, ambao unashikiliwa na washairi wa jadi kuwa uti wa mgongo wa ushairi. Ilitumainiwa kuwa washairi wa baadaye watalenga kuwateua, kuwakuza na kuwasawiri wahusika kwa kina. Wahusika hawa wangesawiriwa kwa kuzingatia mazingira wanamoishi kwa lengo la kuisawiri jamii katika uhalisia wake.

Mtafiti alitumaini kuwa uteuzi, ukuzaji na usawiri wa wahusika kiubunifu ungeufanya ushairi wa Kiswahili kuvutia zaidi. Hatua hii inaweza kuondoa mitazamo na mielekeo

hasi miongoni mwa baadhi ya wasomaji na wahakiki wa mashairi kuwa ushairi wa Kiswahili ni mgumu ukilinganishwa na tanzu nyingine za fasihi. Pia ilitarajiwa kuwa wahakiki wa ushairi wa Kiswahili wangezama zaidi katika uhakiki kwa kuzingatia wahusika. Hii inatokana na umuhimu wa wahusika katika ujenzi wa taswira ya masuala halisi yanayoikumba jamii.

1.6 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika uhakiki wa mwanasiasa kama mhusika katika mashairi teule ya Kiswahili. Uhakiki wa kazi teule uliangazia jinsi washairi husika walivyomsawiri mwanasiasa wa Afrika kwa mujibu wa sifa na vitendo vyake katika vipindi mbalimbali vya kihistoria. Aidha, athari za sifa na vitendo hivyo kwa wanajamii na hisia za wanajamii kuwahusu viongozi wa kisiasa kwa jumla zilijadiliwa.

Mtafiti alizingatia diwani tano ambazo ni:

- i) *Utenzi wa Uhuru wa Kenya* (Salim A. Kibao, 1972)
- ii) *Sauti ya Dhiki* (Abdilatif Abdalla, 1973)
- iii) *Chembe cha Moyo* (Alamin Mazrui, 1988)
- iv) *Diwani ya Karne Mpya* (Ken Walibora, Mh. 2007)
- v) *Msimu wa Tisa* (Kithaka wa Mberia, 2007)

Diwani hizi ziliteuliwa kwa misingi kwamba baadhi ya mashairi yaliyomo yamewasawiri wanasiasa kama wahusika, kwa lengo la kubainisha sifa na vitendo vya mwanasiasa wa Afrika. Mashairi yaliyopatikana humo yalidhihirisha usawiri mwafaka wa mwanasiasa katika vipindi vitatu muhimu; kabla ya uhuru, baada ya uhuru na katika kipindi cha siasa za vyama vingi ambavyo vilirejelewa katika utafiti huu.

Diwani hizi pia zina mashairi yaliyotungiwa katika mazingira tofauti kiwakati na kimahali; hivyo, kutimiza mahitaji ya utafiti huu. Kiwakati, ilichukuliwa kuwa kwa vile mashairi haya yalichapishwa katika vipindi tofauti vya kihistoria, watunzi wake wana tajriba tofauti wanazojadili katika mashairi yao. Kwa mfano, utenzi uliotungwa na Kibao (1972) unarejelea kipindi cha kabla ya uhuru na dhima ya mwanasiasa wa Afrika kama mpiganiaji uhuru. Abdalla (1973) alitunga kudhihirisha jinsi mwanasiasa

wa Afrika alivyobadilika punde tu baada ya uhuru na kuanza kuwanyanyasa wananchi wenzake, hasa waliojaribu kukosoa sera mbovu za ukandamizaji, akiwemo yeye kama mshairi. Naye Mazrui (1988) amemsawiri mwanasiasa wa Afrika katika harakati za kuondoa unyanyasaji wa siasa za chama kimoja na kuingia katika mfumo wa demokrasia ya vyama vingi.

Mkusanyo wa mashairi katika *Diwani ya Karne Mpya* na *Msimu wa Tisa* unamsawiri mwanasiasa wa Afrika katika kipindi cha siasa za vyama vingi. Uhakiki wa mashairi haya ulinuiwa kutathmini mabadiliko ya mwanasiasa wa Afrika baada ya kuondolewa kwa unyanyasaji wa siasa za chama kimoja. Aidha, ulitarajiwa kubainisha iwapo tabia na vitendo vyake ni sawa na vile vya mwanasiasa wa kabla na baada ya uhuru.

1.7 Maelezo ya Istilahi

Afrika: Bara linalozungukwa na bahari za Hindi, Atlantiki, Mediterani na Bahari Nyekundu.

Mashairi ya kisiasa: Sanaa yoyote ya ushairi inayoangazia maudhui ya kisiasa kwa mujibu wa matukio, wahusika na ujumbe uliomo.

Mwanasiasa: Mtu yeyote anayeongoza au aliye na nia ya kuongoza nchi, kaunti, eneo bunge au eneo dogo zaidi la uchaguzi; iwe kwa kuteuliwa, kuchaguliwa au kutumia nguvu.

Mwonoulimwengu: Ni dhana ya kifasihi inayotumiwa kuleta picha ya jinsi mwandishi anavyoona ulimwengu wake, hasa kwa mujibu wa kipindi fulani.

Uhalifu wa kisiasa: Jambo lolote bovu linalotendewa mtu yeyote kutokana na hali iliyochochewa na wanasiasa na kusababisha matokeo ya muda mfupi au mrefu.

Ushairi: Utungo wa kisanaa uliowasilishwa kiubunifu kwa lugha ya mkato na mnato, uwe umezingatia arudhi au la.

Wafadhili wa kisiasa: Watu wanaotumia uwezo wao wa kiuchumi na kijamii kusababisha ghasia, kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

SURA YA PILI

MWAUO WA MAANDISHI

2.1 Utangulizi

Sura hii inajumuisha uhakiki wa maandishi yanayohusiana na utafiti huu. Mtafiti alipitia maandishi mbalimbali kuhusu siasa na wanasiasa wa Afrika kwa lengo la kupata kazi zinazowekea msingi utafiti huu. Mtafiti pia aliaua maandishi yanayohusiana na usawiri wa wahusika katika ushairi kwa jumla kwa lengo la kupata mwelekeo kuhusiana na jinsi angewahakiki wahusika katika diwani zilizoteuliwa. Kazi mbalimbali za kiutafiti zinazohusiana na mada hii pia zilialiwa kwa lengo la kupata kina kilichofikiwa na watafiti wa awali ili kupata pengo la kiutafiti lililohitaji kujazwa. Aidha, misingi ya nadharia zilizoongoza utafiti huu imebainishwa kwa lengo la kuupa mwelekeo wa kitaaluma.

2.2 Ushairi wa Kisiasa

Watunzi na wahakiki mbalimbali wa ushairi kama vile Kezilahabi (1976) wanadokeza kuwa washairi wengi wa Kiswahili huongozwa na matatizo au ufunuo unaowafikia wakati wanapotunga. Mtaalamu huyu anaamini kuwa mtu anayedhulumiwa hawezi kujikomboa pasi na kujiamini na kujiandaa kisaikolojia. Jamii nayo haiwezi kujikomboa bila kuchunguza hali na matukio yanayoizunguka kutegemea mahali na wakati. Kutokana na maoni haya, ni dhahiri kuwa kuna umuhimu wa kuuhakiki ushairi wa Kiswahili kwa kuzingatia matukio ya kihistoria.

Nafasi ya msanii katika kuiakisi jamii yake pia imeelezwa na Thiong'o (1981) anaposema kuwa mwandishi, kama binadamu mwingine yeyote, ni zao la historia, wakati na mahali. Anamwagalia mwandishi kama mwananchi aliye katika tabaka fulani katika jamii; na hivyo, huwa mhusika muhimu katika mapambano ya kitabaka ya kizazi chake. Hapa tunashuhudia uhusiano mkubwa kati ya mshairi na mwanasiasa au waandishi na siasa. Hii ni kwa sababu mwandishi huakisi hali ilivyo katika jamii; na hivyo, mambo kama vile mifumo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii hujitokeza katika kazi yake. Migogoro na misugvano iliyomo katika jamii pia hudhihirika katika kazi za fasihi, ukiwemo ushairi.

Kwa mujibu wa Mulokozi (1982) ushairi wa Kiswahili, ambao una asili yake barani Afrika, una historia ndefu ya utetezi dhidi ya dhuluma za kiuongozi hata kabla ya

eneo hili kujinyakulia uhuru. Akirejelea mfano wa ushairi wa Muyaka, mwanafasihi huyu anaeleza kuwa ushairi tangu kale umekuwa chombo cha kujadilia masuala ya kisiasa. Anasema kuwa mashairi ya Muyaka yanadhihirisha vita vya kihistoria kati ya miji ya Waswahili ya Pate, Lamu, Unguja na Mvita na pia vita dhidi ya walowezi, yaani Waarabu wa Oman na Wareno. Msingi huu unasaidia katika kuutambulisha ushairi wa Kiswahili, ambao ulishughulikiwa katika utafiti kama utanzu muhimu ambao umetumiwa na wasanii kuyajadilia masuala ya kisiasa kwa muda mrefu. Nadharia ya Baada-Ukoloni ambayo iliongoza utafiti huu inaangazia jinsi wanasiasa wa Afrika walivyojitolea kuondoa kasumba za kikoloni baada ya mataifa mengi ya Afrika kujipatia uhuru katika miaka ya 1950 na 1960.

Ushairi halikadhalika hukusudiwa kueleza hisi za ndani alizo nazo mtu kuhusu kitu, kadhia fulani au mtu mwingine na kumfanya mtu yule anayeelezewa kuguswa moyoni na yale yanayosemwa na kumpa maono ya kinachosemwa. Massamba (1983) anaeleza kuwa ushairi huchochea hisia, kuamsha ari, kutoa msisimko na kumzindua mtu na kumfanya aliyelengwa kuathirika sana na yale yasemwayo. Jambo hili linadhihirika katika mashairi ya Abdalla (1973) kama vile 'Jipu' (kur. 7-8) na 'Naja' (uk. 77) ambayo yanatoa taswira ya uchungu wa kudhulumwa kifungoni na ari ya kutaka kuikomboa jamii. Mashairi ya aina hii pia yametungwa na Mberia (2007) yakilenga kuonyesha dhiki zinazoikumba jamii inayonyanyaswa na wanasiasa. Mashairi kama vile 'Minyororo ya njaa' (kur. 1-2), 'Tope la mizozo' (kur. 6-7) na 'Mdundo wa dhiki' (uk.56) yanaafiki kauli hii. Utoaji wa hisia pia unasisitizwa na nadharia ya Ulimbende iliyoongoza utafiti huu. Hata hivyo, kazi ya Massamba (1983) inatofautiana na utafiti huu kwa vile inaangazia tu dhima ya ushairi katika kutolea hisia bila kujifunga na mada ya mwanasiasa wa Afrika kama ilivyofanyika katika utafiti wetu.

Ingawa siku za ukoloni zimepita haimaanishi kwamba matatizo na dhiki za mataifa yetu zimekwisha; sio kwamba maisha katika mataifa yetu yamefikia kilele cha fanaka. Ni kwamba maisha yameingia katika enzi nyingine na kwamba matatizo yake bado yanaendelea; labda sasa kwa hali nyingine. Kazungu (1984) anatambua dhima ya mashairi ya kuifafanulia jamii matatizo yanayoikumba kupitia tungo badala ya kuwafanya wanyonge kuamini kuwa hali ngumu wanazopitia ni majaaliwa yao. Mashairi ya Mvungi (1982) kama vile 'Watu' (uk.49) na 'Vita' (uk.53) yanajadili

matatizo yanayoendelea kuwakumba wanyonge licha ya kuwa huru, huku viongozi wa kisiasa wakiendelea kuishi katika anasa.

Vilevile, kuna washairi walioangazia tamaa ya baadhi ya viongozi waliotaka kusalia mamlakani kwa muda mrefu. Mfano wa washairi hawa ni King'ei (1999). Katika shairi liitwalo 'Kinyume cha Katiba' (uk. 49) mshairi huyu amedhihirisha jinsi baadhi ya wanasiasa huibadilisha katiba ili iwanufaishe. Mshairi huyu anahitimisha kuwa mabadiliko kama hayo hayafai kamwe. Utafiti huu ulichunguza jinsi Mwanasiasa wa Afrika alivyochangia katika kudorora kwa juhudi za wananchi za kujikomboa kikamilifu, sio tu kutoka kwa ukoloni mkongwe bali ukoloni mamboleo.

Baadhi ya tungo za kishairi zilizotungiwa nje ya bara la Afrika pia zinadhihirisha migongano kati ya viongozi wa kisiasa. Katika uhakiki wa utenzi wa *Kalevala* Mulokozi (1992) anadhihirisha jinsi wanasiasa huhusika katika ushindani wa mara kwa mara. Utenzi huu, ambao asili yake ni Ufini unasawiri utangamano kati ya wahusika binadamu na miungu ambao wanajitokeza kama mashujaa wanaopimana nguvu kati ya ufalme wa Karelia na Polijola. Ingawa utenzi huu ulitungiwa katika mazingira ya Ufini ya 1809-1917, uhakiki wake ulichangia utafiti wetu kwa kuwa uligusia suala la upimanaji nguvu wa kisiasa kama unavyoweza kujitokeza popote ulimwenguni, likiwemo bara la Afrika. Hata hivyo, tahakiki hii haikushughulikia mabadiliko ya kitabia na kivitendo ya mwanasiasa wa Afrika kama utafiti wetu ulivyofanya.

Sawa na tungo za kutoka nje ya Afrika, utafiti huu uliutambua ushairi wa Kiswahili kama utanzu ulio na uwezo wa kuhakikia mambo mbalimbali yanayoiathiri jamii. Hii inatokana na historia yake ndefu ukilinganishwa na tanzu nyinginezo za fasihi ya Kiswahili. Kwa mujibu wa King'ei na Kemoli (2001) ushairi ni chombo cha kijamii kilichotumika kwa muda mrefu kuhifadhia historia ya jamii. Aidha, ushairi ulitumiwa kuwasifia viongozi wema na pia kuwahamasisha watu kujikomboa dhidi ya tawala dhalimu. Ni kutokana na misingi hii ambapo utafiti huu ulilenga kudhihirisha dhima ya ushairi kama chombo kilichotumiwa kuhifadhi mabadiliko mbalimbali aliyopitia mwanasiasa wa Afrika kupitia usawiri wake kama mhusika katika tungo mbalimbali.

Katika kuyaangazia baadhi ya masuala nyeti katika kazi za kishairi, Wamitila (2002) anatambua maudhui kadha ambayo hujitokeza sana katika mashairi ya kisiasa. Haya ni pamoja na ukombozi wa wanyonge wanaoteseka kutokana na utawala wa wajanja wachache, udhalimu wa viongozi, upofu wa watawaliwa na unafiki wa viongozi. Mtaalamu huyu anapendekeza kuwa baada ya kuyasoma mashairi, msomaji hana budi kuchukua hatua ya kukemea, kusuta, kulaumu na kujikusuru kuibadilisha hali mbaya inayomzunguka ili kuiunda jamii inayomfaa. Ingawa maoni haya yalichangia utafiti huu kwa kuangalia baadhi ya sifa hasi za wanasiasa, mtaalamu huyu hukuangazia baadhi ya sifa chanya ambazo utafiti huu uliangazia kwa kurejelea baadhi ya wanasiasa wa Afrika kabla na baada ya uhuru kama walivyosawiriwa katika ushairi wa Kiswahili.

Dhima ya mshairi katika masuala ya kisiasa pia imejadiliwa na Mohamed (2002) anapokiri kuwa mshairi kwanza hujitazama kama raia wa nchi yake na pia kama raia wa kimataifa na kuzama katika nafsi yake huku akimulika hisia zake za kiutu na za kiuraia katika upeo mfinyu na mpana. Anasema kuwa yeye kama mtunzi huzingatia dhiki, raha, furaha, shida, uvumilivu na hata kukata tamaa miongoni mwa wanajamii. Anaongeza kusema kuwa mambo haya hayamchomi peke yake bali pia huwachoma na kuwakasirisha raia wengine ndani na nje. Maoni haya yalichangia utafiti huu kwa kuwa yalijadili nafasi ya mshairi kama mwakilishi wa tabaka fulani.

Katika utafiti wake kuhusiana na usemezano katika umalenga wa Kiswahili, Mwamzandi (2002) aliangazia jinsi taarab hutumiwa katika miktadha mbalimbali, ikiwemo mikutano ya kisiasa, kama chombo cha kuwawezesha wananchi kuwasifu na pia kuwasaili viongozi wa kisiasa. Utafiti wake uliangazia jinsi nyimbo za taarab zilivyotumiwa kuyapamba maongozi ya chama cha *Kenya African National Union* (KANU) huku baadhi ya nyimbo zikiukosoa uongozi wa chama kimoja nchini Kenya. Utafiti huu ulichangia utafiti wetu kwa kuwa uliangazia masuala ya kisiasa na sifa za mwanasiasa wa Afrika kabla na baada ya siasa za vyama vingi. Tofauti na utafiti wetu, Mwamzandi alizingatia nyimbo za taarab ambazo ni utanzu wa fasihi simulizi ilhali utafiti wetu unaangazia ushairi andishi. Mtafiti huyu pia hakudhamiria kutafitia masuala ya siasa kama ilivyofanyika katika utafiti huu bali alishughulikia suala la usemezano katika taarab.

Ushairi pia unachukuliwa kama utanzu ulio na uwezo wa kuupa utafiti huu nafasi ya kutalii uwanja mpana; na hivyo, kupata maoni ya washairi wengi iwezekanavyo. Simala (2004) anautambua ushairi wa Kiswahili kama mmojawapo wa tanzu za fasihi zilizo na dhima pana. Anawaeleza washairi wa Kiswahili kama waandishi maarufu waliotambulika kwa usanii wao na uwezo wao wa kushughulikia maudhui mengi. Baadhi ya maudhui waliyoshughulikia ni matukio ya kisiasa barani Afrika, ambayo baadhi yake washairi wenyewe waliyashuhudia. Ni utanzu unaoweza kuchunguzwa kama historia ya utangamano wa wakoloni na jamii ya Waafrika. Aidha, mashairi mengi yametungwa yakilenga kuwasifu na vilevile kuwakosoa wanasiasa katika vipindi mbalimbali vya kihistoria, jambo ambalo limejadiliwa katika utafiti huu.

Aidha, mchango wa washairi wa Kiswahili kama wahakiki wa hali ya siasa ya Afrika unatambuliwa na Njogu (2004) anapowasawiri washairi kama washiriki kamili katika siasa za nchi. Anatoa mfano wa kampeni za uchaguzi kisiwani Lamu ambapo wanasiasa huwalipa washairi maarufu ili wasifiwe nao huku wakiwakashifu wapinzani wao kupitia mashairi. Wanaokashifiwa nao huchukua hatua kama hiyo na kuwatafuta washairi wao ili kupambana na kashifa kutoka kwa wapinzani. Mashairi hayo, ambayo hujulikana kama *kimondo* hughaniwa na manju moja kwa moja ama kurekodiwa kwenye kanda na kucheza redioni. Masuala ya kisiasa, kijamii na kiuchumi ya kipindi hicho cha kisiasa hudhihirika waziwazi katika mashairi hayo. Jamii iliyojigawanya katika vikundi kutegemea uhusiano wa wanajamii na wanasiasa pia hudhihirika. *Kimondo* hutumiwa kuizindua jamii ili kuwapima waomba kura na kuzitathmini historia na vitendo vyao, viwe wazi au vya kisiri, vikilinganishwa na mafunzo ya kidini. Historia na vitendo vya mwanasiasa wa Afrika ndivyo vilivyohakikiwa katika utafiti huu kwa lengo la kuangazia jinsi vinavyoathiri umma.

Uhusiano mkubwa uliopo baina ya washairi na hadhira yao pia umeangaziwa na Ntarangwi (2004). Mtaalamu huyu anadai kuwa wakati mwingine hadhira hutekwa kabisa na wahusika katika kazi ya fasihi mpaka ikajitambulisha na wahusika hao kiasi cha kupoteza utambulishi wake asilia hata kama ni kwa muda tu. Mtaalamu huyu anashikilia kuwa kuna visa ambapo watu wamewahi kubadilisha mienendo yao katika maisha kwa kuathiriwa na wahusika wa kubuni katika fasihi. Hali hii inaweza kujitokeza katika tungo za kisiasa zinazowasawiri wanasiasa kama wahusika. Iwapo watasawiriwa kiubunifu, wahusika hawa wanaweza kuathiri hisia za wasomaji au

hadhira kwa jumla. Hadhira hii inaweza kuchukizwa au kupendezwa na sifa na vitendo vya wanasiasa halisi. Hili linaweza kusababisha mabadiliko makubwa ya kisiasa katika jamii husika, hasa kutokana na ubadilishaji wa mikondo ya upigaji kura; na hivyo, kuufanya ushairi kuwa chombo bora cha kupigania mageuzi ya kisiasa.

2.3 Sifa za Mwanasiasa wa Afrika

Sio washairi pekee walioshughulishwa na tabia na vitendo vya wanasiasa. Wataalamu wa masuala ya siasa pia wamejaribu kuipambanua taswira ya mwanasiasa wa Afrika kwa jumla. Upambanuzi huu unadhihirisha umuhimu wa mwanasiasa wa Afrika kama mhusika muhimu katika maendeleo ya bara hili. Mbugua (1988) anaukosoa mtindo wa uchaguzi wa *mlolongo* uliozingatiwa nchini Kenya katika uchaguzi mkuu wa 1988. Katika uchaguzi huo, wapiga kura walitakiwa kupiga foleni nyuma ya mpigiwa kura au mwakilishi wake na kura kuhesabiwa moja kwa moja. Licha ya mbinu hii kudaiwa kuwa ingepunguza wizi wa kura, mambo yalienda kinyume. Katika baadhi ya sehemu nchini, wanasiasa ambao foleni zao zilikuwa na wapiga kura wachache waliibuka kuwa washindi. Hali hii ilizua mtafuruku mkubwa wa kisiasa nchini, hii ikiwa ni pamoja na kupigwa marufuku kwa jarida maarufu la *Beyond* ambalo liliangazia kwa kina wizi huu wa kura. Hili ni dhihirisho kuwa mwanasiasa wa Afrika wa kipindi cha siasa za chama kimoja alijaribu kila mbinu ili kubaki mamlakani, kama ilivyobainishwa na baadhi ya kazi za kishairi zilizohakikiwa.

Kiini cha mizozo ya kisiasa pia kimechanganuliwa na Bigombe (1993) anayedai kuwa kihistoria, mizozo mingi duniani imewahi na inaendelea kusababishwa na viongozi kukosa kutuliza taharuki zinazosababisha makabiliano kwa kutumia silaha. Anasema kuwa kuna mizozo inayozuliwa na viongozi wanaochezea hisia na nguvu za kimwili za wafuasi wao ili kutimiza matakwa yao ya kibinafsi, kitabaka ama kisiasa. Anatoa mfano wa hali ya mambo nchini Uganda mara tu baada ya uhuru ambapo wanasiasa waliwagawanya wananchi kwa misingi ya kabila, dini na siasa za vyama; na hivyo, kuzua hali ya kutoridhika na kutoaminiana. Hali hii iliendelea nchini Uganda kwa miaka mingi hadi ilipopatikana serikali ya kidemokrasia iliyopo wakati huu. Baadhi ya mashairi yaliyohakikiwa kutoka kwa diwani ya *Msimu wa Tisa* kama vile ‘Werevu’ (uk.8) ‘Waharifu Huru’ (uk. 30) na ‘Magenge Matatu’ (uk. 32)

yalithibitisha jinsi mwanasiasa wa Afrika alivyowagawanya wananchi kwa misingi ya kikabila, kiuchumi na vyama vya kisiasa ili ajinufaishe kisiasa.

Utumiaji mbaya wa mali ya umma na ufisadi kwa jumla ni mambo mengine yaliyotambuliwa na baadhi ya wahakiki kama maovu makuu yaliyovuruga sifa za mwanasiasa wa Afrika. Kibwana (1996) anajadili hali ya kisiasa nchini Kenya wakati wa kupigania mabadiliko ya kikatiba nchini katika miaka ya tisini. Anatoa mfano wa ufisadi katika siasa za vyama ambapo chama cha KANU kilichotawala wakati huo kilitumia pesa nyingi kuwashawishi wapinzani kujiunga nacho kama njia mojawapo ya kuumaliza upinzani. Jambo hili linaashiria mabadiliko ya mwanasiasa wa Afrika kutoka kwa kiongozi mzalendo hadi kiongozi fisadi, kama ilivyobainishwa na Abdalla (1973) katika shairi litwalo 'N'shishiyelo ni lilo' (uk. 1). Katika shairi hili, mshairi anashikilia kuwa alitiwa gerezani na serikali kwa kuwakosoa wanasiasa waliokuwa wakiunyanyasa umma licha ya kupatikana kwa uhuru wa bendera.

Akirejelea migogoro ya kisiasa katika upembe wa Afrika, Wanyande (1997) anasema kuwa mizozo ya kisiasa iliyozuka katika mataifa kadha ya Kiafrika ilisababisha hasara kubwa kupitia kupoteza maisha ya watu, mali na pia uharibifu wa miundomsingi. Mfano mwafaka anaorejelea ni ule wa nchi ya Uganda ambapo rais Idi Amin aliwahi kutawala bila ya kuwepo kwa bunge la taifa ambalo angalau lingeidhinisha sera zake. Hali hii haikuathiri tu nchi ya Uganda bali ilisababisha ukosefu wa usalama katika eneo zima la Afrika na kuifanya nchi ya Tanzania kuungana na waasi wa jeshi la Uganda na kumpindua rais Amin. Nadharia ya Baada-Ukoloni ambayo iliongoza utafiti huu inaafikiana pakubwa na hali ya mambo barani Afrika kama ilivyojadiliwa katika makala haya. Nadharia hii inabainisha kuwa ingawa majeshi ya wakoloni yaliondoka barani Afrika raia wake bado hawajapata uhuru kamili. Baadhi ya wanasiasa barani wamekuwa waking'ang'ania mamlaka na kusababisha mizozo katika nchi zinazohusika, sawa na walivyofanya wakoloni walipong'ang'ania rasilmali barani Afrika. Mizozo ya aina hii imechangia pakubwa katika kuvuruga uhusiano wa mataifajirani kama tunavyoona katika kisa cha nchi ya Uganda na Tanzania.

Baada ya kusambaratika kwa mfumo wa utawala wa chama kimoja katika nchi nyingi za Afrika, siasa za vyama vingi katika sehemu kubwa barani zilishamiri. Kulingana na

Asingo (2003), hatua hii ilionekana mwanzoni kama maendeleo makubwa ya kisiasa yaliyotarajiwa kuondolea mbali uongozi wa kimabavu wa chama kimoja. Hata hivyo, wanasiasa walianza kuvitumia vyama hivi kama chombo kipya cha kujiendeleza kisiasa na kiuchumi. Kwa mfano, baada ya kuanzishwa kwa siasa za vyama vingi nchini Kenya, kulizuka ushindani mkubwa wa kisiasa ambapo baadhi ya wanasiasa hawakujali tena maslahi ya umma bali walivitumia vyama vingi vilivyokuwemo kujihami dhidi ya wapinzani wao. Wengine wao walisababisha vurugu kama ilivyotokea katika baadhi ya maeneo nchini Kenya wakati wa uchaguzi wa 1992. Sifa na vitendo vya wanasiasa wa aina hii zinadhihirika kupitia tungo za washairi mbalimbali katika *Diwani ya Karne Mpya* na *Msimu wa Tisa* ambapo watunzi wanaukosoa utendakazi wa wanasiasa wa aina hii ndani na nje ya bunge.

Shirika la *Kenya Family Development Association* (KENFAD), (1997) linaeleza changamoto zilizokumba uanzishaji wa mfumo wa vyama vingi vya kisiasa nchini Kenya katika miaka ya tisini. Wakati huo, viongozi wengi walioshikilia mfumo wa chama kimoja walieneza propaganda kuwa vyama vya upinzani nchini Kenya viliendelezwa kinyume na sheria. Jambo hili liliwafanya viongozi wa vyama hivi kunyimwa vibali vya kupanga na kuhutubia mikutano ya kisiasa. Kilichoshuhudiwa ni unafiki wa wanasiasa waliotaka kusifiwa na wananchi ambao hawakuridhishwa na uongozi wao. Mazrui (1988) amebainisha unafiki huu wa wanasiasa katika shairi liitwalo 'Vinyago' (uk. 21) ambapo anaonyesha jinsi wananchi walivyolazimika kuwasifu wanasiasa wa kipindi cha siasa za chama kimoja huku wakijua vyema kuwa siasa hizo zilikuwa zimepitwa na wakati. Juhudi hizi za wanasiasa za kujidumisha mamlakani zinajadiliwa katika nadharia ya Baada-Ukoloni ambayo inadhihirisha jinsi wanasiasa wenye ubinafsi wanaweza kuukandamiza umma kwa lengo la kuendelea kutawala.

Gachukia (2005) amejadili suala la uongozi wa kikabila na ule wa vyama vya kisiasa nchini Kenya. Anasema kuwa suala nyeti ambalo Wakenya wanafaa kuhoji ni iwapo nchi yao itaendelea kuongozwa na wanasiasa wanaojali maslahi ya vyama vya kisiasa vilivyowapeleka bungeni au makabila yao. Huku akirejelea historia ya Kenya tangu mwaka wa 1963, mtafiti huyu anasema kuwa nchi hii ilikaribia kuongozwa na chama cha kisiasa muda mfupi baada ya uhuru wakati wa uongozi wa vyama vya *Kenya African National Union* (KANU) na *Kenya African Democratic Union* (KADU). Huu

ni msimu uliotawaliwa na uzalendo wa kipekee na kila juhudi zilielekezwa katika kuboresha maslahi ya Wakenya kama ilivyodhihirika katika *Utendi wa Uhuru wa Kenya* ambao ulihakikiwa katika utafiti huu. Ingawa maoni haya hayakukitwa katika utafiti wa kishairi, kwa kiasi kikubwa yanaoana na yale ya Kibao (1972) ambaye anamsawiri mwanasiasa wa Afrika wa kipindi cha kabla ya uhuru kama wazalendo waliowapa wananchi matumaini makubwa ya maisha bora baada ya uhuru. Hata hivyo, mwanasiasa huyu alibadilika katika kipindi cha baada ya uhuru na kuyavunja matumaini ya umma kama inavyobainishwa na Mberia (2007) katika shairi liitwalo 'Magenge matatu' (uk. 32). Kwa mujibu wa shairi hili, ilitarajiwa kwamba baada ya kuwaondoa wakoloni, viongozi wapya wa Afrika wangesaidia kuyaimarisha mataifa husika bila kujali misingi ya kikabila au miegemeo ya kisiasa.

Kumekuwa na malalamiko ya mara kwa mara kuhusu jinsi wagombeaji wengi wa viti vya udiwani na vile vya ubunge husababisha taharuki katika maeneo yenye mizozo ya mipakani na kutumia nafasi hiyo kujinufaisha kisiasa. Ripoti ya *Government of Kenya* (GoK) (2008) inadokeza jinsi mizozo hii inapofikia kilele wanasiasa hawa hujifanya wakombozi wa kabila zao na kuwahadaa wapiga kura kuwa iwapo wangewachagua wangeyakomboa mashamba yanayodaiwa kunyakuliwa na majirani zao. Ripoti hii inafichua kuwa baada ya wanasiasa hawa kuchaguliwa, hawatimizi ahadi zao bali huchochea vurugu kwa mara ya pili kama njia ya kuwafanya wapiga kura kusahau hadaa zao. Ripoti hii inadhihirisha hali halisi ya maisha ya wanasiasa na uhusiano wao na umma. Aidha, ripoti hii inawachanganua wanasiasa kitabia na kimaadili na kudhihirisha kuwa umma unafaa kuwa mwangalifu usije ukatumiwa na wanasiasa wenye ubinafsi, ambao lengo lao ni kujinufaisha kisiasa na kiuchumi. Uhusiano uliopo kati ya ripoti hii na utafiti wetu ni kuwa kazi zote mbili zinachunguza sifa za mwanasiasa wa Afrika na uhusiano wake na umma. Tofauti yake na utafiti huu inatokana na mabadiliko ya kikatiba yaliyofanyika nchini Kenya. Ripoti hii inajifunga na mwanasiasa katika kiwango cha udiwani na ubunge bila kushughulikia viwango kama vile uongozi wa kaunti na urais kwa mujibu wa washairi wa Kiswahili kama ulivyofanya utafiti huu.

Maoni tuliyojadili hapo juu yanaafikiana na yale ya wahakiki wengine wa kisiasa wanaokisia kuwa mataifa mengi ya Kiafrika yanatawaliwa kwa misingi ya kikabila. Hawa ni pamoja na Southall (2008) anayetoa mfano wa mgogoro wa kisiasa na

kijamii uliozuka nchini Kenya baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007. Mhakiki huyu anayasawiri matukio ya wakati huo kama shinikizo lililokuwemo kwa muda mrefu ambalo hatimaye lilisababisha mlipuko wa uhasama wa kikabila wa tangu jadi uliopandwa na kurutubishwa na wanasiasa. Anashikilia kuwa mgogoro huo haukusababishwa na uchaguzi wa mwaka wa 2007 bali wanasiasa waliutumia uchaguzi huu kama kisingizio cha kueneza ajenda zao za kikabila. Maoni haya yanathibitishwa na yale yanayotolewa na Mberia (2007) katika shairi liitwalo 'Kasisi' (uk. 82) anapozungumzia mauaji ya kasisi aliyekuwa shahidi mkuu katika kesi ya mauaji ya kisiasa yaliyosababishwa na wanasiasa katika Bonde la Ufa. Hii ni ithibati kuwa baadhi ya wanasiasa wa Afrika huongozwa na ukabila wanapoongoza wala sio kujali maslahi ya umma. Tofauti ya maoni ya Southall (2008) na utafiti wetu ni kuwa hayakujikita katika kazi yoyote ya kifasihi, hasa ushairi wa Kiswahili kama ulivyofanya utafiti wetu.

Migogoro ya kisiasa pia inachangiwa na viongozi wa kisiasa waliopo mamlakani kukatalia uongozini hata baada ya kushindwa uchaguzini. Aidha, vyama vya upinzani kwa upande mwingine hudai kuna wizi wa kura au kusia uchaguzi pale tu vinaposhindwa na washindani wake. Kanyinga, Long na Ndi (2008) wanasema kuwa hali kama hii inapozuka malalamiko ya pande zote mbili huwa si ya kuaminika. Hii ni kwa sababu viongozi hawa hawaonekani kutetea haki za wapiga kura bali huongozwa na ubinafsi na tamaa ya uongozi. Ingawa maoni haya yanatokana na ripoti ya tume ya serikali wala sio utafiti wa kishairi, mchango wake ni muhimu katika kuthibitisha hoja za utafiti wetu. Hii ni kwa sababu yametokana na uchaguzi kuhusiana na vitendo vya wanasiasa pamoja na athari zake kwa umma, kama ulivyofanya utafiti wetu.

Ufafanuzi zaidi kuhusu sifa za viongozi wa kisiasa unatolewa na Makillah (2009) anaposema kuwa bara la Afrika kwa kiasi kikubwa huongozwa na wanasiasa waliojaa ubinafsi, choyo, jeuri, kiburi, ujibari na dharau. Anatoa kauli kuwa, katika kizazi hiki, kuna viongozi wahuni, waongo, wababaishaji na hata wajinga walio na elimu duni. Wengi wao hawana uwezo wa kuchambua na kutathmini wanayoambiwa na wananchi. Matokeo yake ni kuzuka kwa maovu kama vile uvisada, vita na kuuana kama ilivyoshuhudiwa katika mataifa ya Kiafrika kama vile Uganda, Somalia na Sudan. Maoni haya yanatofautiana kwa kiasi fulani na utafiti huu kwa kuwa sio sifa za viongozi wabaya tu zilizohakikiwa kwani viongozi vielelezo walichunguzwa.

Utafiti huu ulizingatia sifa za mwanasiasa mzalendo wa kipindi cha kabla ya uhuru na pia mwanasiasa wa baadaye na jinsi alivyobadilika kwa mujibu wa ushairi wa Kiswahili.

Mchango wa mwanasiasa wa Afrika katika uzukaji na uenezaji wa mizozo ya kikabila umechunguzwa na Mworio (2009) kwa kurejelea vurugu la muda mrefu katika mpaka wa jamii za Tigania na Tharaka nchini Kenya. Utafiti wake umegundua kuwa wanasiasa huchangia pakubwa katika uzukaji na uenezaji wa mizozo na chuki za kikabila. Mworio anatoa mfano wa vita vya kikabila kati ya Watigania na Watharaka katika mwaka wa 2007 ambapo viongozi wa kisiasa walitumia fursa ya kutoridhika miongoni mwa wanajamii hawa na kusababisha mizozo iliyotokana na masuala ya ardhi, mipaka ya wilaya na ukabila. Ili kujipatia kura nyingi kutoka kwa kabila zao, wanasiasa hawa walijifanya watetezi wa kabila zao walizodai kukomboa dhidi ya ukandamizwaji na makabila mengine. Utafiti huu, ingawa si wa kishairi, ulichangia kazi yetu kwa vile mtafiti anajadili tabia za wanasiasa sawa na kazi yetu. Visa vya mapigano ya kisiasa vilivyozuka nchini Kenya wakati wa uchaguzi wa miaka ya 1992, 2002 na 2007 vilijadiliwa katika diwani ya *Msimu wa Tisa* kupitia shairi litwalo 'Kasisi' ambapo kasisi aliyeshuhudia mauaji ya kikabila katika Bonde la Ufa aliuawa ili kuficha dhuluma waliyotendewa wananchi.

Maoni kuhusu sifa za mwanasiasa wa Afrika pia yametolewa na Skinner (2010) anayeshikilia kuwa bara la Afrika limejaa viongozi waliozingirwa na ufiada na ukabila. Anasema kuwa baadhi ya viongozi hawa waliwalazimisha wananchi kufuata mfumo wa chama kimoja cha kisiasa huku wakidai kuwa ndio uliokaribiana zaidi na mfumo wa kijamii ya Kiafrika. Udanganyifu huu wa wanasiasa hatimaye ulizua miungano ya kisiasa ya kikabila katika mataifa mengi ya Afrika. Matokeo yake ni kuibuka kwa serikali zilizojaa vurugu na kutoafikiana. Skinner anapendekeza kuwa wanasiasa wa Afrika wanapaswa kubadilisha mitazamo yao ya kisiasa kutoka kwa miungano ya kikabila hadi muungano wa kitaifa. Tofauti na utafiti wetu, mwandishi huyu ametoa maoni ya jumla ambayo hayakuthibitishwa kupitia utafiti. Maoni yake vilevile yamejifunga na kipindi kimoja tu cha kihistoria, yaani kile cha utawala wa chama kimoja. Utafiti wetu ulizingatia sifa na mabadiliko ya mwanasiasa wa Afrika kabla ya uhuru, baada ya uhuru na kipindi cha siasa za vyama vingi kama anavyosawiriwa katika ushairi wa Kiswahili.

Uongozi ni suala linaloathiri sekta nyingi za kimaendeleo, sio tu barani Afrika bali katika ulimwengu mzima. Viongozi wa kisiasa ndio wanaoshikilia, kudhibiti na kusambaza mamlaka na rasilimali katika taasisi nyingi za kisiasa. Kwa mujibu wa Kipsang na Chepkuto (2011) wanasiasa, iwe wameingia uongozi kupitia uchaguzi au mapinduzi ya kijeshi, sharti wajitayarisha kikamilifu katika masuala ya uongozi, wajitolee kuitumikia jamii na wawe vielelezo wanaowatia moyo raia ili waweze kufikia maazimio yao maishani. Maoni ya wataalamu hawa yanachangia utafiti wetu kwani yanahusiana na suala la uwajibikaji wa wanasiasa kama lilivyojitokeza katika diwani ya *Msimu wa Tisa*. Kupitia mashairi yake yaitwayo ‘Msimu wa Tisa’ (uk. 9) na ‘Msimu Mwingine wa Wasaliti’ (uk. 12) mshairi anajadili jinsi Afrika inaongozwa na wanasiasa wasiowajibika bungeni. Mshairi anawakashifu wanasiasa hawa kwa uzembe wao bungeni ambapo hawajadili na kupitisha mambo muhimu ya kuunufaisha umma.

Uchanganuzi wa kisiasa uliofanywa na mwanasiasa mmoja wa Kenya unatilia shaka dhima ya mwanasiasa wa Afrika kama kielelezo. Hamisi (2011), ambaye aliwahi kuwa mbunge nchini Kenya, anafichua uozo mkubwa uliowahi kutekelezwa na wanasiasa nchini Kenya. Mwandishi huyu anaonyesha jinsi baadhi ya wabunge katika bunge la tisa walikosa uwajibikaji na pia kushiriki ufiisadi na uzinzi katika ofisi za umma. Hamisi, pia, anafichua jinsi uteuzi wa baadhi ya viongozi wakuu serikalini ni wa kutiliwa shaka. Hili ni dhahirisho kuwa uteuzi huu hutekelezwa kwa lengo la kujinufaisha kisiasa au kujaribu kuficha ukweli fulani. Ufichuzi huu ulichangia utafiti huu kwani ulisaidia kudhihirisha jinsi mwanasiasa wa Afrika anavyoendelea kubadilika kitabia sawa na ulivyofanya utafiti huu. Diwani ya *Msimu wa Tisa*, ambayo ni baadhi ya kazi zilizohakikiwa katika utafiti huu, inajadili tabia na vitendo vya wabunge wa Kenya, kama inavyodokezwa na Bertoncini (2010).

Ripoti kuhusu ushindani wa nguvu za silaha katika eneo la Afrika Mashariki pia zinajitokeza kupitia vyombo vya habari. Muindi (2012) anaripoti kuwa kwa mara ya kwanza bajeti ya jeshi la Uganda imeipiku ile ya Kenya. Matumizi haya makubwa ya fedha katika ununuzi wa silaha na uimarishaji wa jeshi yanadaiwa kutokana na mzozo wa kisiwa cha Migingo. Umiliki wa kisiwa hiki ulizua mzozo kati ya serikali na wavuvi wa Kenya na wale wa Uganda; hivyo, kutishia kuzuka vita kati ya mataifa haya. Ripoti hii inachangia utafiti huu kwani inaonyesha jinsi viongozi wa kisiasa

hutumia mbinu mbalimbali katika kuimarisha utawala wao. Ushahidi unaotolewa na Wamitila, (2007) katika shairi litwalo ‘Tazama’ (uk. 25) unaonyeshakuwa masikini wanapoendelea kuishi katika dhiki wanasiasa hutumia rasilimali za kitaifa katika kuimarisha utawala wao. Hali hii huwafanya wananchi kutokuwa na imani na viongozi wao kiasi cha kuwashuku hata viongozi walio na mipango bora ya kuleta maendeleo.

Mwandishi mwingine aliyechangia katika kufafanua tabia za Mwanasiasa wa Afrika ni Miguna (2012). Miguna anafafanua jinsi unyakuzi wa ardhi pamoja na mali nyingine ya umma ulivyofanywa nchini Kenya katika kipindi cha siasa za chama kimoja. Anatoa mfano wa unyakuzi wa Msitu wa Mau na viongozi wa kisiasa, wakiwemo viongozi wakuu serikalini. Unyakuzi huu ulisabababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na kuathiri pakubwa upatikanaji wa maji kwa wananchi wanaozunguka eneo hilo. Suala la unyakuzi wa ardhi pia lilibainika katika utafiti wetu kuwa mojawapo ya matatizo sugu yanayolikabili bara la Afrika. Kwa mfano, katika diwani ya *Msimu wa Tisa* kwenye shairi litwalo ‘Usingizini’ (uk. 3) mshairi analalamika jinsi wanasiasa hujinyakulia mashamba yenye rutuba huku familia za walionyang’anywa mashamba hayo zikiangamizwa na njaa. Hata hivyo, mshairi hakufafanua kinachowafanya wanasiasa hawa kuwa na tabia hii.

Maoni ya watafiti na wahakiki mbalimbali tuliowajadili katika sehemu hii yalichangia katika utafiti huu kwa kuwa yaliangazia, kwa kiasi fulani, sifa za mwanasiasa wa Afrika. Aidha, yalithibitisha mchango wake kwa baadhi ya mizozo inayolikumba bara la Afrika. Kauli za wataalamu hawa ni muhimu kwani zinamulika mataifa na viongozi halisi; hivyo kuusaidia utafiti huu katika kujenga taswira yao kamili kwa mujibu wa mahali na wakati kama inavyojitokeza katika kazi za kishairi zilizohakikiwa.

2.4 Usawiri wa Wahusika wa Kishairi

Watafiti kadha wa kitaaluma walichangia utafiti huu kwa namna walivyoushughulikia ushairi wa Kiswahili. Baadhi ya utafiti ulijikita katika kazi za kishairi zilizohakikiwa katika utafiti wetu huku utafiti mwingine ukijadili mchango wa mwanasiasa katika mizozo mbalimbali inayoiathiri jamii.

Utafiti uliofanywa na Chacha (1980) kuhusu maudhui katika mashairi ya Abdilatif Abdalla unamwagalia mshairi kama mtetezi wa haki za wanyonge. Utafiti wake ulibainisha jinsi ushairi wa Kiswahili unaweza kutumiwa kama chombo mahususi cha kutolea hisia za wananchi kuhusu dhuluma wanazotendewa na viongozi wao. Utafiti wa Chacha ulishughulikia maudhui ya kisiasa kwa lengo la kubainisha matatizo yaliyolikumba bara la Afrika baada ya uhuru wa bendera. Ameyagusia baadhi ya matatizo yaliyojadiliwa katika utafiti wetu kama vile ushindani wa kisiasa na ujilimbikiziaji mali kwa upande wa wanasiasa walioingia mamlakani. Hata hivyo, utafiti wetu haukujifunga na ushairi wa mtunzi mmoja kama ulivyofanya utafiti wa Chacha. Utafiti wetu ulipiga hatua zaidi na kuchunguza kazi za washairi wengine na pia ulilenga kipindi kipana zaidi. Utafiti wa Chacha ulifanywa katika kipindi cha baada ya uhuru na kabla ya kuingia katika kipindi cha utetezi wa siasa za vyama vingi na hatimaye kuzaliwa kwa mfumo wa siasa za vyama vingi.

Masuala ya wanawake katika fasihi ya Kiswahili yameshughulikiwa na Ndungo (1985) huku akiongozwa na nadharia ya Kifeministi. Mtafiti huyu ameuchunguza usawiri wa mwanamke katika *Utendi wa Mwanakupona*(1860) na kudhihirisha jinsi mhusika wa kike anavyonyanyaswa katika miktadha ya kidini na ndoa. Hata ingawa mtafiti huyu hakuwachunguza wahusika katika muktadha wa kisiasa, utafiti wake uliujengea msingi utafiti huu kwani umehusika na usawiri wa wahusika katika ushairi wa Kiswahili. Vilevile unagusia suala la dhuluma ambalo pia limejadiliwa katika utafiti huu kupitia usawiri wa baadhi ya wanasiasa wanaojitokeza kama viongozi dhalimu, hasa baada ya uhuru. Kazi hii ilipiga hatua zaidi kwani ilichunguza usawiri wa wahusika wa kisiasa kwa mujibu wa hisia zinazotolewa na washairi wa Kiswahili kama wawakilishi wa wanajamii.

Utafiti uliofanywa na Mwamzandi (1996) ulidhihirisha kuwa wahusika katika ushairi wa Kiswahili ni muhimu hasa pale suala la maigizo linapoangaziwa. Utafiti huo ulibaini kuwa wahusika katika tungo za Kiswahili wanaweza kutazamwa kama watendaji wanaotoa kauli zinazosaidia kutimiza lengo la mwandishi. Utafiti wa Mwamzandi ulichangia utafiti wetu kwa kuwa ulishughulikia baadhi ya tungo za Abdilatif Abdalla (1973) sawa na ulivyofanya utafiti wetu. Aidha, ulimulika baadhi ya sifa za mwanasiasa wa Afrika kama ulivyofanya utafiti wetu. Mfano wa sifa hizi ni

kiburi kama inavyofichuliwa na Abadalla (1973) kutika shairi liitwalo ‘Mamba’. Ubeti wake wa pili unasema hivi:

Kuna mamba, mtoni metakabari
Ajigamba, na kujiona hodari
Yuwaamba, kwamba ‘taishi dahari

Mtafiti huyu amejadili sifa za mwanasiasa wa Afrika kwa kumlinganisha na mamba, sawa na ulivyofanya utafiti wetu. Mamba anasawiriwa kama mnyama mwenye nguvu aliyejaa kiburi. Mbali na kuwatishia wanyama wengine wanaoenda mtoni kunywa maji, mnyama huyu huwaua na kuwala wanyama hao. Uhusiano wa mamba na wanyama wengine unadhihirisha jinsi baadhi ya wanasiasa hujiona kama watakuwa na mamlaka milele. Jambo hili huwatia kiburi, sawa na kile cha mamba anayetawala mtoni na kuwadhulumu wanyama wanyonge. Tofauti na utafiti wa Mwamzandi, kazi hii ilishughulikia mwanasiasa wa Afrika kwa kina zaidi kwa lengo la kuonyesha sifa zake kabla ya uhuru na kutathmini mabadiliko ya kisiasa na kimaadili aliyopitia baada ya uhuru, ikiwa ni pamoja na kipindi cha siasa za vyama vingi.

Usawiri wa wahusika katika muktadha wa kidini ni mada nyingine iliyotafitiwa katika ushairi wa Kiswahili. Momanyi (1998) ametafiti kuhusu usawiri wa mwanamke Mwislamu katika jamii ya Waswahili na kudhihirisha jinsi mwanamke Mwislamu hudhulumiwa na kudunishwa kupitia mafunzo ya dini ya Kiislamu. Sawa na Ndungo (1985), mtafiti huyu alijifunga na masuala ya kifeministi katika utafiti wake na kuwaacha nje wahusika wa kisiasa. Utafiti wetu ulishughulikia mwanasiasa wa Afrika na mabadiliko aliyopitia katika kipindi cha kabla ya uhuru, baada ya uhuru na wakati wa siasa za vyama vingi.

Aidha, utafiti uliofanywa na M’Ngaruthi (2007) kuhusu usawiri wa wahusika katika mashairi ya Mbega (1984) na yale ya Mohamed (2002) ulidhihirisha aina kadha za wahusika. Hawa ni pamoja na wahusika binadamu, wahusika wanyama, vitu visivyo hai na viungo vya mwili. Utafiti huo pia ulidhihirisha mazingira mbalimbali wanamopatikana wahusika wa kishairi. Haya yalijumuisha mazingira ya kijiografia, kihistoria, kiuchumi na kisiasa. Utafiti huo unauwekea msingi utafiti wetu kuhusiana na wahusika katika ushairi hasa pale unapobainisha wahusika wa kishairi katika mazingira ya kisiasa. Hata hivyo, utafiti wetu unapiga hatua zaidi na kuwashughulikia

wahusika maalum, ambao ni wanasiasa wa Afrika na mabadiliko wanayopitia katika vipindi mbalimbali vya kihistoria.

Uhusiano wa wahusika katika kazi za kishairi na zile za maigizo unajitokeza kupitia utafiti wa Emaittah (2007) kuhusu tamthilia ya Kiswahili na maendeleo yake nchini Kenya kati ya 1953 na 1975. Mtafiti huyu amedhihirisha jinsi utanzu wa utendi unavyoweza kuchunguzwa kwa misingi ya kidrama kupitia wahusika katika *Utendi wa Fumo Liyongo* na *Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa*. Suala la migogoro ya kisiasa na utawala wa Afrika kabla ya uhuru linajitokeza katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Utenzi huu unasimulia juu ya ushindani na wivu wa kisiasa kati ya Fumo Liyongo na Daudi Mringwari. Mringwari, ambaye alikuwa mtawala wa Pate wakati huo, alichelea upinzani na hivyo kupanga njama ya kumwangamiza Fumo Liyongo. Hatimaye anafanikiwa kumwua Fumo Liyongo ambaye alimwona kama mpinzani wake mkuu. Mtafiti huyu anadhihirisha kuwa ushindani, wivu na usaliti wa kisiasa vilikuwepo hata kabla ya majilio ya wakoloni na hivyo kuchangia katika kufafanua tabia za viongozi wa kisiasa katika bara la Afrika. Tofauti iliyoko hapa ni kuwa mtafiti huyu hakulenga usawiri wa wahusika wa kisiasa katika ushairi wa Kiswahili kama ulivyofanya utafiti wetu bali alizingatia kipengele cha maigizo.

Matokeo ya utafiti wa Waliaula (2009) yalidhihirisha kuwa maandishi mengi ya kisiasa, yakiwemo ya kishairi, huchochewa na mazingira ya kisiasa ya wakati wa uandishi. Mtafiti huyu anaeleza kuwa baada ya nchi ya Kenya kujipatia uhuru, viongozi wa kisiasa waliamua kuunyamazisha Upinzani. Wengi wa waliothubutu kuikosa serikali walitiwa kizuizini, jambo ambalo lilisaidia kuijenga fasihi iliyotungiwa magerezani. Kazi hizi zilidhihirisha hisia za waandishi wake kama Wakenya na pia kama watu binafsi waliodhulumiwa na serikali yao. Baadhi ya waandishi waliowahi kufungwa nchini Kenya kwa kuikosa serikali ni pamoja na Abdilatif Abdalla na Alamin Mazrui, ambao tungo zao zilihakikiwa katika utafiti huu. Tofauti ya utafiti wa Waliaula na utafiti wetu ni kuwa utafiti wake ni wa fasihi linganishi ilhali utafiti wetu ni wa ushairi wa Kiswahili. Aidha, mtafiti huyu alizingatia kazi zilizotungiwa gereza kwa jumla, zikiwemo zile za fasihi ya Kiingereza. Utafiti wetu ulijumuisha mashairi ya Kiswahili yaliyotungiwa ndani na nje ya gereza.

Utafiti uliofanywa na Kelly (2014), ulidhihirisha ufiada wa hali ya juu ambao umekuwa ukiendelezwa na baadhi ya wanasisia barani Afrika. Wanasisia hawawalihusika katika kashfa za unyakuzi wa ardhi pamoja na wizi wa pesa kutoka kwa benki na taasisi nyingine za kifedha. Akirejelea mfano kutoka kwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, mtafiti huyu wa masuala ya kisiasa anasema kuwa aliyekuwa rais wa Jamhuri hiyo, Mobutu Sese Seko alikuwa amejilimbikizia kiasi cha dola bilioni nane kabla ya serikali yake kupinduliwa mnamo 1997. Fedha hizi zilikuwa zimefichwa katika benki zilizo nje ya bara la Afrika. Ingawa utafiti wake si wa kishairi, Kelly anatusaidiakuthibitisha kwamba baadhi ya wanasisia wa Afrika wa kipindi cha baada ya uhuru walijawa na tamaa na ubinafsi, kama wanavyoshikilia washairi ambao kazi zao zilihakikiwa katika utafiti wetu.

Kwa muhtasari, mazingira ya kisiasa yametambuliwa kuwa na umuhimu mkubwa katika uteuzi na usawiri wa wahusika katika ushairi wa Kiswahili. Mshairi anapotaka kuzungumzia unyanyasaji wa kisiasa kupitia uongozi mbaya huwatumia wahusika kama vile viongozi dhalimu, vibaraka wao na umma unaonyanyaswa. Migogoro ya kisiasa inayotokana na matukio na hali hizi hujengeka waziwazi kupitia mahusiano ya wahusika hawa, kama inavyodhihirika katika utafiti huu.

2.5 Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili zilizokamilishana ili kutimiza madhumuni ya utafiti. Nadharia mojawapo ni ile ya Ulimbwende. Kulingana na Ousby (1996) nadharia hii iliasisiwa na washairi William Wordsworth na Samuel Taylor Coleridge. Watunzi hawa walihisi kuwa fasihi, hasa ushairi, ilifaa kutumika kuelezea hisia nzito kupitia ubunifu wa hali ya juu bila kufungwa na arudhi za kijadi. Ousby anafafanua kuwa mtazamo wa kilimbwende ulijaribu kuelezea mabadiliko yaliyodhihirika katika fasihi, sanaa na utamaduni huko Uropa kwa lengo la kuinusuru fasihi kutokana na minyororo ya kiarudhi iliyosababisha utata katika ufafanuzi wa masuala mbalimbali.

Kuhusiana na ushairi wa Kiswahili, sifa za Ulimbwende zinadhihirika kupitia utunzi wa mashairi yasiyofungamana na sheria zilizowekwa kitambo. Wafula na Njogu (2007) wakimnukuu Topan (1974) wanaeleza kuwa, tofauti na ushairi wa kimapokeo unaosisitiza uzingatiaji wa arudhi, wanaulimbwende wanashikilia kuwa ushairi wa Kiswahili unafaa kuelekezwa na hisia za mtunzi. Aidha, wanasisitiza utumizi wa lugha

rahisi na ya kawaida inayotumiwa na watu katika maongezi na majibizano ya kila siku badala ya kutumia lugha ngumu na ya kikale isiyooana kamwe na hali halisi ya maisha ya watu. Kwa wanaulimbwende, dhima ya ushairi ni kuwasiliana na watu wa kawaida wanaoishi mashambani.

Nadharia hii ni muhimu katika utafiti huu kwani inasisitiza utunzi wa mashairi bila kujifunga na arudhi; na hivyo, kuyapa nafasi mashairi huru. Utafiti huu ulichunguza mashairi ya kiarudhi pamoja na mashairi huru. Uhakiki wa aina hizi mbili za tungo ulisaidia kudhihirisha kuwa suala la kuzingatia au kutozingatia arudhi haliathiri kamwe uwasilishaji wa ujumbe. Diwani za *Utenzi wa Uhuru wa Kenya* na *Sauti ya Dhiki* zinajumuisha mashairi ya arudhi ilhali diwani za *Chembe cha Moyo*, *Diwani ya Karne Mpya* na *Msimu wa Tisa* zinajumuisha mashairi huru na yale ya kiarudhi.

Kwa mujibu wa Hill (1977) William Wordsworth na Samuel Taylor Coleridge waliendeleza msimamo wa kilimbwende kupitia mashairi ya kihisia waliyoyaita *Lyrical Ballads*. Coleridge aliyatunga mashairi yaliyosisitiza kuwepo kwa wahusika mashujaa wenye sifa za ukiaumbile. Hawa pia walifungamanishwa na hisia nzito ambazo zingejitokeza endapo matukio hayo yangekuwa halisi huku yakisababishwa na nguvu zisizo za kimaumbile.

Ufaafu wa nadharia hii ulitokana na mihimili kadha. Kwanza, nadharia hii inasisitiza ubunifu wa hali ya juu katika uteuzi wa aina mbalimbali za wahusika na vitendo vyao, ambapo vitu vya kawaida huwasilishwa akilini kwa njia isiyo ya kawaida. Ubunifu wa hali ya juu huhitajika hasa katika kuwaunga wahusika pamoja, wawe viumbe vilivyo hai au vitu visivyo hai. Kwa kuwa ushairi ni sanaa inayotumia lugha kiubunifu, usawiri bora wa wahusika kwa kiasi kikubwa huzingatia ukweli wa kibunilizi au ushabihikweli. Mashairi mengi yaliyohakikiwa katika utafiti huu yametungwa kwa ubunifu wa hali ya juu, hasa yale yanayowakosoa wanasiasa. Baadhi ya watunzi kama vile Abdalla (1973) na Mazrui (1988) wametumia jazanda katika kuwasawiri wanasiasa kwa sababu za kiusalama, hasa katika vipindi vya kisiasa, ambapo wanasiasa walikuwa na uwezo mkubwa wa kumkandamiza yeyote aliyethubutu kuwakosoa.

Wahusika katika tungo mbalimbali zilizohakikiwa katika utafiti huu wamewasilishwa kwa ubunifu wa hali wa juu ambapo washairi wanawarejelea kwa kutumia mbinu za kitamathali kama vile sitiari, ambapo mtu hutajwa kama kitu au mnyama fulani badala ya kumrejelea moja kwa moja. Katika mashairi kama vile ‘Nahodha na jahazi’ (uk. 5) na ‘Mwashi’ (kur. 40-42) katika diwani ya *Msimu wa Tisa*, mwanasiasa analinganishwa na nahodha kutokana na umuhimu wake wa kuliongoza taifa. Aidha, rais Nyerere anaitwa mwashi kwa jukumu alilotekeleza katika ujenzi wa Tanzania baada ya uhuru.

Pili, nadharia hii inasisitiza uteuzi wa wahusika na matukio kutokana na maisha ya kawaida kama ambavyo wangepatikana katika kijiji chochote na vitongoji vyake. Kwa mujibu wa Wordworth (1925), Coleridge katika ushairi wake alikuwa akiwatafakari, kuwafuatilia na kuwatambua wahusika hao pindi walipojitokeza ili aweze kuwasawiri katika mashairi yake katika uhalisia wao. Hii inamaanisha kuwa mashairi anapotunga kazi yake anafaa kuchota maudhui yake kutoka kwa mambo yanayoendelea mahali anapoishi. Ni hali zinazomkumba au kuwakumba walimwengu wenzake zinazofaa kumpa msukumo wa kuandika. Watunzi wa mashairi yaliyohakikiwa katika utafiti huu wamerejelea matukio ya kisiasa katika bara la Afrika ambalo wao ni wenyeji, huku wakimsawiri mwanasiasa wa Afrika kama mhusika katika mashairi yao kwa mujibu wa vipindi mbalimbali. Kwa mfano, Kibao (1972) anasema jinsi alivyojitahidi kuyafuatilia na kuyakusanya matukio ya kipindi cha kabla ya uhuru katika ubeti ufuatao:

3

Jitihada nimefanya
Kuwaeleza wa Kenya
Mambo niliyokusanya
Kitabuni kuyatia

Ubeti huu unadhihirisha uhalisia wa kazi zilizohakikiwa katika utafiti huu. Watunzi wake walichota maudhui na wahusika katika mazingira walimoishi.

Tatu, kama anavyosisitiza Hill (1977) ulimbwende unakita katika kuyafanya matukio na hali zilizomo katika kazi za kishairi kuwa ya kuvutia kwa kuyahusisha na hali ya kimaumbile na ujenzi wa taswira. Ujenzi wa taswira ni muhimu mno katika kazi za

fasihi kwani ndio humfanya msomaji kupata picha fulani mawazoni mwake kuhusiana na kinachorejelewa na mwandishi. Katika utafiti huu, baadhi ya mashairi yaliyohakikiwa yanajenga taswira kamili akilini mwa msomaji kwa mujibu wa mazingira yalimotungiwa. Kwa mfano, Mberia (2007) katika shairi liitwalo ‘kitini’ (uk.18) anamrejelea mwanasiasa wa Afrika kama mkalatusi. Mshairi anasema hivi:

Baada ya umma uliochoshwa na kiu cha haki
Kumiminika shambani wakiimba kwa umoja
Na kung’oa mikalatusi iliyonyima umma maji
Waliotukejeli kwa tashbihi za mtini na wembe
Sasa, wameketi kwenye kiti cha bembea cha taifa
Wakila matunda ya mti uliopandwa na waliosahaulika

Kupitia usawiri huu, msomaji anapata taswira ya mazingira yenye miti mirefu kwa mifupi. Miongoni mwa miti hii ni mikalatusi inayofyonza maji mengi kutoka ardhini na kuifanya mimea midogo inayoizunguka kunyauka kwa kukosa unyevu wa kutosha. Taswira hii inamfanya msomaji anayeufahamu mkalatusi kufanya urejeshi kwa upesi na kulinganisha uhusiano wa mikalatusi na miti mingine na ule wa mwanasiasa dhalimu na umma.

Nne, nadharia ya Ulimbwende inatilia mkazo hali ya kuwafanya wahusika kuziakisi hali za mazingira kwa mujibu wa wakati. Huu ni mhimili muhimu sana katika utafiti huu kwa sababu mtafiti alimrejelea mwanasiasa wa Afrika kwa mujibu wa vipindi vitatu maalumu. Vipindi hivi ni wakati wa ukoloni, baada ya uhuru na kipindi cha siasa za vyama vingi. Utafiti huu ulichunguza nafasi ya ushairi wa Kiswahili katika uhifadhi wa historia ya mwanasiasa wa Afrika.

Tano, nadharia ya Ulimbwende inashikilia hali ya kuwafungamanisha wahusika na hisia nzito. Kupitia ushairi, watunzi hudhihirisha hisia kama vile mapenzi, hasira au chuki kutokana na mambo wanayoyapitia au kushuhudia umma ukiyapitia. Tabia na vitendo vya watu mbalimbali, wakiwemo wanasiasa, vinaweza kuwafanya wananchi kupendezwa, kuchukizwa au kufurahishwa na wanayoyashuhudia. Ni hisia hizi zinazowafanya wananchi kutoa maoni yao kuhusiana na viongozi hao. Hisia zinazodhihirishwa zinaweza kutumiwa kuonyesha uhusiano uliopo kati ya kundi la watawala na watawaliwa, kama utafiti huu ulivyogundua.

Nadharia ya Ulimbwende inashughulikia usawiri wa wahusika kwa jumla bila kujikita katika aina maalum ya wahusika. Kutokana na udhaifu huu, palihitajika nadharia ambayo ingeshughulikia masuala ya kisiasa, hasa kuhusiana na tabia na vitendo vya wanasiasa. Nadharia ya Ulimbwende pia haiangazii sababu za kisiasa, kijamii na kiuchumi zinazochangia kuibuka kwa mizozo ya kisiasa katika viwango vya kitaifa na kimataifa. Palihitajika nadharia ambayo ingeangazia mchango wa tabia na vitendo vya wanasiasa wa Afrika katika mizozo hii.

Nadharia iliyosaidia kufidia pengo hili ni ile ya Baada-Ukoloni. Kwa mujibu wa Childs & Williams (1997) baada-ukoloni ni dhana inayohusishwa na kazi za Edward W. Said, Gayatri Chakravorty Spivak na Homi K. Bhabha. Kazi za waandishi hawa zinajumuisha kipindi kilichofuatia kile cha ukoloni baada ya zilizokuwa koloni za Uingereza kujipatia uhuru katika miaka ya 1950 na 1960. Licha ya mataifa husika kuushangilia uhuru, Childs & Williams (1997) wanaonya kuwa uhuru kutoka kwa mkoloni ni ndoto ambayo haikutimia. Hii ni kwa sababu mkoloni alijigeuza sura na kujitokeza kama mkoloni-mamboleo. Mkoloni alihakikisha kuwa amemwathiri Mwafrika kisiasa, kitamaduni na kiuchumi. Hali hii ilisababishakuibuka kwa tabaka jipya la Waafrika walioanza kuwanyanyasa Wafrika wenzao, hasa wale wa tabaka la chini. Utafiti wetu ulitathmini mabadiliko ya mwanasiasa wa Afrika baada ya uhuruna athari za mabadiliko hayo kwa umma.

Ashcroft na wenzake (2007) wanaeleza kuwa dhana ya baada-ukoloni inajihusisha na athari za ukoloni kwa tamaduni na jamii mbalimbali. Wanasema kuwa tangu miaka ya 1970 uhakiki wa fasihi unaojadili athari za kitamaduni zilizotokana na ukoloni umekuwa ukizingatia nadharia ya Baada-Ukoloni. Aidha, nadharia hii imekuwa ikitumiwa kuchunguza taratibu na athari za ukoloni pamoja na hatua za kuuondoa tangu karne ya kumi na sita hadi uondoaji wa ukoloni-mamboleo wa kipindi cha sasa. Utafiti wetu ulishughulikia sifa za mwanasiasa wa Afrika kabla na baada ya uhuru kwa lengo la kuchunguza jinsi kiongozi huyu alivyojitolea kupigana na ukoloni. Aidha, utafiti wetu ulishughulikia athari za ukoloni-mamboleo kwa umma kupitia sifa na tabia za mwanasiasa wa baada ya uhuru. Hii ilitokana na ukweli kwamba iwapo taifa halijakuwa huru kikamilifu kutoka kwa wakoloni, raia wake pia hawajakuwa huru (Childs & Williams, 1997).

Kimsingi, nadharia ya Baada-Ukoloni hujumuisha uhakiki wa kazi za fasihi kwa lengo la kuelewa uhusiano uliopo baina ya mataifa yaliyotawaliwa na yaliyotawala (Njogu & Chimerah, 1999). Hii inamaanisha kuwa uhakiki wa fasihi unaoongozwa na nadharia hii hulenga kubainisha jinsi mkoloni alivyomwathiri Mwafika wakati na baada ya ukoloni. Uhakiki huu pia huzingatia hatua zilizochukuliwa na Mwafrika ili kujikomboa kutoka kwa mkoloni, akiwemo mkoloni-mamboleo. Utafiti wetu ulizingatia sifa za mwanasiasa wa Afrika kabla ya uhuru kwa lengo la kudhihirisha jinsi mashujaa wa ukombozi walivyojitolea kuung'oa ukoloni. Aidha, ulitathmini athari za mkoloni kwa mwanasiasa wa baada ya uhuru na jinsi athari hizi zilivyokinza maendeleo barani.

Kwa kuongozwa na nadharia ya Ulimbende, utafiti huu ulidhihirisha jinsi mwanasiasa wa Afrika alivyosawiriwa kiubunifu katika mashairi ya Kiswahili kama mhusika. Kwa upande mwingine, nadharia ya Baada-Ukoloni ilisaidia kumwagazia zaidi mwanasiasa wa Afrika sio tu kama mhusika wa kifasihi bali kama binadamu halisi katika mazingira halisi kiwakati na kihistoria katika muktadha wa uhusiano wake na mkoloni.

2.6 Hitimisho

Sura hii imejadili mwauo wa maandishi yaliyohusiana na utafiti wetu. Kazi mbalimbali zilichunguzwa kwa lengo la kudhihirisha mchango wake katika utafiti wetu. Ilibainika kuwa watafiti wa awali walipiga hatua muhimu katika utafiti wa kishairi, kihistoria na kisiasa ambao kwa kiasi ulihusiana na utafiti wetu. Hata hivyo, palihitajika utafiti ambao ungechunguza kwa kina nafasi ya ushairi wa Kiswahili katika uhifadhi wa historia ya mwanasiasa wa Afrika pamoja na udhihirishaji wa mabadiliko aliyopitia katika vipindi mbalimbali vya kisiasa. Aidha, misingi ya kinadharia ilibainishwa kwa lengo la kuupa utafiti wetu dira ya kitaaluma.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Katika sura hii, mbinu za utafiti zilizotumiwa katika utafiti huu zimejadiliwa kwa lengo la kudhihirisha eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli na uchanganuzi na uwasilishaji wa data. Kwa kubainisha eneo la utafiti, mtafiti amedhihirisha maktaba alizokusanya data yake iliyotosheleza mahitaji ya utafiti kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti. Sampuli iliyoteuliwa pia imebainishwa ili kuonyesha diwani zilizoteuliwa pamoja na mashairi yaliyohakikiwa. Hatimaye mtafiti amebainisha jinsi data iliyokusanywa ilivyochanganuliwa na kuwasilishwa baada ya utafiti kukamilika.

3.2 Eneo la Utafiti

Huu ulikuwa utafiti wa maktabani uliohusisha uhakiki wa kazi teule za kishairi. Utafiti ulitekelezwa katika maktaba za vyuo vikuu kadha nchini Kenya. Hivi ni pamoja na Chuo Kikuu cha Chuka, Methodisti, Egerton, Kenyatta na Nairobi. Mtafiti alidurusu kazi mbalimbali zilizohusiana na mada iliyotafitiwa pamoja ma misingi ya kinadharia. Kazi hizi ni pamoja na diwani zilizoteuliwa, tasnifu, majarida na magazeti mbalimbali. Mtafiti pia aliaua kazi mbalimbali zilizohusiana na mada ya utafiti kupitia kwa mtandao.

3.3 Uteuzi wa Sampuli

Kwa kuwa utafiti huu ulichanganua kazi za kishairi zilizomsawiri mwanasiasa wa Afrika kama mhusika, mbinu ya uteuzi wa kudhamiria ilitumiwa. Mashairi hayo yaliteuliwa kutoka kwa diwani zifuatazo: *Utenzi wa Uhuru wa Kenya*, *Sauti ya Dhiki*, *Chembe cha Moyo*, *Diwani ya Karne Mpya* na *Msimu wa Tisa*. Diwani hizi ziliteuliwa kutokana na misingi kwamba watunzi wa mashairi yaliyolengwa walizingatia sifa, vitendo na mabadiliko ya kisiasa na kimaadili ya mwanasiasa wa Afrika kabla ya uhuru, baada ya uhuru na kipindi cha siasa za vyama vingi.

Utenzi wa Uhuru wa Kenyani diwani yenye utenzi mmoja unaosimulia historia ya mwanasiasa wa Afrika katika muktadha wa upiganiaji wa uhuru nchini Kenya. Diwani hii iliusaidia utafiti huu kupata data kuhusiana na kipindi cha kabla ya uhuru. Nazo diwani za *Sauti ya Dhiki* na *Chembe cha Moyo* zina mashairi yanaoangazia jinsi baadhi ya viongozi wa kisiasa walioingia mamlakani mara tu mataifa ya Afrika

yaliyojinyakulia uhuru walivyobadilika kisiasa na kimaadili na kuusaliti umma, wakiongozwa na tamaa ya mali na ubinafsi. Kwa upande wake, mashairi yaliyomo katika *Diwani ya Karne Mpya* na *Msimu wa Tisa* yanamrejelea mwanasiasa wa Afrika katika kipindi cha siasa za vyama vingi. Kwa jumla, mashairi yaliyohakikiwa kutoka kwa diwani hizi yaliuwezesha utafiti huu kupata data kuhusiana na vipindi vilivyotafitiwa.

3.4 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa katika utafiti huu iligawanywa katika makundi matatu kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti. Kundi la kwanza lilijumuisha mashairi yaliyomsawiri mwanasiasa wa Afrika kabla ya uhuru. Mashairi haya yalihakikiwa kwa mujibu wa madhumuni ya kwanza ya utafiti. Madhumuni haya yalikuwa kuchunguzanafasi ya ushairi wa Kiswahili katika uhifadhi wa historia ya mwanasiasa wa Afrika kabla ya uhuru kwa mujibu wa ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu uliangazia sifa na vitendo vya mwanasiasa wa kipindi hiki kama kiongozi kielelezo aliyejitolea kupigania uhuru.

Kundi la pili lilikuwa na mashairi yaliyoangazia sifa za mwanasiasa wa Afrika baada ya uhuru. Kundi hili la mashairi lilinuiwa kudhihirisha mabadiliko aliyopitia mwanasiasa wa Afrika baada ya kuchukua uongozi kutoka kwa mkoloni kwa mujibu wa madhumuni ya pili ya utafiti. Utafiti huu ulibainisha jinsi mwanasiasa huyu aliutupilia mbali uzalendo na kuwa mkoloni mamboleo aliyewanyanyasa wananchi wenzake, hasa wakati wa mfumo wa siasa za chama kimoja.

Nalo kundi la tatu liliwasilishwa kwa mujibu wa madhumuni ya tatu ya utafiti. Kundi hili lilijumuisha mashairi yaliyoangazia mwanasiasa wa Afrika katika kipindi cha siasa za vyama vingi. Utafiti huu ulichukulia kuwa mfumo wa siasa za vyama vingi katika bara la Afrika ulitetewa kwa muda mrefu ili kuleta demokrasia kamili. Mashairi yaliyohakikiwa yalinuiwa kuonyesha iwapo mwanasiasa wa Afrika wa kipindi cha siasa za vyama vingi amebadilika na kuwa kiongozi bora akilinganishwa na yule wa kipindi cha siasa za chama kimoja. Hii ilitokana na ukweli kwamba wengi wa wanasiasa waliokuwa wapinzani wakuu wa siasa za chama kimoja ndio walioingia uongozini baada ya kusambaratika kwa mfumo huo.

3.5 Uwasilishaji wa Data

Uwasilishaji wa kinaelezo ulizingatiwa katika kuishughulikia data iliyokusanywa kuhusiana na mwanasiasa wa Afrika. Mtafiti aliyahakiki mashairi teule, kisha akatoa uamuzi wake kuhusiana na usawiri wa mhusika huyu kiubunifu, sifa na vitendo vyake, pamoja na kutathmini mabadiliko aliyodhihirisha katika vipindi mbalimbali vya kisiasa.

SURA YA NNE
TASWIRA YA MWANASIASA WA AFRIKA
KABLA YA UHURU

4.1 Utangulizi

Sura hii inaangazia historia ya ukombozi wa nchi ya Kenya chini ya aliyekuwa rais wa kwanza wa Jamhuri, marehemu Mzee Jomo Kenyatta kama ilivyopakidwa na Salim A. Kibao katika *Utenzi wa Uhuru wa Kenya*. Aidha, inasimulia jinsi Mzee Kenyatta pamoja na viongozi wenzake wazalendo walivyokamatwa, kuhukumiwa na kufungwa na wakoloni. Hatimaye inasimulia jinsi wazalendo hawa walivyowaongoza Wakenya kujinyakulia uhuru kutoka mikononi mwa wakoloni. Sura hii pia inaonyesha migogoro mbalimbali ya kisiasa iliyotokea wakati wa upiganiaji wa uhuru wa Kenya na jinsi vyama mbalimbali vya kisiasa vilivyochangia kuzuka kwa migogoro hii. Kufikia mwisho wa sura hii tunaona jinsi utenzi huu, ambao ulitungwa kati ya mwaka wa 1964 na 1966 na kuchapishwa 1972, unavyomsawiri mwanasiasa wa Afrika wa kipindi cha kabla ya uhuru kama mzalendo aliyejitolea kikamilifu kuupigania uhuru licha ya changamoto nyingi zilizomkabili. Usimulizi wa historia ya ukombozi wa Kenya pamoja na juhudi za wanasiasa katika kuafikia ukombozi huu unadhihirisha umuhimu wa ushairi wa Kiswahili katika uhifadhi wa historia. Madhumuni ya kwanza ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza nafasi ya ushairi wa Kiswahili katika uhifadhi wa historia ya mwanasiasa wa Afrika.

4.2 Uhifadhi wa Historia Kupitia Ushairi

Mshairi ameugawa utenzi huu katika sehemu nne ambazo zinarejelea hatua mbalimbali za kupigania uhuru. Sehemu hizi ni: Waafrika Wanaungana (kur.3-14), Hali ya Hatari (kur.15-26), Mikutano ya Uhuru (kur.27-53) na Uhuru na Baadaye (kur.54-75). Sehemu hizi zinaufanya utenzi huu kuwa na muwala. Msomaji anaweza kufuatilia visa vya ukombozi wa Kenya kwa utaratibu kutokea hatua za mwanzo za ukombozi hadi mwisho. Mpangilio huu pia unaupa utenzi huu upekee kwa kuwa unatoa taswira kamili ya wanasiasa wa kipindi cha kabla ya uhuru.

Kama ilivyo katika tenzi nyingi za kimapokeo, mtunzi anaanza utenzi huu kwa kuomba dua kwa Mola ili amjalie katika utenzi. Kisha mshairi anaeleza kusudi la utenzi wake ambalo ni kujadili jinsi siasa za Kenya zilivyoanza na jinsi zilivyoendelea. Katika ubeti wa pili wa sehemu ya dibaji, mtunzi anaonyesha dhima

ya ushairi wa Kiswahili kama chombo cha kuhifadhi historia ya nchi. Katika beti mbili zinazofuatia, mtunzi anaeleza kuwa amejitahidi alivyoweza kuwasimulia Wakenya jinsi alivyoweza kuhusiana na harakati za ukombozi wa taifa lao.

Kupitia beti hizi mshairi anaonyesha juhudi kuu alizofanya katika kuzikusanya na kuzihifadhi kumbukumbu hizi. Vilevile mtunzi anaonyesha kuwa habari alizokusanya ni muhimu kwa Wakenya; hivyo, zimemchukua muda kuzikusanya na kuzinakidi ili zieleweke waziwazi. Hili ni dhahirisho kuwa mshairi ni mwanajamii ambaye huongozwa na matatizo ya wakati anapotunga (Kezilahabi, 1976 na Thiong'o, 1981).

Katika ubeti wa 7, mshairi anaitetea hatua aliyoichukua ya kuifafanua historia ya nchi ya Kenya kupitia utenzi huu. Anasema kuwa hanuii kamwe kukashifu jambo lolote bali analenga kuyafafanua mambo jinsi yalivyotendeka. Hii inamaanisha kuwa mtunzi wa utenzi hachukui msimamo wowote wa kisiasa ama kwa kuunga mkono au kwa kupinga upande wowote.

Ubeti huo unadhahirisha kuwa ushairi wa Kiswahili unaweza kuhakikiwa kama kazi ya kifasihi iliyotumiwa kuhifadhi matukio halisi. Hali hii inadhahirika katika mshororo wa mwisho wa ubeti ulionukuliwa hapo juu ambapo mshairi anasema kuwa anataka kuyaweka mambo wazi jinsi yalivyotokea. Kwa hivyo, tunapoendelea kuuhakiki utenzi huu hatuna shaka yoyote kuwa tunarejelea historia muhimu na ya kuaminika kuhusiana na vita vya ukombozi wa taifa la Kenya. Katika sehemu inayofuata tutaangalia jinsi wazalendo wa Kenya walivyoungana na kukabiliana na mkoloni chini ya uongozi wa marehemu Mzee Jomo Kenyatta.

4.3 Taswira ya Viongozi Wazalendo

Utenzi huu ulichangia pakubwa katika uchunguzi wa sifa za mwanasiasa wa Afrika katika ushairi wa Kiswahili. Nadharia ya Ulimbwende ambayo iliongoza utafiti huu inasisitiza umuhimu wa kuwasawiri wahusika wa kishairi jinsi wanavyoweza kupatikana katika mahali na wakati halisi ulimwenguni. Kupitia sehemu ya kwanza ya utenzi huu, mshairi anaibua kumbukumbu za viongozi wazalendo waliopigania uhuru wa Kenya pamoja na changamoto walizopitia katika kutekeleza jukumu hili la kihistoria. Ubeti wa 15 unauwekea msingi usimulizi huu kwa kuashiria changamoto za mwanzo mwanzo katika harakati za upiganiaji uhuru. Mshairi anaanza usimulizi wake kwa maneno haya:

Sasa ndio ninaanza
 Wananchi kuweleza
 Zile taabu za kwanza
 Haliye ilivyokuwa

Ubeti huu unaashiria kwamba uhuru wa Kenya pamoja na mataifa mengine ya Afrika haukupatikana kwa urahisi bali ulihitaji juhudi kubwa. Juhudi hizo zilihitaji uzalendo mkubwa wa viongozi tangu hatua za mwanzo za upiganiaji uhuru. Hii ni kwa sababu vitendo vyovyote vya usaliti vingethiri ama kusambaratisha harakati hizi za kihistoria. Usaliti huu vilevile ungewavunja mioyo wananchi ambao walikuwa na matarajio makubwa kutoka kwa viongozi wao kama ilivyodokezwa na Kinyatti (1992).

Umuhimu wa kuwakumbuka viongozi wazalendo ni jambo lingine muhimu linalosisitizwa na utenzi huu. Katika beti za 16 na 17 mshairi anawataja wazalendo hawa kama viongozi wa hakika. Kwa mujibu wa mshairi, lau wazalendo hawa wasingejitolea uhuru tunaojivunia sasa usingekuwapo. Aidha, uvumilivu mkubwa ulihitajika; jambo ambalo linamfanya mshairi kuwapamba wazalendo hawa kwa maneno haya:

16
 Lazima kuwakumbuka
 Viongozi wa hakika
 Uhuru waloutaka
 Nao wakatuletea

17
 Tabu walizopata
 Uhuru kuutafuta
 Halafu wakaupata
 Sote tukafurahia

Inadhihirika hapa kuwa viongozi wa kipindi cha upiganiaji uhuru hawakuwa na ubinafsi kwani juhudi zao za kupigania uhuru ziliufaidi umma kwa jumla. Hawa ni tofauti na baadhi ya wanasiasa wa kipindi cha baada ya uhuru ambao walinyakua mali ya ummakama inavyodokezwa na Kelly (2014). Mtafiti huyu amebainisha jinsi baadhi ya wanasiasa wa Afrika walivyojilimbikizia utajiri huku wakificha fedha walizoiba kutoka kwa benki na taasisi nyingine za kifedha katika mataifa ya kigeni. Aidha, mshairi anaonekana kuwashangilia viongozi wa kabla ya uhuru kwa niaba ya umma anaposema kuwa uhuru ulipopatikana sote tulifurahia.

Juhudi za viongozi wazalendo zinazidi kujitokeza, hususan katika ubeti wa 19, ambapo mshairi anaonyesha jinsi viongozi hawa hawakuridhishwa na uvamizi wa

wakoloni. Mshairi anadhihirisha jinsi wazalendo walivyoanza kujikusanya ili kutafuta juhudi za kuwaondoa wakoloni. Ubeti huu unasema hivi:

19

Wakaanza kukutana
Makamo na wavulana
Mawazo kila namna
Nchi kuifikiria

Katika ubeti huu, tunaona suala la ushirikiano likidhihirika, tofauti na ilivyo katika kipindi cha siasa za vyama vingi ambapo baadhi ya viongozi wanawadharau wenzao kwa kigezo cha umri. Kabla ya uhuru, uzalendo wa wanasiasa haukukinzwa kamwe na tofauti za umri wala tabaka. Tunaona kuwa watu wazima kwa vijana walianza kukutana na kuweka mawazo yao pamoja ili kuikomboa nchi. Hili ni dhihirisho kuwa watu hawa walikuwa na nia moja tu – ile ya kujinyakulia uhuru – ambayo walitimiza kwa kuongozwa na sifa zilizojadiliwa hapa chini.

4.3.1 Uwajibikaji kwa Umma

Uwajibikaji wa wanasiasa katika mazungumzo yao ni jambo muhimu linalojitokeza katika utenzi huu. Matamshi ya viongozi wakati wa kupigania uhuru yaliheshimiwa mno kwani kiongozi yeyote alikadiria athari za maneno yake kwa umma kabla hayajitamka. Kufikia ubeti wa 20, uongozi wa Mzee Kenyatta unianza kujitokeza. Hili linatokea baada ya Mzee Kenyatta kupata habari kuhusu wazalendo waliokuwa wameanza kukutana ili kupanga mikakati ya kujipatia uhuru. Mzee Kenyatta anajitokeza hapa kama kiongozi shupavu anayewazia kila neno kabla hajalitamka. Hebu tuangalie beti tatu zifuatazo:

20

Mzee wetu Kenyatta
Habari alizipata
Wala haukumpita
Naye akahudhuria

21

Ndipo alipoinama
Mawazo akayapima
'Neno gani nitasema
Litakalokuwa sawa?'

Beti hizi zinaonyesha kuwa juhudi za kupigania uhuru zilihitaaji uongozi wa busara. Tunaona kuwa Mzee Kenyatta alikuwa mwangalifu katika usemajji wake kwani hakusema jambo lolote ambalo lingezua taharuki au kutatiza juhudi za ukombozi. Ni dhahiri katika ubeti wa 21 kuwa kiongozi huyu alilipima kila neno kabla ya kulitamka na pia aliwajibika katika unenaji wake.

Kuwajibika katika unenaji kunathibitishwa katika ubeti wa 22 ambapo tunaona kuwa baada ya kufikiri na kuyapima maneno yake Mzee Kenyatta aliinuka na kuwahutubia waliokusanyika. Mshairi anasema kuwa Mzee Kenyatta hakuwa na shaka kamwe na maneno aliyoyasema. Mshairi ananakili:

22

Halafu akainuka
Maneno akatamka
Ambayo hayana shaka
Wananchi kuwambia

Ni dhahiri pia kuwa Mzee Kenyatta alitangamana vyema na umma. Hali hii inaweza kuthibitishwa kuanzia ubeti wa 23 ambapo wananchi wanamwandama Mzee Kenyatta kwa maswali punde tu anapowatangazia umuhimu wa kupigania uhuru. Hebu tuutazame mjadala unaofuatia:

23

Mzee alotamka
'Uhuru wetu twataka
Nchi yetu kuishika
Bila wageni kungia'

24

Ndipo watu wakaanza
Maswali kumuuliza
Ili apate weleza
Na kuwaonyesha njia

Mjadala huu unadhihirisha kuwa viongozi waliwajibika kwa umma kwani umma usingekubali kamwe kupewa ahadi za uwongo. Ni dhahiri pia kuwa uhusiano wa viongozi na umma ulikuwa mwema kwani walijadiliana nao juu ya masuala yaliyowakabili kabla ya hatua zozote kuchukuliwa. Wananchi pia walikuwa huru kuwauliza viongozi maswali pale walipokuwa na shaka. Kwa mfano, katika ubeti wa 25 wananchi wanamtaka Mzee Kenyatta kuwaeleza jinsi angeweza kuwaondoa wabeberu na hatimaye kuwawezesha kupata uhuru. Wananchi wanamsaili hivi:

25

'Jambo gani utafanya
Wabeberu kuwaonya
Kutoa uhuru Kenya?
Bwana utatuambia

Uwajibikaji unaojitokeza katika ubeti huu ni wa hali ya juu. Hata hivyo, kiwango hiki cha uongozi kilielekea kushushwa na baadhi ya viongozi wa kipindi cha siasa za vyama vingi ambao walijipata taabani kwa kutoa matamshi yaliyozua chuki na utengano katika jamii.

Ili kukabiliana na maswali ya umma uliokuwa na ari ya kupata uhuru, palihitajika viongozi wenye akili pevu. Mzee Kenyatta anasawiriwa kama mnenaji bora na kiongozi mwenye busara. Katika beti zifuatazo, Kenyatta anaanza kuyajibu maswali ya umma bila kutatizika:

26
Ndipo kuanza kujibu
Kwa haraka bila tabu
'Mambo yote taratibu
Nitaanza kuwambia'

27
'Fimbo yake mbeberu
Ili tupate uhuru
Ni kumtia kukuru
Apate kutuachia'

Mshairi anaonyesha hapa kuwa kiongozi huyu hakuwa mnenaji tu bali pia alikuwa na mikakati mwafaka ya kumwondoa mkoloni. Hili ni dhihirisho kuwa ili kupatikana uhuru katika bara la Afrika palihitajika viongozi wenye vitendo wala sio wapayukaji tu. Mshairi anaonyesha kuwa viongozi walihitajika kumchunguza mkoloni kwa makini ili wapate mbinu mahsusi za kumwondolea mbali. Mzee Kenyatta anasawiriwa kama kiongozi aliyejua vyema siri ya kuuangamiza ukoloni. Siri yenyewe ilikuwa kumpiga vita mkoloni, kama inavyodhihirika katika ubeti wa 27 tuliounukuu hapo juu.

Mzee Kenyatta pia aliamini kuwa uhuru usingalipatikana iwapo wananchi wanalitengana na pia kukosa kujitolea. Kwa hivyo, alijitokeza kama kiongozi muunganishaji, kama inavyodhihirika katika beti zifuatazo:

28
'Jambo kubwa kuungana
Akaanza kueleza
'Ile hatua ya kwanza
Tujiweke sawa sawa.'

33
Bila ya kubaguana
Kwa wazee na vijana
Mbeberu kumpaza
Ni watu kujitolea.'

Kupitia beti hizi tunaona kuwa viongozi wa kipindi cha kabla ya uhuru waliwahusisha wananchi katika hatua mbalimbali za kumwondoa mkoloni. Sio Mzee Kenyatta tu aliyewahusisha wananchi katika upiganiaji uhuru bali pia viongozi waasisi wa mataifa ya Uganda na Tanzania, yaani Milton Obote na Mwalimu Julius Nyerere mtawalia waliendeleza moyo huo. Hatua hii ya kuwaunganisha watu na pia kuwaomba ushauri ili wafanya viongozi hawa kupata umaarufu miongoni mwa wananchi. Katika ubeti wa 37 tunaona wananchi wakikubaliana kwa kauli moja kuwa Mzee Kenyatta ndiye aliyefaa kuwaongoza:

37

Baada ya hayo kupita
Wananchi wakakata
'Ni wewe Bwana Kenyatta
Uongozi kuchukua.'

Ubeti huu unaonyesha kuwa wananchi hawakushurutishwa kuwakubali viongozi wao bali ni uhusiano mzuri kati ya viongozi na wananchi uliowapa viongozi hao umaarufu. Kutokana na hali hii, wananchi walipata imani kamili kuhusiana na viongozi wao na hivyo kuamini kuwa ndio waliofaa kuwaondoa utumwani wa kikoloni. Katika beti za 38 na 39 wananchi wanakiri hivi kuhusiana na uongozi wa Mzee Kenyatta:

38

'Ni wewe ndiwe wa kwanza
Sote tutakusikiza
Sasa utatuongoza
Utumwani kututoa'

39

'Twataka utuongoze
Wabeberu tufukuze
Na uhuru ueneze
Dunia ipate jua.'

Beti hizi ni ushahidi kuwa viongozi wa kipindi cha kabla ya uhuru hawakujipendekeza kamwe kwa wananchi. Ni wananchi wenyewe waliojiamulia aina ya viongozi waliofaa kutekeleza majukumu yaliyokuwepo wakati huo, kinyume na uongozi wa baada ya uhuru. Katika siasa za vyama vingi, uongozi umejaa ushindani na ubinafsi kama inavyodhihirishwa na Njogu (2004) na Kanyinga, Long & Ndi (2008). Aidha, wataalamu hawa wanashikilia kuwa ubinafsi wa wanasiasa mara nyingi huzua uongozi wa kidikteta. Uongozi wa aina hii huuathiri umma kisiasa, kiuchumi na kijamii.

4.3.2 Uongozi wa Kidemokrasia

Uongozi wa kidemokrasia ulioendelezwa na wapiganiaji uhuru unadokezwa na maoni ya Mzee Kenyatta katika beti za 41 na 42. Mzee Kenyatta anasema kuwa angependa kamati zichaguliwe upesi punde atakaposhikilia uongozi na kutaja sifa za wanakamati waliofaa kuchaguliwa. Anawataka wananchi wawachague wanakamati ambao ni shupavu, wervevu na wenye bidii. Hebu tuyatazame maneno halisi ya Mzee Kenyatta kwa mujibu wa mshairi:

41

Kenyatta akatamka
 ‘Uongozi nitashika
 Kamati nitazitaka
 Upesi kuchaguliwa’

42

‘Tuchague washupavu
 Tena walio werevu
 Wasiwe ni walegevu
 Utumwa tutaondoa’

Beti hizi zinaonyesha kuwa sio tu viongozi wakuu waliohitajika kuwa na sifa maalum. Hata viongozi wa mashinani, ambao katika muktadha huu wanatambuliwa kama wanakamati, walihitajika kuwa viongozi waadilifu. Viongozi hawa hawakuchaguliwa kwa misingi ya kikabila wala miegemeo yao ya kisiasa kama ilivyobainika katika kipindi cha baada ya uhuru. Usawiri huu wa viongozi unawaakisi wanasiasa kama wanavyoweza kujitokeza katika mazingira halisi kwa mujibu wa wakati na mahali, kama inavyobainishwa na nadharia ya Ulimbwende. Aidha, lugha ya ushawishi iliyotumiwa na Mzee Kenyatta pia inadhahirisha nafasi ya lugha kama nyenzo ya Mwanasiasa wa Afrika ya kuchochea uzalendo, kupinga ubinafsi, kuondoa chuki na hatimaye kujenga jamii mpya.

4.3.4 Ujasiri

Sifa nyingine muhimu iliyowatambulisha wanasiasa wa kipindi cha kabla ya uhuru ni ujasiri. Mzee Kenyatta anamlinganisha mkoloni na simba mkali anayeweza kuwarukia wapiganiaji uhuru. Licha ya ukali huu, Kenyatta anajitolea kumshika simba huyu mkiani na kuwashawishi wapiganiaji uhuru wenzake kutomkimbia kamwe. Matamshi ya kijasiri ya Mzee Kenyatta yanapatikana katika ubeti wa 44 na kuendelezwa katika ubeti wa 45:

44

Kenyatta akawambia
 ‘Nimshikapo mkia
 Simba atawarukia
 Msije kumkimbia’

45

‘Hili sio jambo dogo
 Ni zito kushinda gogo
 Wabeberu si kidogo
 Wengine watatujia’

Mshairi hapa anamlinganisha mkoloni na simba mkali kwa lengo la kuonyesha kuwa juhudi za kupigania uhuru zilihitaaji ujasiri kwa upande wa wapiganiaji uhuru. Mpiganiaji uhuru hapa anasawiriwa kama mwindaji wa simba. Ujenzi wa taswira katika ushairi ni mbinu muhimu ya uwasilishaji wa maudhui inayosisitizwa na nadharia ya Ulimbwende ambayo iliongoza utafiti huu. Mbinu hii hulinganisha kitu na kitu kingine moja kwa moja.

Taswira hii ya kumshika simba mkiani inaonyesha kuwa palihitajika viongozi waliojitolea mhanga kiasi cha kuhatarisha maisha yao ili uhuru wa mataifa ya Afrika uweze kupatikana. Mzee Kenyatta mwenyewe anakiri wazi kwamba hili halikuwa jambo dogo kwani wabeberu hawangeweza kuondolewa bila kujipigania; bila shaka kwa kutumia silaha kali kuliko zile za wenyeji.

Mwanasiasa wa kabla ya uhuru pia anasawiriwa kama kiongozi mpatanishi. Sifa hii inajitokeza kupitia juhudi za Mzee Kenyatta za kutembelea maeneo mbalimbali ya Kenya akisikiliza maoni ya wananchi na pia kuwahimiza washirikiane ili kumwondoa mkoloni. Katika ubeti ufuatao tunayapata maneno yake akiwazungumzia wazalendo wa Pwani:

51

Mzee akatamka
'Umoja tunautaka
Kamba moja kuishika
Kwa pamoja sote pia'

Maneno haya yanaonyesha kuwa wanasiasa wa kabla ya uhuru hawakutaka kusifiwa kwa kumwondoa mkoloni. Badala yake walitaka upatikanaji wa uhuru uonekane kama juhudi za pamoja zilizofanywa na wazalendo. Mshairi, ambaye anachukuliwa na utafiti huu kuwa anazungumza kwa niaba ya wananchi, anawasifu wanasiasa hawa kwa unyenyekevu wao. Jambo hili linaudhihirisha ushairi wa Kiswahili kama utanzu muhimu wa fasihi unaotumiwa kuwasifu viongozi wema kama inavyosisitizwa na King'ei na Kemoli (2001).

4.3.5 Uangalifu na Kuheshimika

Viongozi waliopigania uhuru pia walikuwa na sifa ya uangalifu. Mara kwa mara Mzee Kenyatta aliwaelimisha wananchi kuhusu athari za ukoloni huku akiwatahadharisha dhidi ya tabia ambazo zingekinza upatikanaji wa uhuru. Kati ya mambo ambayo Mzee Kenyatta alipinga vikali ni uvivu na ukabila. Katika beti zifuatazo tunamwona akiwahimiza wananchi kuyatafakari yajayo na kuikabili hatari iliyowakabili:

66

'Mbeberu kazunguka
Kila kitu ameshika
Sasa hataki kutoka
Mali yetu ajilia'

67

'Na wenyewe tumelala
Bora kupata chakula
Na kupenda ukabila
Na mengineyo mabaya'

68

‘Yataka tuyafikiri
Tuyakate mashauri
Tuangalie hatari
Mbele inayotujia’

Kupitia kwa maneno haya tunaona kuwa Mzee Kenyatta hakutaka wananchi wajihusishe na tabia na vitendo ambavyo vingewafanya baadhi yao kupuuza umuhimu wa kupata uhuru. Aidha, aliwataka wananchi kuwa macho ili kuweza kukabiliana na upinzani wowote ambao ungepunguza kasi ya kujinyakulia uhuru.

Uangalifu wa wanasiasa wa kabla ya uhuru uliwafanya kuheshimiwa na umma. Katika beti zifuatazo, tunashuhudia wananchi wakimsikiliza Mzee Kenyatta kwa makini na kuyatilia maanani maneno yake ya busara:

69

Na watu wamenyamaza
Kwa makini wasikiza
Maneno ya muangaza
Akilini yawangia

70

Tena akasema sana
Maneno yenye maana
Na wote wanamuona
Na huku wametulia

Ushahidi wa kuheshimika kwa viongozi wa kabla ya uhuru tunaopata hapa unawasawiri viongozi waliojali waliyoyasema. Viongozi hawa waliwazia kwa makini athari za kauli walizotoa, na kwa jinsi hii walizuia madhara yake kwa umma. Jambo hili linadhihirisha ukomavu wa kisiasa uliokuwepo wakati huo. Makillah (2009) anawasawiri wanasiasa wa baada ya uhuru kama watu waliojaa jeuri, kiburi na dharau. Kumekuwa na visa vingi ambapo mikutano ya wanasiasa wa wakati huu imeishia kwa vurugu kutokana na uchochezi unaozuliwa na wanasiasa na kusababisha uhasama wa kikabila.

Miaka ya hivi punde, taifa la Kenya limeshuhudia viongozi ambao wamekuwa wakitumia fursa yoyote kutoa matamshi ya uchochezi; baadhi yao wakinukuliwa katika vyombo vya habari wakitumia lugha ya matusi hadharani na hata bungeni. Iwapo viongozi wa kabla ya uhuru wangetumia lugha kama hii wangepoteza hadhi kuu waliyopewa na umma na hatimaye kutatiza juhudi za kupigania uhuru.

Ili kuhakikisha kuwa sera zake za kisiasa ziliungwa mkono na umma, Mzee Kenyatta aliwashirikisha wananchi katika uundaji na uimarishaji wa chama cha kisiasa cha

Kenya African Union. Katika safari yake mkoani Pwani Mzee Kenyatta aliwambia wazalendo hivi:

73

‘Hicho chama jina lake
Ni KAU ufupi wake
Na nyinyi mkikumbuke
Bila ya kuwapotea.’

74

Sasa mpange kamati
Msipoteze wakati
Pamoja na wenyeviti
Hapana cha kungojea.’

Hapa tunaona kuwa suala la uundaji na uimarishaji wa vyama vya kisiasa halikuwa shughuli ya mtu mmoja au kundi dogo la watu kama tunavyoshuhudia sasa. Ushindani wa wanasiasa kupitia vyama vya kisiasa haukuwa umeanza kushuhudiwa katika bara la Afrika. Kwa hivyo, kuanzishwa kwa chama cha KAU kulichukuliwa na wananchi kama hatua mojawapo muhimu ya kufikia upatikanaji wa uhuru. Hii ni kinyume na jinsi mambo yalivyobadilika baadaye ambapo wanasiasa walianza kuwashurutisha wananchi kuingia katika chama cha kisiasa, kama anavodokeza Skinner (2010). Moyo wa kushauriana na wananchi uliwafanya viongozi wa kabla ya uhuru kuheshimiwa na umma.

Ni kutokana na kuheshimika huku ambapo Mzee Kenyatta alisikizwa kila alikoenda. Isitoshe, wananchi hawakupuuza kamwe alipowatahadharisha dhidi ya tabia na vitendo vya vibaraka ambao wangetishia juhudi za kupatikana kwa uhuru. Hili ni dhihirisho kuwa palihitajika viongozi waliokuwa na uwezo wa kuona mbali na kuuhamasisha umma. Katika beti zifuatazo tunamuona Mzee Kenyatta akiweka bayana tahadhari hii:

76

Mzee akatamka
Kabla ya kuondoka
‘Kutakuja vibaraka
Ili kuwaharibia.’

77

‘Na wao watakazana
Kuiingiza fitina
Na nyinyi mtawaona
Mtakuja kunambia.’

Beti hizi pia zinaonyesha imani kubwa ambayo wananchi walikuwa nayo kwa viongozi wao wakuu. Katika ubeti wa 77 ambao tumenukuu hapo juu tunamwona Mzee Kenyatta akiwaambia wananchi kuwa wangukuja kumwambia juu ya fitina ambayo ingetokana na vibaraka. Hii inadhihirisha jinsi wananchi walivyomheshimu Mzee Kenyatta na pia kuwasiliana naye kuhusu masuala yoyote ambayo walihisi kuwa yalienda kinyume na lengo lao kuu - kujinyakulia uhuru.

Mawasiliano haya mema hayakutatizwa na mipaka ya kijiografia ama kikabila. Mzee Kenyatta alikaribishwa katika maeneo mbalimbali aliyotembelea na kuhamasisha umma juu ya umuhimu wa kuupigania uhuru. Kwa mfano, alipoenda Kisumu alipokelewa vyema na wananchi ambao walimngoja, kama inavyohibitishwa katika ubeti huu:

79

Alipofika Kisumu
Akawakuta timamu
Wananchi wametimu
Tayari wamngojea.

Ubeti huu unaendelea kusisitiza umaarufu ambao Mzee Kenyatta alipata katika taifa zima. Umaarufu wa aina hii ulivurugika baada ya uhuru ambapo visa vya utovu wa nidhamu vimeshuhudiwa katika mataifa kadha ya Afrika ambapo baadhi ya wanasiasa huwachochea wananchi kuwashambulia wapinzani wao wanapoyazuru maeneo waliyo na umaarufu. Uhasama huu hutokea katika mikutano ya kisiasa, shughuli za kitamaduni, kidini na kwenye matanga.

Ushahidi zaidi wa kukubalika kwa Mzee Kenyatta kama kiongozi wa taifa unapatikana katika beti zifuatazo. Aidha, tunaona wananchi wakikubaliana na mawazo ya Mzee Kenyatta bila ubishi wowote. Mshairi anasema hivi:

81

Wakati alipofika
Watu wamekusanyika
Na alipotemka
Wote wakampokea

82

Ndipo watu kumwambia
'Tumekwisha kusikia
Njia uliyotumia
Twakubali sote pia.'

Makaribisho haya yanaashiria jinsi wananchi walivyokuwa na hamu ya kupata uhuru. Aidha, viongozi wao hawakupoteza muda kuwanenea mambo ambayo hayangewaelekeza katika upatikanaji wa uhuru. Mshairi anasema kuwa baada ya kuwasiliana vyema na wenyeji wa Kisumu Mzee Kenyatta hakukawia pale bali alielekea Nairobi. Huko alipata makaribisho mahususi kama tunavyoona katika ubeti ufuatao:

86

Nairobi akafika
Kwa furaha na kucheka
Wakati aliposhuka
Watu wanamngojea.

Makaribisho haya ni ishara kwamba wakati wa kupigania uhuru wananchi hawakuwa wamegawanyika katika misingi ya kikabila kama ilivyotokea baada ya uhuru. Mzee Kenyatta hakuchukuliwa kama kiongozi wa kabila au eneo lolote bali alikubalika kama kiongozi wa kitaifa. Siku hizi ni nadra sana kwa kiongozi wa kisiasa kupata makaribisho ya aina hii kote nchini. Mara kwa mara wanasiasa hukumbana na upinzani kwa misingi ya kikabila au vyama vya kisiasa. Vyama vingi vya kisiasa pia vimeundwa kwa misingi ya kikabila (Gachukia, 2005).

Kukubalika kwa Mzee Kenyatta kote nchini kunajitokeza vyema katika utenzi huu. Tunaona wananchi wa Nairobi wakimuunga mkono katika juhudi zake za kuwafikia wazalendo wa Ukambani. Mazungumzo yafuatayo ni thibitisho kamili la wazo hili:

87

Akawaambia, 'Jamani
Nimezunguka nchini
Imebaki Ukambani
Sasa nitawaendea.'

Mzee Kenyatta alipowatajia wenyeji wa Nairobi wazo la kwenda Ukambani, ilionekana wazi kuwa tayari ujumbe ulikuwa umewasilishwa kwa wenyeji wa huko. Mazungumzo yaliendelea hivi:

88

Na wao wakamjibu
'Ipunguze hiyo tabu
Ukambani ni karibu
Tumekwisha kuwambia.'

Mazungumzo haya yanaonyesha jinsi wanasiasa wa kipindi cha kabla ya uhuru waliwashirikisha wananchi katika shughuli za uongozi, hususan kupitia uenezaji wa habari. Pia yanabainisha kuwa kulikuwa na kuaminiana kati ya viongozi na umma. Kasumba ya tabaka tawala kuonekana likiliamulia tabaka tawaliwa kila kitu haikuwa imekita mizizi kama ilivyo katika kipindi cha siasa za vyama vingi.

4.3.6 Uadilifu

Sifa ya uadilifu inajitokeza katika utenzi huu ambapo tunamwona Mzee Kenyatta akiwa na madhumuni ya kutekeleza maendeleo kila alikoenda kwa ushirikiano na umma. Uadilifu huu ndio uliomfanya kujikita katika shughuli za ukombozi bila kujitakia makuu kama walivyofanya baadhi ya viongozi wa baada ya uhuru. Alipozuru maeneo ya Ukambani (ubeti wa 93-103), Mkoa wa Kati, ama nyumbani kama anavyoita mshairi (ubeti wa 104- 108) na Mkoa wa Bonde la Ufa, ambako mshairi anataja kama Masaini na Kalenjini (ubeti wa 109- 127) hakupata upinzani wowote. Wananchi walikubaliana na mawazo yake ya ukombozi. Katika ubeti wa 128 tunaona jinsi Mzee Kenyatta alivyofanya kila jambo kwa uadilifu popote alipoenda:

128

Namna alivyokuta
Muheshimiwa Kenyatta
Hakuyafanya matata
Kazini aliingia.

Mtindo huu wa kiuongozi ni tofauti kabisa na ule wa baada ya uhuru ambapo baadhi ya wanasiasa walipoteza muda mwingi wakieneza propaganda badala ya kuzingatia masuala muhimu ya kimaendeleo. Kama anavyodokeza Makillah (2009) wengi wa viongozi wa wakati huu hulenga kujinufaisha katika vitendo vyao vingi badala ya kulenga kujenga nchi zao.

Ili kuthibitisha umuhimu wa uadilifu katika uongozi, Mzee Kenyatta aliwaonya wananchi dhidi ya tabia za baadhi ya wanasiasa wanafiki. Mshairi anadokezea hapa jinsi ufisadi wa kisiasa ulivyopenyeza katika mataifa ya Afrika hata kabla ya uhuru kupatikana. Mzee Kenyatta anasema hivi kuhusiana na wanasiasa wafisadi:

129

Alianza kuwambia
'Vibaraka watangia
Kuzivunja zenu nia
Ili tupate potea.'

130

Watu hao vibaraka
Wataanza kuzunguka
Na pesa watazishika
Wapate tuvurugia.'

Lengo la Mzee Kenyatta hapa lilikuwa kuwatahadharisha wananchi dhidi ya wanasiasa walionuia kukiangusha chama cha KAU ambacho alitaka kukitumia kama chombo cha kisiasa cha ukombozi. Onyo hili lilizaa matunda kwani wananchi walipata chombo cha kuwaleta pamoja kama inavyobainika katika ubeti huu:

137

Siasa ziliposhika
Kwa taabu na mashaka
Na zikawajaa hakika
Mwisho walijitolea.

Mshairi hapa anadokeza kuwa ili kupatikana kwa uhuru palihitajika wanasiasa ambao hawangechelea upinzani kutoka kwa wabeberu pamoja na vibaraka wao. Vitendo vya kisaliti, ikiwa ni pamoja na matumizi ya pesa ili kuvuruga juhudi za upiganiaji uhuru, vimefafanuliwa katika ubeti wa 139 hadi 141 ambapo mshairi anasema hivi:

139

Beberu na vibaraka
Fitina wakazipika
Kenya wakaizunguka
Sumu yao kuitia

140

Wakatoa na mapesa
Nairobi na Mombasa
Kuzichafua siasa
Kwa umoja kupotea

141

Wakapita kila njia
Wananchi kuwambia
Wapate geuza nia
Siasa kuziachia

Beti hizi tatu zinadhihirisha jinsi hongo na ufisadi katika siasa vilianzia hata kabla ya uhuru kupatikana katika baadhi ya mataifa ya Afrika. Visa vya wabunge kuhongwa na wanasiasa wenzao ili kubadilisha msimamo wao kuhusiana na masuala yenye umuhimu wa kitaifa si vigeni hapa Afrika. Kwa mfano, Hamisi (2011) amefichua jinsi baadhi ya wabunge katika bunge la tisa la Kenya walikuwa wakihongwa na upande wa serikali au upinzani na kupiga kura bungeni kinyume na walivyoniua hapo awali. Ufisadi huu uliathiri pakubwa jinsi uafikiaji wa maamuzi muhimu ya kitaifa ulivyoafikiwa bungeni. Tofauti na wanasiasa wa wakati huu, Mzee Kenyatta na wenzake hawakubatilisha kamwe msimamo wao wa kupigania uhuru licha ya ufisadi wa wakoloni na vibaraka wao.

4.4 Mashujaa Wengine wa Ukombozi wa Kenya

Uwezo wa ushairi wa Kiswahili katika uhifadhi wa matukio ya kisiasa barani Afrika kama alivyotambuliwa na Simala (2004) unathibitishwa katika sehemu hii. Hapa

tunaona jinsi utanzu huu unaweza kuchunguzwa kama historia ya utangamano wa wakoloni na jamii ya Waafrika na kati ya fasihi na siasa.

Aidha, usawiri wa wanasiasa wa kipindi cha kabla ya uhuru kama wahusika katika utenzi huu unathibitisha mhimili muhimu wa nadharia ya Ulimbende ambayo iliongoza utafiti huu. Nadharia hii inashikilia kuwa ushairi unafaa kuwasawiri wahusika katika uhalisia wao ili waweze kuziakisi hali za mazingira kwa mujibu wa wakati. Wanasiasa wanaorejelewa katika sehemu hii waliwahi kuishi na pia mtunzi ametumia majina yao halisi katika utenzi huu.

Mshairi ameinakidi historia ya unyanyasaji wa kikoloni na juhudi zilizofanywa na wanasiasa wa kipindi cha kabla ya uhuru kuumaliza unyanyasaji huu. Vilevile, mshairi amejadili baadhi ya changamoto zilizowakumba wanasiasa hawa, ikiwa ni pamoja na kutiwa kizuizini na kuteswa kwa wazalendo hao wakiongozwa na Mzee Kenyatta na wenzake watano. Mshairi hapa anathibitisha kauli ya Kinyatti (1992) kwamba mfumo wa serikali ya kikoloni haukuwa na nia yoyote ya kuwafaidi Waafrika bali uliendeleza unyakuzi wa rasilmali na hivyo kuzua haja ya kuukomesha.

Kwa kutumia mtindo wa kisimulizi, mshairi anatusawiria hatua kwa hatua vitendo vya unyanyasaji vilivyochochea hatua za kishujaa zilizochukuliwa na wanasiasa wa kabla ya uhuru ili kuwakomboa Wakenya. Udhihirishaji wa hisia za wananchi unaofanywa na mtunzi unaungwa mkono na mawazo ya Mohamed (2002) anaposema kuwa yeye kama mtunzi huzingatia dhiki, raha, furaha, shida, uvumilivu na hata kukata tamaa miongoni mwa mwanajamii. Wamitila (2002) pia anautaja ukombozi wa wanyonge kama maudhui ambayo hujitokeza sana katika ushairi wa Kiswahili. Kwa upande mwingine, Nadharia ya Ulimbende ambayo iliongoza utafiti huu inashikilia kuwa ushairi unafaa kutumiwa kutolea hisia za watu kuhusiana na masuala mbalimbali yanayowasibu maishani.

Katika ubeti ufuatao tunaona jinsi hisia za Wakenya zilivyoanza kuathiriwa na ubaguzi ulioshuhudiwa mara tu watu walipoanza kujipanga katika vikundi vya kikabila na kitabaka nchini Kenya. Hapa palizuka matabaka matatu ya watu; Wazungu, Wahindi na Waafrika. Wazungu na Wahindi walikuwa wakijipatia

mishahara mikubwa mikubwa huku Waafrika wakiumia, kama ilivyopakidwa katika ubeti ufuatao:

155

Wahindi pia Wazungu
Walijipanga mafungu
Mishahara chungu chungu
Wananchi waumia

Ubaguzi wa aina hii haukujitokeza Kenya pekee bali pia uliathiri wananchi wa koloni jirani za Uganda na Tanzania kama anavyosema Atieno na wenzake (1977). Utabaka huu uliwaudhi wanasiasa wa Afrika wa wakati huo na kuwatia ari ya kujikomboa.

Wanasiasa wakiwa bado wanatafakari juu ya athari za utabaka, mashamba mazuri yalianza kunyakuliwa na walowezi. Unyakuzi huu uliwaudhi viongozi hawa na kuwafanya kuongoza harakati za kuyakomboa mashamba yaliyokaliwa na walowezi. Waafrika wengi waliopinga unyakuzi huu walitiwa kizuizini, jambo ambalo liliwaudhi zaidi wanasiasa na wananchi wazalendo kwa jumla. Vita vilizuka kati ya walowezi na wananchi. Vita hivi viliongozwa na kundi la mashujaa lililojulikana kama Mau Mau. Mshairi anafafanua masuala haya katika beti zifuatazo:

156

Waliokuwa shambani
Na walioko mijini
Walikuwa mashakani
Hakika ninawambia

157

Mashambani wakaanza
Matata kuyachokoza
Wazungu kuwafukuza
Wapate kuyakimbia

Tunaona hapa kuwa wanasiasa wa kabla ya uhuru hawakuwa viongozi wa kuketi tu na kutazama wananchi wakiumizwa na ukoloni. Badala yake walichukua hatua na kujitolea bila kushurutishwa wala kutarajia malipo yoyote. Ushujaa wao unadhihirika hapa kwani walipigana na wakoloni ambao bila shaka walikuwa na silaha kali zaidi na hata ujuzi wa vita ulioupiku ule wa Waafrika. Katika beti zifuatazo mshairi anatumfufanulia misukosuko iliyofuatia hali ya hatari ilipotangazwa nchini Kenya:

158

Matata yaliposhuka
Kenya ikasukasuka
Ikawa ni pata shika
Na watu wakapotea

159

Watu wengi wakashikwa
Nyayani wakenda wekwa
Mwahali musipofikwa
Hata kwa kuangalia

160

Ndiyo vita kuenea
Mau Mau kuingia
Na wengi wakapotea
Lakini hapana njia

Misukosuko iliyoelezwa hapa inawasawiri wanasiasa wa kipindi cha kabla ya uhuru kama watetezi madhubuti wa haki za wanyonge. Kupitia uundaji wa kikundi cha Mau Mau, wanasiasa hawa pia wanadhahirika kama viongozi waliokuwa na mikakati mahususi ya kupambana na wakoloni. Aidha, mshairi amewasawiri kama mashujaa wasiotetereka wala kutishwa na mbinu za mkoloni za kuwakandamiza. Mbinu hizi ni pamoja na kuwapiga wazalendo, kuwatia kizuizini na hata kuwaua. Mbinu hizi zilinuiwa kuhakikisha kuwa wakoloni wangebaki mamlakani na kuondolewa kwao kungefanyika tu kupitia matumizi ya nguvu. Kama inavyodhahirika katika utenzi huu, matumizi ya nguvu yalihatiji wanasiasa wakakamavu na mashujaa. Usawiri wa wahusika mashujaa ni dhana ambayo imeshikiliwa na nadharia ya Ulimbende ambayo iliongoza utafiti huu.

Ukakamavu huu unathibitishwa kupitia kushikwa na kutiwa kizuizini kwa Mzee Kenyatta pamoja na wenzake watano. Beti zifuatazo zinasimulia kadhia nzima:

167

Vilipozidi kuwaka
Mzee wakamshika
Na ndani wakamuweka
Kesi yake kungojea

168

Hakushikwa peke yake
Bali yeye na wenzake
Ni sita hesabu yake
Pamoja wakaingia

Beti hizi zinaonyesha kuwa ukombozi wa Afrika ulihatiji kujitolea na pia ushirikiano mkubwa wa viongozi wa kisiasa. Tunaona hapa kuwa Mzee Kenyatta hakupigania uhuru peke yake bali alishirikiana na wenzake. Ushirikiano huu haukuwa wa kujijenga kibinafsi bali ulinuiwa kuwakomboa Wakenya wote.

Mashujaa wengine watano waliotiwa kizuizini wanaorodheshwa na mshairi kama Bwana Karumba, Kaggia, Ngei, Oneko na Kubai. Mshairi amewasawiri wanasiasa hawa kama viongozi kielelezo waliotekeleza majukumu mbalimbali katika siasa za ukombozi. Kupitia sifa zao tunawaona wanasiasa waliofanya kazi kwa ushirikiano; waliojengana na kukamilishana wala sio washindani.

Nafasi ya ushairi wa Kiswahili katika uhifadhi wa historia na sifa za mwanasiasa wa Afrika kabla ya uhuru inadhihirika katika ubeti ufuatao ambapo mshairi anabainisha kujitolea kwa Kung'u Karumba kupambana na unyanyasaji wa kikoloni. Mshairi anampamba Bwana Karumba kwa maneno haya:

170

Kwanza ni Bwana Karumba
Aliyevunja miamba
Kwa kuikamata kamba
Ya umoja kuenea

Kwa mujibu wa mshairi, Bwana Karumba alikuwa kiongozi aliyejitolea kuhakikisha kuwa umoja ulienea miongoni mwa wapiganiaji uhuru na Wakenya kwa jumla. Kwa kumsawiri kama kiongozi aliyevunja miamba, mshairi hapa anaonyesha kuwa umoja haukuwa rahisi kuenezwa. Ilimbidi Bwana Karumba kupambana na upinzani mwingi. Shujaa huyu alitambua vyema nafasi ya umoja katika upiganiaji wa uhuru kwani iwapo pangetokea migawanyiko lengo la kupata uhuru lingesambaratika. Wananchi wangeanza kujitambua kama vikundi vidogovidogo vya kikabila; hivyo kukosa mwelekeo.

Kupitia jicho la mshairi tunaona usawiri wa mwanasiasa mkakamavu, Bildad Kaggia ambaye hakuchelea kuwakosoa wenzake pale walipokosea. Ukakamavu na ushujaa wa mwanasiasa huyu unaelezwa katika ubeti huu:

171

Pili ni Bwana Kaggia
Mambo wakiyakosea
Mara yeye huwambia
Akawaonyesha njia

Mwanasiasa huyu alitambua kuwa watu wanapofanya kazi yoyote pamoja makosa hayana budi kutokea na suluhisho huhitajika. Suluhisho hupatikana kwanza kwa kukubali kwamba makosa yamefanyika. Jukumu la Bwana Kaggia lilikuwa kuwaambia wenzake pale walipokosea na hatimaye kuwaonyesha njia ili makosa hayo yasivuruge utendakazi wao. Sifa hii ni muhimu katika uongozi kwani palipo na kukosoana mizozo ya kisiasa hupungua na maendeleo hupatikana.

Mwanasiasa Paul Ngei anasawiriwa kama mtetezi wa watu asiyebugua. Mshairi anafafanua jinsi Ngei alivyotekeleza juhudi za ukombozi katika ubeti huu:

172

Bwana Ngei ni wa tatu
Yeye hakujali kitu
Bali kutetea watu
Kila anayemwendea

Mshairi anasema kuwa Bwana Ngei hakujali kitu bali alimsaidia Mkenya yeyote aliyemwendea akitaka kutetewa dhidi ya dhuluma za wabeberu. Kiongozi wa aina hii ni nadra sana kupatikana siku hizi. Wakati mwingi wanasiasa hao huwajali wafuasi wao wa karibu na kuwapiga vita wapinzani wao kama inavyohibitishwa na utafiti uliofanywa na Mworira (2009). Ni vyema kutambua hapa kuwa umma unapaswa kuwa na uhuru wa kuwaendea viongozi wake pale unapodhulumiwa ili kupata suluhisho kwa matatizo yanayokabili.

Katika kumsawiri mwansiasa wa ukombozi, Achieng Oneko, mshairi anajenga taswira ya mwanasiasa aliyekuwa tayari kupambana na changamoto zilizokumba wananchi kila mahali nchini. Mshairi anatongoa yafuatayo:

173

Wa nne Bwana Oneko
Atetea nchi yako
Kila mahali huwako
Matata yakitokea

Sawa na Bwana Ngei, kiongozi huyu hakujiwekea mipaka yoyote katika utetezi wake. Ni kiongozi aliyesafiri kote nchini akiwasikiliza wananchi na kutafuta suluhisho kwa matatizo yoyote yaliyowakabili. Iwapo wanasiasa wa wakati huu wataiga mfano wa kiongozi huyu na kuwahudumia wananchi bila kuwabagua kwa misingi ya vyama vya kisiasa, kabila na tabaka bila shaka mataifa ya Afrika yatapiga hatua kubwa kimaendeleo.

Vilevile, mwanasiasa Fred Kubai anajitokeza kama shujaa aliyejitolea kuwatetea watu wa tabaka la chini, ambao mshairi anaita wabeba karai. Kuhusu utetezi huu mshairi anasema hivi:

174

Wa tano Bwana Kubai
Aliongeza madai
Wenye kubeba karai
Pia aliwatetea

Wakati wa kupigania uhuru kulikuwepo na miradi mingi iliyoendelezwa na Wazungu na Wahindi. Kwa mujibu wa Kinyatti (1992), Waafrika walitumiwa kama watumwa na vibarua. Waajiri wao hawakujali kamwe maslahi yao bali waliniuia kuwatumia kujinufaisha. Unyanyasaji wa aina hii ulihitaji kushughuliwa na kiongozi kama Bwana Kubai ambaye aliwajali wanyonge. Ni dhahiri kuwa viongozi wanaowatetea wanyonge husaidia pakubwa katika kupambana na ubaguzi wa kitabaka. Hatua hii pia husaidia kuwainua wanyonge kiuchumi, hali ambayo huliendeleza taifa zima kupitia kupunguza umaskini.

Kupitia beti hizi, mshairi amezinakidi sifa kadha muhimu zilizomfanya mwanasiasa wa Afrika wa kipindi cha kabla ya uhuru kubaki kumbukumbuni mwa Waafrika hadi leo. Katika beti hizi tunawaona mashujaa hawa watano wakijitolea kwa kila njia kuhakikisha kuwa makundi mbalimbali ya Wakenya yamepata mtetezi. Aidha, palikuwa na kukosoana miongoni mwao ili kuhakikisha kila jambo lingetekelezwa kama lilivyopangwa. Usawiri wa wahusika wenye sifa ya ushujaa, kama ulivyodhidhirika katika beti zilizonukuliwa hapo juu, umesisitizwa na nadharia ya Ulimbwende iliyoongoza utafiti huu.

Kujitolea hadi kuheshimika kwa mashujaa tuliojadili hakukupita bila kusifiwa na mshairi kama inavyodhidhirika hapa:

175

Watu hao wa heshima
Ambao walisimama
Pasi na kurudi nyuma
Nchi hii kutetea

Kinachojitokeza wazi hapa ni kuwa ili kuitwa mheshimiwa sharti mwanasiasa awe na sifa zinazomfanya kutambuliwa na wananchi. Mshairi, ambaye utafiti huu ulichukulia kuwa aliakisi maoni ya wananchi kuwahusu viongozi wao, anawaita mashujaa hawa 'watu wa heshima' waliosimama wima bila kurudi nyuma katika kuitetea nchi yao. Kigezo alichotumia mshairi kukadiria 'uheshimiwa' wa waheshimiwa kinafaa

kutumiwa hata leo. Hii ni kwa sababu baadhi ya wanaoitwa waheshimiwa wakati huu ni watu waliojaa ubinafsi na ambao hujali tu maslahi yao ya kisiasa na kiuchumi (Government of Kenya, 2007).

Ili kuthibitisha kiwango chao cha uzalendo, mshairi anaendelea kusimulia jinsi watetezi hawa wa wanyonge walivyoshikwa na mbeberu na kujipata katika mateso makubwa. Wanasiasa hawa pia walilaumiwa na mbeberu kwa kuanzisha kundi la Mau Mau na kuwachochea wananchi dhidi ya Wazungu. Mshairi anaeleza hivi:

176	177
Beberu aliwashika	Tena akawaeleza
Na ndani akawaweka	‘Ni nyinyi ndio wa kwanza
Tabu kubwa na mashaka	Mau Mau kuanza
Lakini walitulia	Ugaidi kuenea
178	
‘Namna ilivyokuwa	
Wananchi wametua	
Wa radhi kutawaliwa	
Bila ya kufikiria’	

Kama tunavyoona katika ubeti wa 178, mbeberu mwenyewe anakiri kuwa mashujaa hawa walitenda jambo muhimu, ambalo ni kuwazindua wananchi na kuwafanya kufikiri. Inaonekana wazi kuwa iwapo si kwa uzindushi uliofanywa na wanasiasa hawa pengine wabeberu wangukuwa wakitawala na kuwanyanyasa wananchi hadi leo.

Baada ya kupatikana na hatia ya kile mbeberu alichokiita ugaidi, mashujaa hawa watano pamoja na Mzee Kenyatta walifungwa gerezani Kapenguria. Isitoshe, ulinzi mkali uliwekwa na hata mawakili wao kunyimwa nafasi ya kuwatetea kama inavyoonekana katika beti hizi:

183	186
Kesini waliingia	Mbeberu kawanyima
Mjini Kapenguria	Ikibali ya kusema
Ulinzi ukaenea	Shauri lao ni moja
Kuzunguka kila njia	Ni kuja kuwatetea

Mbinu waliyotumia wabeberu ya kuwanyima wanasiasa hawa haki ya kujitetea ilinuiwa kuwakandamiza kisheria ili uhuru usije kupatikana. Hata hivyo, mawakili wawili, Priti na Kapila hatimaye waliruhusiwa kuwatetea mashujaa hawa. Walipoona

kuwa wangepoteza kesi hii, wabeberu walileta mashahidi wa uwongo kama ilivyonakidiwa katika beti zifuatazo:

190
Mashahidi walikuja
Macharia ni mmoja
Na wengi waliokuja
Maneno hayana njia

191
Macharia akaanza
Ya uwongo kueleza
Priti kamuuliza
Maswali haya na haya

192
Macharia akajibu
Maswali haya kwa tabu
Mara akayaharibu
Majibu kuyakosea

Licha ya juhudi za wabeberu za kujaribu kuwakandamiza Mzee Kenyatta na wenzake kule Kapenguria, tunaona hapa kuwa mashahidi wa uwongo waliowaleta hawakuweza kamwe kutoa ushahidi tosha wa kuwafunga mashujaa hawa. Wakili wa serikali alijaribu kila njia kupata ushahidi ambao haukupatikana. Mshairi anaeleza kupitia beti zifuatazo kuwa hata ingawa ushahidi haukupatikana serikali ya mbeberu bado ilitumia hila ili iweze kuwafunga wale sita:

198
Upande wa serikali
Somaho ndiye wakili
Alifanya kila hali
Ndani apate watia

200
Kila njia alipita
Ya kumfunga Kenyatta
Kwa umoja wetu sita
Kifungoni kuwatia

Kesi iliyofafanuliwa kupitia beti hizi inaonyesha jinsi mbeberu alijaribu kila njia kubaki mamlakani katika mataifa ya Afrika na hivyo kuendelea kutumia rasilmali zilizofaa kuwanufaisha Waafrika. Nadharia ya Ulimbwende ambayo iliongoza utafiti huu inashikilia umuhimu wa kuwafuatilia wahusika wa kishairi na kutambua mabadiliko wanayopitia. Hapa tunashuhudia hali mbalimbali walizopitia wanasiasa kabla ya uhuru, ikiwa ni pamoja na kupelekwa mahakamani katika juhudi za kulikomboa bara la Afrika.

Katika beti zifuatazo mshairi anatusawiria viongozi waliokuwa tayari kulipa gharama ya uzalendo kwa kujitolea kufungwa gereza miaka saba. Ufuatiliaji huu wa wahusika wa kishairi unasisitizwa katika Nadharia ya Ulimbwende. Mshairi

anatusawiria wanasiasa katika mazingira tofauti yakiwemo yale ya mashambani, mijini na gerezani. Kwa kufanya hivi, panawasawiri viongozi wakakamavu waliovumilia kifungo hicho bila kulalamika kwa kujua vyema kuwa uhuru ungepatikana tu kupitia mateso ya aina hii. Mshairi anatongoa:

212	213
Ndipo wakatiwa ndani	Na wote waheshimiwa
Wote sita kifungoni	Myaka waliichukuwa
Myaka saba gerezani	Bila tabu wakatuwa
Hapakuwa na sheria	Siku wakiingojea

Baadaye tunaona wazalendo hawa wakihamishiwa Lodwar na kuendelea na mateso zaidi. Mshairi anazidi kusimulia:

260	261
Tuwakumbuke wa kwanza	Ndiyo wote kuhamishwa
Myaka waliimaliza	Lodwar wakafikishwa
Kutoka hawakuweza	Ndipo wakateremshwa
Ndipo wakazuiliwa	Matesoni kuingia

262
Mzee kaadhibiwa
Na wote waheshimiwa
Tabu kubwa ilikuwa
Mungu kawasaidia

Tunaona hapa kuwa wazalendo wale sita waliteseka kwa miaka saba gerezani ili uhuru upatikane. Huku kulikuwa kujitoa mhanga kwa hali ya juu, sio tu kwa ajili ya uhuru wao binafsi bali kwa ajili ya uhuru wa Wakenya wote. Nadharia ya Ulimbende inasisitiza juu ya usawiri wa wahusika wa kishairi ambao wana sifa za kishujaa kama wanavyojitokeza katika shairi hili.

Ili kuthibitisha sifa hii ya ushujaa, mshairi anazidi kusimulia juu ya mateso yaliyojiri kule kizuizini Lodwar:

263	264
Walisulubiwa sana	Malazi yakawa chini
Na tabu kila namna	Bila kitu sakafuni
Mashaka waliyaona	Hawakuwa na imani
Ili wageuze nia	Huruma kuwafanyia

Mateso waliyopata wazalendo hawa yanalinganishwa na kusulubiwa, yaani kuangikwa msalabani kama alivyofanywa Masihi kwa mujibu wa imani ya Wakristo. Taswira hii inaonyesha kuwa wazalendo hawa walijitolea kufa kwa ajili ya wananchi kama alivyojitolea Kristo kwa ajili ya binadamu. Pia, inadhihirika hali ya kutokuwa na uwezo wowote wa kujitoa katika mateso yale. Wazalendo hawa pia walikumbana na mazingira mabovu gerezani kama inavyoshuhudiwa katika beti hizi. Haya ni pamoja na kulala sakafuni bila chochote cha kutandaza wala kujifunika. Isitoshe, wazalendo hawa waliteswa kwa kupewa chakula kibovu, kama inavyoelezwa katika ubeti huu:

265

Chakula walichopewa
Si chakula cha kuliwa
Ni mashaka yalikuwa
Siwezi kuhadithia

Ni dhahiri hapa kuwa wazalendo walinyimwa haki za kimsingi ambazo ni chakula bora na malazi. Chakula walichopewa kilikuwa duni na hakikufaa kamwe kwa afya ya binadamu. Kama tunavyoona katika ubeti wa 263 ulionukuliwa hapo juu, nia kuu ya wabeberu katika kuwatesa wazalendo hawa ilikuwa kuwageuza nia ili juhudi zao za kupigania uhuru zikome. Licha ya mateso haya, wazalendo hawa waliendelea na juhudi za ukombozi.

Kupitia beti hizi tunaona dhima ya mshairi ikijitokeza kuhusiana na usawiri wake wa matukio halisi ya wakati anaoishi kama anavyodokeza Kezilahabi (1976). Mshairi anakiri kuwa mambo haya hakika yalitendeka, huku akitaja mwaka halisi wa utendekaji wake kuwa 1952, mwaka ambao hali ya hatari ilitangazwa nchini Kenya. Haya ni kwa mujibu wa ubeti ufuatao:

214

Hapo haikuwa mbali
Ni hamsini na mbili
Mambo yalikuwa kweli
Nchi nzima kuenea

Ushahidi huu wa mshairi unaweza kuaminika tukizingatia kuwa mshairi mwenyewe alizaliwa mnamo 1933 kama ilivyonakiliwa katika utangulizi wa diwani hii. Hii inamaanisha kuwa wakati wa tukio hili la kihistoria, mshairi alikuwa na umri wa

miaka 19. Huu ni ushahidi kuwa alikuwa amekomaa kiasi cha kufahamu kilichokuwa kikiendelea. Hili linathibitisha madai ya Waliaula (2009) kuwa maandishi mengi ya kisiasa huchochewa na mazingira ya kisiasa ya wakati wa uandishi. Aidha, mshairi hutunga kazi zake kutokana na matukio anayoshuhudia maishani.

Matukio mengine ya kihistoria yaliyonakidiwa na mshairi ni pamoja na kushikwa kwa wanasiasa wengine kama vile Odede na Chokwe ambao walikuwa viongozi wa KAU. Kuwahusu wanasiasa hawa mshairi anasema:

221	222
Odede msheshimiwa	Na Pwani ni kiangaza
Naye akazuiliwa	Bwana Chokwe aongoza
Pwani walimchukuwa	KAU kuieneza
Huko wakamzuia	Watu kuizungukia
223	
Mambo yalipowaka	
Chokwe wakamshika	
Hola wakampeleka	
Kwenda kumzuilia	

Kuwahusu viongozi hawa, mshairi anadhihirisha kuwa sio wanasiasa wakuu sita tu, yaani Kenyatta, Karumba, Kaggia, Ngei, Oneko na Kubai walioingia kumbukumbuni kwa kujitolea ili Kenya iwe huru. Kwa mfano, mshairi anamtaja Bwana Chokwe kama kiangaza. Hii ina maana kuwa Bwana Chokwe alikuwa mwanasiasa kielelezo. Aliongoza kwa vitendo huku akiwazindua wananchi wa Pwani kuhusiana na masuala ya ukombozi kupitia kwa chama cha KAU. Ni kutokana na juhudi hizi ambapo kiongozi huyu alijipata mashakani kwa kushikwa na kupelekwa kizuizini Hola.

Kama tulivyoona hapo juu, wanasiasa hawa hawakutiwa kizuizini tu bali walipata mateso makali. Kutokana na uzalendo mkubwa waliokuwa nao, viongozi hawa walivumilia mateso haya licha ya kushuhudia baadhi ya wenzao wakiuliwa kule kizuizini. Mshairi anayaweka wazi mateso hayo:

224	226
Hapo walipomshika	Tabu walizokipewa
Kambini wakamuweka	Ni mauti yalikuwa
Tabu kubwa na mashaka	Wengine waliuliwa
Naye akavumilia	Maisha yakapotea

Kutokana na maelezo haya ya mshairi, tunawaona wanasiasa ambao hawakutetereka katika msimamo wao. Ni nadra sana kuwapata watu kama hawa wanaoweza kuendeleza juhudi za ukombozi ambazo wameshuhudia wazi zikikomesha maisha ya wenzao, hasa juhudi ambazo ni za kujitolea bila malipo yoyote.

Uzalendo kama kishawishi cha kuingia uongozini wa kisiasa ni jambo lingine ambalo mshairi amezingatia katika utenzi huu. Mshairi anasimulia jinsi baadhi ya wazalendo waliacha kazi zao za kuajiriwa na kuingia katika siasa za ukombozi. Hii ni tofauti kabisa na kipindi cha baada ya uhuru ambapo wanasiasa wamekuwa wakifurahia mishahara minono pamoja na marupurupu mengineyo. Mfano bora wa kujitolea anaotoa mshairi ni ule wa Bwana Ngala. Mshairi anasema hivi kumhusu shujaa huyu:

250	251
Akisodesha shuleni	Wakati ulipofika
Huko Mombasa mjini	Ndipo alipogutuka
Shule ni Bakastani	Akaanza kutamka
Akiwa na cheo pia	‘Na mimi nitaingia’

Mshairi hapa anaonyesha jinsi wazalendo wa wakati huo walikuwa wakizishawishi nafsi zao kikamilifu kabla ya kuingia katika siasa. Tunaona kuwa Bwana Ngala aliacha kazi yake ya ualimu katika shule ya Bakastani ambako alikuwa na cheo. Hatimaye aliingia katika siasa za wakati huo ambazo mbali na kutokuwa na mapato makubwa zilihatarisha maisha ya wahusika.

Bwana Ngala alijiunga na wenzake wachache waliokuwa na elimu wakati huo, akiwemo Bwana Tom na kuelekea Landani baada ya kuchaguliwa kuwa viongozi wa chama. Walipotoka Landani walikuwa wamekubaliana kuunda chama kimoja tu cha kisiasa ili kuondoa tatizo la ukabila ambalo lingetatiza juhudi zao. Wakati huo vyama vya kisiasa havikuwa vimeanza kuundwa kwa misingi ya kikabila kama anavyodokeza Gachukia (2005). Kuhusiana na siasa za vyama, wazalendo hawa walitoa kauli hii:

273	274
‘Vyama hivi vya majimbo	‘Twataka kiwe kimoja
Vyataka haribu mambo	Kila mtu atakuja
Sisi twalitaka umbo	Kujiunga kwa pamoja
La umoja kuenea’	Vidogo vitapotea’

Kauli hii ya wazalendo inaonyesha kuwa kilichohitajika wakati huo ni umoja. Ndiposa wakahubiri siasa za chama kimoja kikuu ambacho kingewaleta Wakenya pamoja kama chombo cha kuwawezesha kupigana na mbeberu kama kundi moja lisilogawanyika kikabila.

Moyo wa wazalendo hawa wa kushauriana unajitokeza pale wanaposafiri hadi Lodwar kupata ushauri kutoka kwa Kenyatta na wenzake kuhusiana na mambo mawili makuu. Haya yalikuwa, kwanza, kuongezwa kwa idadi ya wajumbe ambao wangerudi nao Landani kuendelea na mazungumzo juu ya upatikanaji wa uhuru. Pili, walitaka kushauriana na Kenyatta jinsi ya wangeweza kuwashawishi wabeberu wawakubali kukisajili chama kimoja chenye nguvu. Mashauriano haya yaliwezekana wakati huo kwa kuwa wanasisia wa kipindi cha kabla ya uhuru hawakuwa wakiongozwa na ubinafsi katika maamuzi yao. Mshairi anafafanua hivi:

276

Wajumbe wakafikiri
'Natuifunge safari
Mpaka huko Lodwari
Tutakwenda pata njia'

282

Haja yao ilikuwa
Wajumbe kuongezewa
Na chama kukubaliwa
Kenya nzima kuenea

Mawazo haya ya wajumbe yanaonyesha kuwa kutafuta ushauri ni jambo muhimu sana katika uongozi wowote. Mambo mengi huharibika palipo na uongozi wa kidikteta. Katika uongozi wa aina hii wanasisia huamua mambo mazito yanayoathiri taifa bila kushauriana na wenzao.

Kutokana na kushauriana huku, mshairi anaripoti kuwa hali iliyofuatia ilikuwa ya kuridhisha. Wajumbe waliongezwa na kufikia kumi na tisa na hata waliporejea kutoka Landani chama kilikuwa tayari kimeundwa kikamilifu. Ni muhimu kutambua hapa kuwa wajumbe hawa hawakujipendekeza kwa umma kama ilivyodhihirika katika kipindi cha siasa za chama kimoja na kile cha siasa za vyama vingi. Ung'ang'aniaji wa mamlaka, kama unaobainishwa na nadharia ya Baada-Ukoloni, haukuwa umekita mizizi katika siasa za bara la Afrika. Mshairi anatusimulia matokeo ya mashauriano hayo:

285

Walioongezwa hasa
Wajumbe kumi na tisa
Ikawa pia ramsa
Baada kuwapokea

287

Mambo yakawa tayari
Waliporudi safari
Chama kikawa tayari
Wananchi wangojea

Kinachojitokeza hapa ni kuwa wazalendo hawa waliweza kupiga hatua katika juhudi za ukombozi kwa kuwa waliaminiana na kuheshimiana. Tunawaona wajumbe waliotoka Landani wakitafuta ushauri kutoka kwa wenzao kule Lodwar wanapotatizika. Walijua vyema kuwa ushauri huu ungerahisisha uundaji wa chama na pia uongezwaji wa idadi ya wajumbe na hivyo kufanikisha juhudi za ukombozi.

Katika mikutano ya uhuru wanasiasa hawa waliendelea kushikamana kama kundi la watetezi wa haki. Ni dhahiri kuwa ushindani na wivu wa kisiasa, kama unavyobainishwa na Mulokozi (1992) na Emaittah (2007) haukuwa umeanza kudhihirika miongoni mwa wanasiasa wa Afrika. Muungano wa wanasiasa hawa ulijitokeza kupitia kusesitiza umuhimu wa umoja ambao viongozi walihisi kuwa ungepatikana iwapo wananchi wote wangejiunga na chama cha KANU ambacho kilisifika sana wakati huo. Mshairi anaeleza maana ya chama hiki cha kisiasa hivi:

295

Ni umoja wetu sisi
Waafrika halisi
Kujitawala weusi
Kenya kuiangalia

Mshairi hapa anamaanisha kuwa chama hiki ndicho kingetumiwa na Waafrika kama chombo cha kuleta umoja miongoni mwao na hivyo kuwawezesha kupata uhuru. Kauli hii inaashiria kuwa wanasiasa wa kabla ya uhuru walitambua vyema kuwa uhuru ungepatikana iwapo wangejitambua kama Waafrika na kujikomboa wakiunganishwa na umoja wao.

4.5 Upinzani Kabla ya Uhuru

Siasa za vyama vya upinzani barani Afrika hazikuanza wakati wa harakati za kuondoa utawala wa chama kimoja bali zina historia ndefu. Katika sehemu hii mshairi anatusimulia jinsi upinzani ulivyoanza nchini Kenya na athari zake kwa juhudi za

kupigania uhuru. Tumeshaona jinsi Waafrika walivyoungana kupitia uundwaji wa chama kimoja ambacho walikiona kama dira ya kuwaongoza ili kujinyakulia uhuru.

Licha ya kusesitiza umoja, baadhi ya wanasiasa walionelea umuhimu wa kuwa na chama cha upinzani. Hapo ndipo palipoundwa chama cha KADU, jambo ambalo lilimfurahisha sana mbeberu kwani alipata njia ya kuwatenganisha Waafrika ambao hapo awali waliunganishwa na KANU. Inaonekana wazi kuwa mbeberu alitambua umuhimu wa kuuimarisha utawala wake ili aendelee kufaidi kutokana na rasilimali za Waafrika. Aidha, kwa kuwatenganisha Waafrika, mbeberu angewapunguzia nguvu zao za kupigania uhuru ambazo zilitokana na muungano wao. Nadharia ya Baada-Ukoloni inaeleza kuwa ushindani wa kisiasa ni mojawapo ya athari za kikoloni ambazo zimekuwepo kwa muda mrefu katika bara la Afrika. Kuhusiana nakiini cha ushindani huu mshairi anasema hivi:

333
Bwana Ngala akasema
Upinzani ni lazima
Hapa Kenya kusimama
Ndipo tutaendelea'

334
Wakaanza upinzani
Na Bwana Toweti ndani
Na wengine majirani
Jina nitawatajia

Katika beti zinazofuatia mshairi anawataja wanasiasa wengine waliojiunga na upinzani kama vile Bwana Moi, Muliro, Seronei na Toweti. Ili kuthibitisha jinsi mbeberu alivyofurahishwa na utengano ulioanza kuzuka miongoni mwa Waafrika, chama cha KADU kilipata usajili mara moja. Kufikia hapa tunatambua ushairi wa Kiswahili ukipata dhima ya kuhifadhi historia ya siasa za vyama vingi katika bara la Afrika. Hii inathibitisha maoni ya King'ei na Kemoli (2001) kuwa ushairi huu ulitumiwa kwa muda mrefu kuhifadhia historia ya jamii. Mshairi anainakili historia hii kwa maneno haya:

345
Chama wakakipeleka
Kwa Balozi kikafika
Naye akakiandika
Bila matata kutia

Usajili huu wa haraka wa chama hiki unaonyesha jinsi mkoloni alivyouogopa muungano wa wazalendo. Hili ni dhihirisho la kutosha kuwa wazalendo hawa walikuwa na uwezo mkubwa wa kuung'oa ukoloni kupitia ukakamavu wao.

Baada ya kuwapo kwa upinzani kwa muda na kuundwa chama kingine cha APP, wanasiasa hawa walitambua kuwa kutoungana kwao kungesambaratisha juhudi za kupatikana kwa uhuru. Hii ni kwa sababu kila chama kilitaka kuwa na wajumbe wake katika bunge la kwanza baada ya kupatikana uhuru. Hali hii ilimfanya Bwana Ngei kujaribu kutafuta muungano wa vyama ili kuweza kujipatia wajumbe. Kuhusu mbinu hii mshairi anasema:

489

Bwana Ngei kakubali
Kayaona ni ya kweli
Wakiungana wawili
Watapita kama njia

Kilicho dhahiri hapa ni kuwa baadhi ya wanasiasa walikuwa wameanza kuingiwa na tamaa na ubinafsi na kuanza ushindani baina yao. Hatari iliyotokana na ushindani huu ni kuwa wanasiasa hawa walipoteza muda mwingi wakishindana baina yao badala ya kupigana na mkoloni. Msimamo wa nadharia ya Baada-Ukolonini kuwa athari za kikoloni zinaweza kuufanya umma kuonekana kama haujapata uhuru kamili licha ya kuwa mkoloni aliondoka barani Afrika miongo kadha iliyopita. Hii ni kwa sababu ushindani huu ulianza miongoni mwa wanasiasa wa Afrika kabla ya uhuru, na kuendelea baada ya uhuru na pia katika kipindi cha siasa za vyama vingi.

Ushindani huu ulipochacha, ilifika wakati ambapo vyama vyote vilikosa utulivu hasa ulipowadia wakati wa uchaguzi. Mshairi anatupa taswira kamili ya hali ilivyokuwa:

498

Wakati ulipofika
Vyama vilihangaika
Ikawa ni pata shika
Kila chama chatapia

Ujumbe anaowasilisha mshairi hapa ni kuwa kilichokuwa muhimu kwa wanasiasa wakati huu sio jinsi uhuru ungepatikana bali idadi ya wajumbe ambao vyama vyao vingepata. Ni dhahiri kuwa kwa muda wanasiasa hawa walisahau machungu ya ukoloni na kuanza kujitafutia vyeo katika serikali ambayo ingeundwa baada ya uhuru kupatikana. Ubinafsi, kama unavyodokezwa na Makillah (2009) ulitawala mawazo na vitendo vya wanasiasa.

Suala la miungano ya vyama kama linavyojitokeza wakati wa siasa za wakati wa siasa za vyama vingi pia lilikuwepo kabla ya uhuru. Tunashuhudia wanasiasa wa kabla ya uhuru wakijaribu kuunganisha vyama vyao kwa lengo la kupata wajumbe wengi. Hata hivyo, kwa mujibu wa mshairi, miungano hii haikuwa na manufaa yoyote. Mshairi anaeleza kuwa ni chama kikuu cha KANU kilichopata idadi kubwa ya wajumbe huku vyama vilivyoungana vikiambulia patupu. Matokeo ya ushindani huu wa vyama yalikuwa hivi:

501	502
Majina yalipoanza	Na muungano wa vyama
Ndipo KANU kuongoza	Wale waliosimama
Kwa viti kuvingiza	Wengi wao walikwama
KADU ikiandamia	Hawakuiona njia

Mshairi anasisitiza hapa kuwa kilichohitajika zaidi wakati huo ni umoja. Kujigawanya katika vyama vidogo vidogo na hatimaye kujaribu kuungana hakungesaidia lolote katika harakati za kupigania uhuru. Hatua hii ilisababisha mizozo isiyokuwa na maana katika kipindi ambacho hata serikali ya baada uhuru haikuwa imeundwa na kufikia ukomavu wa kuanzisha siasa za vyama vingi.

Ilichukua muda kwa Mzee Kenyatta kuwashawishi wananchi pamoja na viongozi kupitia mikutano mbalimbali ya uhuru juu ya umuhimu wa kulijenga taifa badala ya kushikilia siasa za vyama. Mzee Kenyatta pia hakusita kuwahimiza wananchi juu ya umuhimu wa umoja kupitia mwito wake wa harambee. Hebu tuutazame wosia wa Mzee:

587	588
Akaanza kuusia	‘Harambe maana yake
Maneno akatwambia	Kamba moja tuishike
‘Wananchi mwasikia	Waume na wanawake
Harambee imeingia’	Tupate kuendelea

Kupitia maneno haya ya mshairi tunaona kuwa Mzee Kenyatta alipenda umoja wa wanajamii wote nchini. Pia hakupendelea ubaguzi wa kijinsia kwani alitaka watu wote, wake kwa waume, kushirikiana ili kuleta maendeleo. Ubaguzi wa kijinsia katika muktadha wowote, kama anavyoshikilia Ndungo (1985), ni adui ya maendeleo. Mchango wa wanawake katika upiganiaji wa uhuru wa mataifa ya Afrika, hasa Kenya, ni ukweli wa kihistoria usioweza kupuuzwa.

Mzee Kenyatta pia hakutaka mtu binafsi wala chama chochote cha kisiasa kijisifu kwa kupigania uhuru bali wananchi wote washiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi. Kwa maneno ya mshairi Mzee Kenyatta alisema hivi:

589	590
‘Tuijenge nchi yetu	‘Sifa hii si ya chama
Lipande taifa letu	Ni sifa ya nchi nzima
Heshima kubwa ni kwetu	Kila mtu kasimama
Vizazi kuviachia’	Kwa pamoja sote pia

Kutokana na maneno haya ya Mzee Kenyatta ni dhahiri kuwa kiongozi huyu alitaka wanasiasa wenzake wayajali maslahi ya Wakenya wote wala sio yale ya kibinafsi. Mzee Kenyatta pia alitambua mchango wa wazalendo wote katika harakati za kupigania uhuru.

Kuhusiana na kuibuka kwa vyama vya upinzani, Mzee Kenyatta alitambua kuwa kuna wanasiasa waliowekeana visasi. Kwa hivyo aliwaomba watu wote wasameheane na kuendelea kuwa na umoja. Mzee alisema hivi:

593
‘Pia hakuna nafasi
Kuwekeana visasi
Kwa wale walioasi
Halafu wakarejea’

Mzee hapa anawarejelea wanasiasa walioanzisha vyama vya upinzani lakini wakarejea katika chama cha KANU wakati wa kuunda serikali mpya ambayo ingechukua madaraka baada ya uhuru kupatikana. Kama tulivyoona hapo mwanzo, palikuwa na ushindani mkubwa wa kisiasa, kama unavyojitokeza katika nadharia ya Baada-Ukoloni, uliowafanya wanasiasa kuanza kupotoka na kung’ang’ania ufanisi wa vyama vyao badala ya taifa zima.

Baada ya changamoto nyingi zilizowakumba wanasiasa waliopigania uhuru, hatimaye uhuru ulipatikana nchini Kenya na kupokelewa kwa furaha kuu. Mshairi anasimulia juu ya furaha iliyojiri:

600

Nayo haikuwa mbali
Ukadhihiri ukweli
Disemba kumi na mbili
Mara ilitufikia

601

Ulikuwa mwaka wetu
Mwaka sitini na tatu
Wakafurahika watu
Wote wakashangilia

Mshairi hapa amenakili tarehe kamili ulipopatikana uhuru nchini Kenya kwa lengo la kuonyesha jinsi uhuru huu ulibaki katika kumbukumbu za Wakenya. Mshairi pia anaonyesha jinsi kupatikana kwa uhuru kulivyoshangiliwa na Wakenya na kuwapa matumaini makubwa ya ufanisi. Taswira ya Wakenya wanaoshangilia uhuru wao inathibitisha udhihirishaji wa hisia na ujenzi wa taswira kama mihimili muhimu ya nadharia ya Ulimbwende.

4.6 Hitimisho

Katika sura hii tumeona jinsi ushairi umetumiwa kuhifadhi historia ya mwanasiasa wa Afrika katika muktadha wa ukombozi wa nchi ya Kenya. Aidha, tumejadili kwa kirefu jinsi mshairi alivyomsawiri mwanasiasa wa Afrika katika kipindi cha kabla ya uhuru. Imebainika kuwa mwanasiasa wa kipindi hicho alikuwa mzalendo aliyejitahidi kuwapatanisha wananchi ili waungane pamoja na kupigania uhuru.

Mwanasiasa wa Afrika wa kipindi cha kabla ya uhuru pia amesawiriwa kama kiongozi mkakamavu aliyejitolea mhanga kupigania ukombozi wa nchi yake. Kujitolea huku kulikumbwa na changamoto nyingi. Hizi ni pamoja na kusalitiwa na wananchi wenzake waliokuwa vibaraka wa wabeberu, kutiwa kizuizini na kufungwa jela na serikali ya kikoloni.

Hatimaye tumejadili jinsi vyama vya upinzani vilivyoanzia nchini Kenya na kusababisha migawanyiko kati ya wanasiasa. Tumeshuhudia pia upinzani huu ukikaribia kusambaratisha juhudi za ukombozi na juhudi za Mzee Kenyatta za kuwapatanisha wanasiasa waliozozana.

Katika sura inayofuatia tutaangalia sifa za Mwanasiasa wa Afrika katika kipindi cha siasa za vyama vingi. Madhumuni ya tatu ya utafiti huu yalikuwa kutathmini mabadiliko ya mwanasiasa wa Afrika baada ya uhuru kwa mujibu wa ushairi wa Kiswahili. Tutajadili jinsi matumaini makubwa ya ufanisi waliyokuwa nayo wananchi yalivyovunjwa na wanasiasa wa kipindi cha baada ya uhuru. Tutachunguza jinsi

ukoloni mamboleo ulivyowatamausha wananchi pamoja na madhara ya utawala wa chama kimoja.

SURA YA TANO

MABADILIKO YA MWANASIASA WA AFRIKA BAADA YA UHURU

5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa tathmini ya mabadiliko ya mwanasiasa wa Afrika mara tu uhuru ulipopatikana na kuendelea hadi kwenye kipindi cha siasa za vyama vingi. Tathmini hii ilitolewa kwa mujibu wa madhumuni ya pili na ya tatu ya utafiti huu. Madhumuni ya pili ya utafiti huu yalikuwa kubainisha sifa za mwanasiasa wa Afrika kabla ya uhuru kwa mujibu wa ushairi wa Kiswahili. Nayo madhumuni ya tatu yalikuwa kutathmini mabadiliko ya mwanasiasa wa Afrika baada ya uhuru kwa mujibu wa ushairi wa Kiswahili.

Sura hii imegawanywa katika sehemu mbili kwa lengo la kuwasilisha matokeo ya utafiti yaliyojumuisha vipindi viwili vya kihistoria. Sehemu ya kwanza inajadili jinsi mwanasiasa wa Afrika alivyobadilika punde tu uhuru ulipopatikana. Kwa mujibu wa utafiti huu, mabadiliko hayo yalisababisha kuzuka kwa udikteta wa chama kimoja cha kisiasa. Sehemu ya pili inaonyesha jinsi mwanasiasa wa Afrika alivyoshindwa kuuridhisha umma licha ya kuingia kwa mfumo wa siasa za vyama vingi ambao ulinuiwa kuleta demokrasia kamili.

5.2 Mabadiliko ya Ghafla

Katika sehemu hii tulijadili jinsi mwanasiasa wa Afrika alivyobadilika ghafla na kudhihirisha sera tofauti na zile alizowaahidi wananchi kabla ya uhuru kupatikana. Kama tulivyoona mwishoni mwa Sura ya Nne, umma wa Afrika ulikuwa na matumaini makubwa ya kupatikana kwa maisha bora baada ya mkoloni kuondoka. Matumaini haya yaliegemezwa kwa viongozi wa kisiasa. Wananchi waliwatazama wanasiasa wa kipindi hicho kama wazalendo na wapiganiaji wa dhati wa haki za umma.

Katika Sura ya Nne tuliona pia jinsi wanasiasa wa kipindi cha kabla ya uhuru walikuwa na uwazi katika kuafikia na kutekeleza maamuzi. Tuliona jinsi walivyojadiliana kati yao pale walipohitaji kukabiliana na changamoto zilizo zuka katika harakati zao za kupigania uhuru. Aidha, viongozi hawa walijitokeza kama wapenda demokrasia walioshauriana na umma kwa karibu. Kama tulivyoona katika ushairi wa Kibao (1972), umma uliwaamini na kuwatukuza sana wazalendo hawa.

Sifa walizolimbikizwa zililifanya kundi dogo la wanasiasa pamoja na vibaraka wao kuanza kupotosha mwelekeo uliokuwa umeanzishwa na umma wakati wa kupigania uhuru. Viongozi wa kisiasa walibadilika na kuwa ‘wazungu weusi’ waliowakandamiza wakosoaji wao kupitia mbinu kadha, ikiwemo ile ya kuwatia kizuizini (Mrikaria, 2010).

5.2.1 Wazungu Weusi

Kwa mujibu wa kazi za kishairi zilizohakikiwa katika sura hii, demokrasia iliyoonekana kuwepo kabla ya uhuru ilikuwa ya muda tu. Punde tu uhuru ulipopatikana baadhi ya wanasiasa waliochukua nyadhifa mbalimbali serikalini, hasa viongozi wa kitaifa, walibadilika na kuiga mbinu zile zile zilizotumiwa na wakoloni katika kuukandamiza umma. Katika sura hii tunawatazama washairi kama watetezi wanaozungumza kwa niaba ya umma. Washairi wanafanya hivi kutokana na dhima ya mshairi ya kujitazama kwanza kama raia wa nchi yake na pia kama raia wa kimataifa. Hatimaye mshairi huzama katika nafsi yake huku akimulika hisia zake za kiutu na za kiuraia (Mohamed, 2002).

Kama njia ya kutolea hisia zake kuwahusu viongozi wa kabla ya uhuru, Abdalla (1973) katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* anatusimulia jinsi wanasiasa walivyowakomesha wakosoaji wao. Katika dibaji ya diwani hii, mshairi anaeleza kuwa aliyatunga mashairi yaliyomo akiwa mfungwa katika Gereza Kuu la Kamiti na Gereza la Shimo la Tewa kati ya Machi 1969 na Machi 1972. Anasema kuwa alifungwa kutokana na kile kilichoelezwa kama kupatikana na hatia ya kuchochea watu kuipindua Serikali ya Kenya kwa kutumia silaha baada ya kuiandika, kuichapisha na kuisambaza karatasi aliyoiita *Kenya: Twendapi?*

Kifungo cha Abdalla kilitokea mwaka wa sita tu baada ya kupatikana kwa uhuru wa Kenya. Hii ni ithibati kuwa viongozi wa kisiasa walitumia mbinu zile zile zilizotumiwa na wakoloni kuwakomesha wazalendo walipokuwa wakipigania uhuru. Mbinu hizi ni pamoja na kuwatia gerezani na kuwatesa wakiwa humo ili kuwatia hofu ilmuradi wasiendeleze juhudi za ukombozi. Hili linaweza kuthibitishwa kupitia shairi liitwalo ‘N’shishiyelo ni Lilo’ (kur. 1-4) ambapo mshairi anaeleza sababu zake za kufungwa na masaibu aliyoyapata gerezani. Kuanzia ubeti wa pili mshairi

anawasawiri viongozi wa baada ya uhuru kama watu wasiopenda kuambiwa ukweli.

Mshairi anasema:

2

Walinena walimwengu, wa zama zilopisiye
Kwamba kweli i utungu, kwa yule aambiwaye
Nami haya ndugu yangu, sasa niyaaminiye
Asojuwa nasikiye, apeleleze ajuwe

3

Kweli nnaifahamu, haipendwi aswilani
Kwa mja hiyo ni sumu, mbaya iso kifani
Mwenye kuitakalamu, hapendezi katwaani
Sasa nshayaamini, ni kweli haya ni kweli

Mshairi analalamikia kufungwa kwake kutokana na 'kosa' la kuwaambia wanasiasa ukweli – kwamba uongozi wao haukulenga kuwanufaisha wananchi. Ni ukweli huu ambao mshairi anasema kuwa una uchungu kwa anayeambiwa. Katika ubeti wa 3 mshairi anashikilia kuwa asiyeupenda ukweli huuona kama sumu mbaya sana. Hali hii ndiyo iliyowafanya wanasiasa wa baada ya uhuru kuwachukia hata washairi waliotunga na kukashifu uongozi wao mbaya. Kutokana na chuki hii Abdalla alitiwa gerezani na kupatikana na dhiki anayoifafanua katika ubeti wa nne:

4

Kweli imenitongeya, kwa kuinena mwendani
Wale nalowaambiya, wamenitia dhikini
Wameniona mbaya, kumshinda Firauni
Kweli, sasa naamini, si wangi waipendao

Hapa mshairi anaanza kusimulia chuki waliokuwa nayo wanasiasa kwa waliowaambia ukweli kuhusiana na uongozi wao dhalimu. Analinganisha chuki waliyokuwa nayo wanasiasa kwake na ile wana wa Israeli waliyokuwa nayo kwa Firauni walipokuwa utumwani Misri. Mzozo unaojitokeza hapa kati ya wanasiasa na washairi unathibitisha kuwa washairi ni washiriki kamili katika siasa za nchi (Njogu, 2004).

Katika beti zinazofuatia mshairi anaendelea kusimulia jinsi yeye na wenzake waliowakosoa wanasiasa walivyoteswa. Mshairi anakiri:

5

Kweli naliwaambiya, wakuu wa nti hini
Haeleza moya moya, kwa wanati wa ntini
Kuhusu walofanyiwa, upande wa Upinzani
Sasa kuwamo tabuni, nalipwa kwa hiyo kweli

Ubeti huu unadhihirisha madai ya serikali kwamba mshairi huyu alitaka kuipindua serikali kwa kutumia silaha hayakuwa ya kweli. Alichofanya mshairi ni kujaribu kuwazindua wananchi kuhusu dhuluma zilizofanywa na serikali dhidi ya wakosoaji wake. Kama kuna silaha aliyoitumia mshairi huyu ni ile anayoizungumzia katika shairi hili, yaani kusema ukweli. Kutokana na ufichuzi huu, tunawaona wanasiasa walioibuka kuwa viongozi waongo na dhalimu, wasiopenda kukosolewa kamwe.

Udhalimu uliokithiri unadhihirika pale mshairi anapotoa taswira ya hali ilivyokuwa kizuizini kupitia ubeti ufuatao:

11

Kweli japo ni ngomeni, kwenye kuta ndefu nene
Kabisa sitangamani, na mahabusu wingine
Na lengo kubwa nadhani, ni: nilonalo 'sinene
Hazua mambo mingine, kwa kuambukiza watu

Katika ubeti huu wanasiasa wanasawiriwa kama viongozi wakandamizaji. Mshairi anaweka peupe kuwa wanasiasa waliwakandamiza wananchi wenzao kwa lengo moja kuu; yaani kuendelea kutawala kwa mabavu. Ndiposa wakawatenga wakosoaji wao mbali na wafungwa wengine ili wasiendeleze uzindushi.

Matokeo ya kufungwa gereza kwa wakosoaji wa wanasiasa yanadhihirisha sura nyingine ya viongozi hawa. Katika ubeti ufuatao, Abadalla (1973) anawasawiri baadhi ya wanasiasa wa kipindi cha baada ya uhuru kama wauaji. Mshairi anafichua:

19

Wangi washasumbuliwa, waneni wa kweli hiyo
Na wangi washauliwa, kwa kutobadili nyoyo
Na mimi nimeradhiwa, ku'yandama sera hiyo
'Tafuwata zao nyayo, n'shishiyelo ni lilo

Kulingana na ubeti huu, baadhi ya viongozi wa baada ya uhuru walikuwa tayari kufanya chochote, ikiwa ni pamoja na kuwaua wapinzani wao mradi wabaki uongozini. Hivi ndivyo walivyofanya viongozi wa Kenya kwa kuwatia waandishi

kadha kizuizini ambao walitunga kazi zao wakichochea na mazingira ya kisiasa ya wakati huo (Waliaula, 2009).

5.2.2 Usawiri wa Wanasiasa Kijazanda

Ulinganishi ni mbinu muhimu sana katika uwasilishaji wa ujumbe kishairi. Hii ni kwa sababu ushairi hutumia lugha ya mkato kuwasilisha ujumbe ambao ungewasilishwa kwa maelezo marefu katika kazi za kinathari kama inavyosisitizwa na Maitaria (2012). Kwa jumla, sanaa ya ushairi inadhihirikia kupitia uteuzi maalum wa maneno unaotokana na uhuru alio nao mshairi wa kutumia ubunifu wa msamiati na miundo mbalimbali ya lugha. Uteuzi huu wa lugha husaidia katika kuathiri hisia na kuigusa mioyo ya hadhira (Mulokozi, 2000).

Jazanda ni aina ya ulinganishi ambapo mtu au kitu hufananishwa na mtu au kitu kingine. Kwa mfano, mtu mlafi anaweza kuitwa fisi kutokana tabia ya ulafi ya mnyama huyo kama inavyotambulika katika ngano nyingi za Kiafrika. Kutokana na mazingira ya kisiasa yalivyokuwa wakati wa utunzi wa mashairi yaliyohakikiwa katika sehemu hii, baadhi ya washairi waliamua kutumia jazanda katika kumsawiri mwanasiasa wa Afrika. Hali hii ilitokana na ukosefu wa uhuru wa kujieleza na hatari zilizowakabili washairi kama baadhi ya wakosoaji wa serikali kama tulivyoona hapo juu. Ili kufanikisha usawiri huu, washairi hawa waliwasawiri wahusika wao kiubunifu, bila kuwataja moja kwa moja, kama inavyosisitizwa na nadharia ya Ulimbende ambayo iliongoza utafiti huu. Abdalla (1973) anachukua mtazamo hasi kwa kuwalinganisha wanasiasa wa kipindi cha baada ya uhuru na jipu, mamba, mkwezi dhalimu na misumari. Kwa upande mwingine, Mberia (2007) analeta taswira ya mwanasiasa kielelezo anapomlinganisha aliyekuwa rais wa Tanzania, marehemu Mwalimu Julius Nyerere na mwashi.

5.2.2.1 Wakatili

Katika shairi litwalo 'Jipu' (uk. 7), Abdalla (1973) anamsawiri mwanasiasa kama jipu, yaani uvimbe wenye uchungu mkali. Anatanguliza ufafanuzi wa dhiki iliyomkumba gereza kwa maneno haya:

3

Nna *jipu* lintunza, linipalo tabu mno
Tangu liliponianza, kamwe sipati usono
Kwamba ni mara ya kwanza, kuuguwa ndwezi hino
Latoma kama sindano, utunguwe nakwambia

Hali ya kuwa chini ya uongozi dhalimu inalinganishwa na kuugua *jipu* ambalo uchungu wake unamnyima mwananchi usingizi. Hii inaashiria ukatili uliozuka katika kipindi cha baada ya uhuru nakuwanyimawananchi utulivu. Viongozi wasiofaa waliwatia uchungu mkali sawa na ule unaotokana na *jipu*.

Ubeti wa 5 unaendelea kusimulia mashaka yaliyompata mshairi. Mshairi anafichua kuwa *jipu* hili liko makalioni na kamwe mhusika hawezi kuketi kutokana na maumivu. Mshairi analilia hali yake hivi:

5

Hitaka keti siwezi, kwamba li makaliyoni
Kutwa huwa yangu kazi, kusimama; ntendeni?
Na usiku usingizi, siupati aswilani
Kucha nakesha mwendani, kwa utungu kuzidiya

Hoja inayosisitizwa kutokana na taswira ya *jipu* lililo makalioni ni kuwa wanasiasa wabaya waliwasinya mno wananchi. Wananchi hawa waliingiwa na ghadhabu kali ambayo iliwanyima raha kiasi cha kutopata usingizi huku wakiwaza jinsi udhalimu huu ungeondolewa.

Kufikia mwishoni mwa shairi, mshairi analinganisha juhudi za kuwaondoa wanasiasa wabaya na uchungu wa kuliminya *jipu*. Anaueleza uchungu huu na furaha itakayoandama hatimaye kama ifuatavyo:

7

Jambo nilingojevalo, ni kutimu yake siku
Ningojevalo ni hilo, tena kwa kubwa shauku
Itimupo ndimi nalo, ja mwewe na mwana kuku
Ni furaha hiyo siku, kwangu na wenzangu piya

8

Siku ya kuiva kwake, hiyo ndiyo siku kweli
Huo ndiwo mwisho wake, na mwisho wa idhilali
Idhilali in'ondoke, mimi nayo tuwe mbali
Siku hiyo ni mawili, kuteka au kuliya

Shauku ya mshairi na ile ya wadhulumiwa wenzake kuhusiana na uwezekano wa kuondolewa kwa wanasiasa dhalimu inadhihirika katika shairi hili. Mshairi anaonekana kujitolea kikamilifu kuhakikisha kwamba udhalimu unasitishwa na uhuru kamili kupatikana.

Juhudi zaidi za mshairi za kuondoa udhalimu zinadhihirika vyema katika ubeti wa 9. Mshairi anaonekana kuwa tayari kuumia ilimradi udhalimu uondoke, kama anavyosisitiza hapa:

9

‘Taliminya litumbuke, lisinisumbuwe tena
Usaha wote utoke, utoke nikiuona
Midamu itiririke, kama ng’ombe alonona
Jipu hili mwana lana, Mn’gu mbwalipa hizaya

Kuondoka kwa jipu pamoja na usaha wake ni ishara ya kuwaondoa kabisa wanasiasa waovu pamoja na vibaraka wao. Umwagikaji wa damu unaashiria kuwa mshairi yuko tayari kwa machungu na hasara yoyote inayoweza kusababishwa na juhudi za ukombozi.

Ili kudhihirisha nia yake ya kuwaondoa viongozi dhalimu, Abdalla (1973) anatangaza msimamo wake kuhusiana na ukombozi wa wanyonge kupitia shairi liitwalo ‘Naja’ (kur. 77-78). Katika shairi hili, mshairi anawasawiri wanasiasa wa baada ya uhuru kama misumari hatari inayodunga umma na ambayo sharti ing’olewe. Ingawa anakiri kuwa kukabiliana na wanasiasa hawa kuna hatari zake, mshairi anashikilia kuwa dhuluma haina budi kuondolewa. Msimamo huu unadhihirika katika ubeti wa 8 na 9 anaposema:

8

Naja na ambao kwamba, mwaningoja kwa vihendo
Wazidi kukaza kamba, wasizibadili nyendo
Wangajiita ni simba, sitazicha zao kondo
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini

9

Naja huu wangu moyo, hauningii mdundo
Sitatishika kwa hayo, niyazowele maondo
Mimi kutishika nayo, huo siwo wangu mwando
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini

Katika beti hizi, mshairi anawasawiri wanasiasa ambao hawako tayari kuacha udhalimu. Madhalimu hawa wanaendelea kuwaumiza wananchi sawa na misumari iliyodunga mitini na kugandama pale. Ili kuondoa misumari hii ya kisiasa, sawa na inavyofanywa misumari ya kawaida, panahitajika nyundo. Ndiposa mshairi anajilinganisha na nyundo na kuwatahadharisha viongozi dhalimu kuwa ingawa wamemdhaliisha kifungoni, punde tu atakaporejea nyumbani atawang'oa. Huu ni wito wa mshairi kwa umma kuwa wanasiasa wasiofaa kuwepo uongozini hawana budi kubanduliwa.

5.2.2.2Wenye Kiburi

Mshairi huyu pia anawalinganisha wanasiasa dhalimu wa kipindi cha baada ya uhuru na mamba. Shairi liitwalo 'Mamba' (uk. 10) linamsawiri mwanasiasa huyu kama mamba aliyekaa mtoni ambapo anajigamba na kujitia uhodari huku akijiona kama ataishi pale milele. Ubeti wa pili wa shairi hili unasema hivi:

Kuna mamba, mtoni metakabari
Ajigamba, na kujiona hodari
Yuwaamba, kwamba 'taishi dahari

Memughuri, ghururi za kipumbavu
Afikiri, hataishiwa na nguvu
Takaburi, hakika ni maangavu

Katika ubeti huu mshairi anawasawiri wanasiasa ambao, baada ya nchi za Afrika kupata uhuru, waliingia mamlakani na kuanza kujiona kama wangedumu mamlakani milele. Jazanda hii ya mamba inaonyesha jinsi viongozi hawa walivyokuwa hatari kwa wananchi. Mshairi anawalinganisha wanasiasa na mamba ambaye huwaua na kuwala wanyama wengine waendao mtoni, wakiwemo binadamu. Maji ya mto pia yanaweza kulinganishwa na rasilimali za kitaifa ambazo zinafaa kumnufaisha kila mwananchi.

Jazanda iliyojitokeza hapo juu inaweza kulinganishwa na hali ilivyokuwa nchini Kenya wakati wa uongozi wa Mzee Kenyatta. Akivaga, (2002) anaeleza kuwa baada ya Wakenya kumtukuza Mzee Kenyatta kwa kuwa mzalendo aliyeongoza katika vita vya kupigania uhuru, kiongozi huyu aliwasaliti kupitia sera zake za kisiasa na kiuchumi. Aliibadilisha katiba ya taifa mara kadha ili kujipatia mamlaka makuu. Hali

hii ilisababisha ukandamizaji mkubwa wa wapinzani wake huku akiingilia utendakazi wa bunge na mahakama.

Kutokana na hali ya wananchi kutoridhishwa na sifa zilizotajwa hapo juu, mshairi anawaonya viongozi hawa kuwa hata wakitumia vitisho utawala wao hatimaye utafika mwisho. Abdalla (1973) anatoa onyo hili:

Akumbuke, siku yake ikifika
Roho yake, ajuwe itamtoka
Nguvu zake, kikomoche zitafika

Afahamu, mtu hajui la kesho
Hatadumu, angatumia vitisho
Maadamu, lenye mwanzo lina mwisho

Katika beti tulizonukuu hapo juu, mshairi anatoa onyo kali kwa wanasiasa dhalimu. Anataka wafahamu kuwa hata wakitawala kwa mabavu kwa muda mrefu kiasi gani, hatimaye watakufa, sawa na binadamu wengine. Hii ni kwa sababu kila jambo lililo na mwanzo lina mwisho wake.

5.2.2.3 Wenye Wivu na Ujeuri

Mabadiliko ya mwanasiasa wa Afrika katika kipindi cha baada ya uhuru yanajitokeza pale anaposawiriwa kama mkwezi mwenye wivu. Mkwezi ni mtu anayepanda mnazini ili kuangua nazi. Katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*, mshairi anazua mgogoro kati ya wahusika Alii na Badi katika shairi liitwalo 'Mnazi: Vuta N'kuvute' (kur. 17-22). Katika shairi hili tunaona kuwa Badi anapokwea mnazini kuangua nazi anakatalia kule juu na kudai kwamba mnazi ule ni wake licha ya kuwa yeye na ndugu yake waliurithi kutoka kwa wazazi wao. Shairi linaanzia hivi:

ALII
Ndugu ulo mnazini, wanitafuta balaa
Nakwambia shuka tini, katakata wakataa
Wafanya ni masakani, mustarehe 'mekaa
Utashuka au la?

BADI
Ndugu tini ya mnazi, nilo juu nakujibu
Haya ni ya upuuzi, unambiyayo swahibu
Kushuka tini siwezi, pasi kujuwa sababu
Hiyo ni yangu jawabu

Mgogoro unaojengeka hapa unadhihirisha madharau makubwa kutoka kwa viongozi wa Afrika waliochukua madaraka katika serikali ya kwanza baada ya uhuru. Alii, ambaye anawakilisha umma, anamsihi Badi ashuke chini ya mnazi na kumlaumu kwa kustarehe pale juu. Badi, ambaye anawakilisha kiongozi dhalimu, anamjibu Alii, anayewakilisha umma, kuwa madai yake ni upuuzi mtupu na kwamba yeye hawezi kushuka bila kuelezwa sababu. Katika ubeti unaofuata Alii anajaribu kumweleza Badi sababu ya kumtaka ashuke:

ALII

Sababu ya kukwambiya, ya kwamba ushuke tini
Ni kuwa nataka kweya, huko juu mnazini
Kwa ajili nami piya, nitunde nazi mwendani
N'shakweleza kwa nini

Kutokana na maelezo haya, ni bayana kuwa mnazi huu unafaa kuwanufaisha wahusika hawa wawili. Ni dhahiri pia kuwa Alii na Badi wana haki sawa ya kujiangulia nazi. Hii inamaanisha kuwa viongozi walioanza kujilimbikizia mali mara tu uhuru ulipopatikana hawakuzingatia haki na uadilifu. Wananchi pia walihitaji rasilimali za kitaifa ambazo wanasiasa walianza kuhodhi kwa tamaa kubwa.

Katika ubeti ufuatao tunawaona wanasiasa wa baada ya uhuru waliojaa jeuri na kiburi. Baada ya Alii kumweleza Badi sababu za kumtaka ashuke mnazini, Badi anamwonyesha madharau na kumwita mwendawazimu. Aidha, Badi anaendelea kushikilia kuwa mnazi ni mali yake na kwamba hawezi kamwe kumwachia Alii kuangua nazi. Mazungumzo yao yanaendelea hivi:

BADI

Hayo ni ya kutekesha, unambiyayo ndu yangu
Wataka niteremsha, juu ya mnazi wangu?
Wanistaajabisha, kuniamuru kwa changu
Una kishaa mwenzangu

ALII

Sina kishaa sinani, akili yangu kamili
Ni wewe usobaini, pale ulipo ukweli
Mnazi ni tangu lini, ukawa ni yako mali?
Sinitendee feeli

Mazungumzo haya yanaonyesha vile wanasiasa wa baada ya uhuru walianza kupuuza ahadi zao kwa wananchi. Katika sura ya nne tuliona jinsi wanasiasa hawa waliwapa wananchi matumaini makubwa ya maisha mema baada ya kumwondoa mkoloni. Ahadi hizi ndizo zinazomfanya Alii (mwananchi) kushangaa ni vipi mnazi, yaani rasilimali za kitaifa ukawa mali ya Badi (mwanasiasa) peke yake. Ung'ang'aniaji wa rasilimali, kama unavyodokezwa katika nadharia ya Baada-Ukoloni unadhihirika hapa.

Ili kujitetea kutokana na dhuluma hii, Alii anamkabili Badi na kumkosoa kuhusiana na madai yake juu ya umiliki wa mnazi. Alii anasema kuwa mnazi huu ni wa shirika kwani waliachiwa na wazazi wao; hivyo Badi hana haki yoyote ya kumzuia kujitundia nazi. Alii anasema hivi:

ALII

Mnazi ni wa shirika, mimi na wewe mwendani
Unshakuwa wataka, kunitowa shirikani?
Hilo halitatendeka, wala haliwezekani
Sikubali abadani

Takupa habari yake, kama wewe hufahamu
Kutokeya mwanzo wake, hata leo ikatimu
'Takweleza utosheke, kwa maelezo timamu
Ujuwe sina wazimu

Mnazi yake aswili, uli mbwa wazazi wetu
Mbwa baba zetu wawili, pasi kungiya wa tatu
Mali yao ya halali, hawakunyang'anya watu
Sasa wafile ni wetu

Katika beti hizi mshairi anawasilisha mawazo ya wananchi kuhusiana na rasilimali za kitaifa. Wananchi wanalalamikia kutengwa na wanasiasa katika ugawanyaji wa rasilimali ilhali rasilimali hii ni haki ya kila mmoja wao. Hatua iliyokosolewa na Abdalla (1973) katika shairi hili ni ujilimbikiziaji mali unaotekelezwa na wanasiasa bila kujali maslahi ya umma, jambo ambalo limejadiliwa pia na Kelly (2014).

Mshairi pia anawasawiri wanasiasa waliobadilika baada ya uhuru na kujawa na wivu. Wivu huu unafafanuliwa katika shairi hili pale Badi anapomtaka Alii kumweleza kati ya wazazi wao wawili ni nani aliyekuwa na fungu kubwa katika ule mnazi. Badi anamsaili Alii:

BADI

‘Takukatiza kauli, niwia radhi mwenzangu
Hapa ninayo suali, ikerayo moyo wangu
Katika hawa wawili, pasi kungiya wa tatu
Yupi mwenye kubwa fungu?

Ni dhahiri hapa kuwa wivu uliowajaa wanasiasa uliwafanya kuhisi vibaya wananchi waliponufaishwa na rasilimali licha ya kuwa wanasiasa hawa hawakuifanyia kazi yoyote. Hali ya Badi kushikilia kuwa babake ndiye aliyekuwa na fungu kubwa kuliko la babake Alii katika umiliki wa mnazi pia inazua suala la kizazi cha wanasiasa na wananchi wa tabaka la chini. Inadhihirika hapa kwamba wanasiasa walijiona kuwa kizazi bora zaidi kilichofaa kupata fungu kubwa wakilinganishwa na wananchi.

Suala la ujenzi wa tabaka pia linadhihirika katika shairi hili. Alii anaturejesha nyuma na kutueleza jinsi mambo yalivyokuwa kabla ya wanasiasa kuzua tabaka la juu na tabaka la chini. Alii anamlaumu Badi kwa kumdhulumu kinyume na hapo awali ambapo walitumia rasilimali kwa ushirikiano. Alii analalamika:

ALII

Pamoja tulipokuwa, vyetu tukivitanganya
Jambo moja hagunduwa, ulokuwa ukifanya
Hukuwa kinipa sawa, wakati wa kugawanya
Changu ukinipokonya

Mawazo haya ya Alii yanaonyesha kuwa hakukuwepo na utabaka kati ya Waafrika kabla ya uhuru. Mwanasiasa wa Afrika ndiye aliyeujenga utabaka huu punde tu alipoanza kujipendelea wakati wa kugawana rasilimali. Hata hivyo, haikuchukua muda mrefu kabla umma haujagundua udanganyifu huu na kuanza kudai haki sawa na wanasiasa. Ndiposa Alii analalamika katika ubeti ufuatao kuhusiana na tofauti kubwa iliyokuwepo kati ya jamii za wanasiasa na zile za wananchi wa kawaida. Alii anasema:

Mwerevu ulijidai, fungu kubwa ukitwaa
Wanayo wala miyai, na vyakula vya kufaa
Wala hata hakinai, kwa mitumbo kuwajaa
Na nguo njema wavaa

Hali kuwa wangu wana, wadhii mno kwa ndaa
Ndiyani ukiwaona, ni mitambara ‘mevaa
Ni kwa kuwa kitu sina, kuwapa nilowazaa
Kwa wewe changu kutwaa

Alii hapa anaweka wazi jinsi wanasiasa wa baada ya uhuru walivyojitwalia mali ya umma na kuzinufaisha familia zao. Kwa upande mwingine, familia za wanyonge ziliishi kwa dhiki. Tunaona Alii akilalamika vikali kuwa watoto wa wanasiasa wanaishi raha mustarehe kwa kula mayai na vyakula vingine vya kufaa. Isitoshe, watoto hawa wanavaa nguo nzuri wakilinganishwa na wale wa maskini wanaoumia kwa njaa huku wakivaa matambara. Kinachomuudhi Alii zaidi ni kuwa wanasiasa hawa bado hawaridhiki - wanaendelea kuwanyanyasa wanyonge ambao hawawezi hata kuzikimu familia zao.

Mjadala kuhusu ugawaji wa rasilimali unaendelea katika beti zinazofuatia. Badi anapoonekana kumlaumu Alii kwa kutoridhishwa na kidogo anachopata. Badi anadai kuwa iwapo Alii angaliridhika na kukubali kunyanyaswa, mzozo kuhusu ugawanyaji wa rasilimali usingalikuwapo kamwe. Badi anasema:

BADI

Wanambiya nilikuwa, kilo kichache hikupa
Nami kingi hitukuwa, wanangu henda kiwapa
Ndiyo sababu wakawa, wanangu wamenenepa
Na nguo njema kuwapa

Makosa haya si yangu, ya wanayo kudhikika
Lau hilo dogo fungu, kwalo ungaliridhika
Watoto wako ndu yangu, wasingelitaabika
Bali hili hukutaka

Uliona ni vizuri, kichache kutokubali
Ukafanya nyingi ari, ya kukiwata kalili
Ni heri nusu ya shari, kuliko shari kamili
Au hufahamu hili?

Madai anayotoa Badi hapa yanaonyesha jinsi wanasiasa wa baada ya uhuru walivyokuwa na ujeuri na ugumu wa mioyo. Tunachoshuhudia hapa ni kizazi cha viongozi wasiojali kamwe matatizo yaliyowakabili wananchi waliowachagua. Badala ya kuwasaidia wananchi, wanasiasa waliwalaumu kwa kutoridhika. Aidha, wanasiasa walijaribu kuwafanya wananchi kuamini kuwa hali waliyopitia ni majaliwa.

Kwa upande wake, wananchi waliwakosoa viongozi waziwazi kwa kuwafahamisha kuwa dhuluma sio majaliwa na hawakuikubali kamwe. Alii, ambaye anawawakilisha wanyonge katika shairi hili, anatangaza msimamo wa umma kwa maneno haya:

Lau kama ningekuwa, ‘meliridhi jambo hili
Ingeonesha ya kuwa, hiyo ni moja dalili
Ya kwamba kudhulumiwa, mwenyewe nimekubali
Na hali hili si kweli

Maneno haya yanaonyesha kuwa hakukuwa na mkataba wowote kati ya wanasiasa na umma kuwa wanasiasa wanufaike zaidi kutokana na rasilimali za kitaifa. Ni dhahiri kuwa haki za wananchi zilikuwa zikikiukwa na wanasiasa.

Katika ngonjera hii tumeona jinsi wanasiasa wa Afrika walivyowavunja mioyo wananchi na kuwafanya kutofurahia matunda ya uhuru. Kupitia wahusika Alii na Badi tumeona kuwa wanasiasa hawa waliiga dhuluma za kikoloni na kuwanyanyasa wananchi. Isitoshe, wanasiasa hawa hawakuwa na nia yoyote ya kuwasikiliza wananchi na kurekebisha makosa waliyowatendea. Badala ya kutoa suluhu kwa matatizo yaliyowakumba wananchi, wanasiasa waliutaka umma kuamini kuwa dhuluma walizotendewa zilikuwa majaliwa. Hata hivyo, kufikia mwisho wa shairi tunaona umma ukiwa na msimamo thabiti kuhusiana na haki yake ya kujikomboa. Mshairi, kupitia sauti ya Alii, anasema kuwa sharti umma uzinduke na kutambua kuwa umedhulumiwa kwa muda mrefu. Aidha, mshairi anawatahadharisha na kuwaapia wanasiasa kuwa kuna siku atakayochoka kuvumilia dhuluma. Siku hiyo ukweli utadhihirika na dhuluma kuondolewa.

5.2.2.4 Mwalimu Julius Nyerere: Mwanasiasa Kielelezo

Licha ya kuwasawiri wanasiasa wa baada ya uhuru kama viongozi wenye dosari, washairi wa Kiswahili hawakupuuza ukweli kwamba sio wanasiasa wote wa kipindi hicho walikuwa wabaya. Mberia (2007) anamsifu aliyekuwa Rais wa Tanzania marehemu Mwalimu Julius Nyerere kwa juhudi zake za kuwaunganisha Watanzania. Katika shairi lake liitwalo ‘Mwashi’ (kur. 40-42), mshairi anamsawiri Mwalimu Nyerere kama mjenzi imara aliyeifahamu kazi yake. Katika shairi hili, mshairi anazungumza moja kwa moja na kiongozi huyu ambaye keshakufa kama ana uwezo wa kumsikiliza. Ushairi unatambulika kama chombo cha kuendeleza mazungumzo

katika viwango kadha, ikiwa ni pamoja na mhusika kujizungumzia kana kwamba anawasiliana na watu ambao hawako hai (M’Ngaruthi, 2012).

Kwa mujibu wa mtunzi huyu, Mwalimu Nyerere alikuwa kiongozi kielelezo kwa wanasiasa, sio tu wa wakati wake, bali pia wa baadaye. Mshairi anamsifu kwa maneno yafuatayo kutoka kwa ubeti wa tatu:

Ulikuwa mwashi aliyekolea ujuzi:
Kiswahili na usawa wa makabila
Ulizifanya mawe adimu ya ujenzi
Matamshi yaliyochujua kwa kichungi
Na maisha yaliyometameta maadili
Yaliyokuwa saruji ya chapa ya kutajika
Sasa tuna msingi imara wa taifa

Katika ubeti huu mshairi anatambua juhudi za Mwalimu Nyerere katika kuendeleza Kiswahili, ambayo ni lugha ya wenyeji, kama chombo cha kuunganisha Watanzania. Aidha, anamsifu kwa uzungumzaji wake uliojaa busara na pia maisha yake ya uadilifu. Sifa hizi, kwa mujibu wa mshairi, ndio msingi uliojengewa nchi ya Tanzania. Uzalendo, ambayo ni sifa muhimu aliyokuwa nayo mwanasiasa wa kabla ya uhuru, ndio uliotarajiwa kuendelezwa na mwanasiasa wa Afrika baada ya uhuru.

Mshairi anaendelea kumpamba Mwalimu Nyerere kwa kumlinganua na viongozi wenzake wa mataifa ya Afrika. Anampongeza kwa kuongoza kwa unyenyekevu na hatimaye kung’atuka kutoka uongozini bila kushurutishwa. Mshairi anasema hivi:

Tofauti na wenzako waliolewa chakari
Kwa kunywa pombe haramu ya ujeuri
Wakabakia kubwakia kama mbwa hatari
Kulinda mapochopocho yasiponyoke,
Kinyume na wanaojiinua kwa ngazi ya tamaa
Na kujiweka kwenye vilele vya miparamuzi
Tayari kuvamia wapinzani kutoka angani,
Tofauti na wanaotesa pua za wananchi
Wanaogandama ikulu kama dondandugu,
Ulipogundua ukuukuu katika damu yako
Hukusema “Nchi hii ni mimi!”
Uliinuka bila mieleka na mikwaruzano
Na kuacha usukani mikononi mipya

Mwalimu Nyerere anasifiwa katika kifungu hiki kwa kuzingatia demokrasia katika uongozi wake. Huu ni mtindo tofauti na ule wa wenzake wanaokashifiwa kwa kujiinua na kujaa tamaa ya mali na uongozi. Aidha, Mwalimu Nyerere hakuwakandamiza wapinzani kama tulivyoshuhudia wenzake wakifanya katika sehemu iliyotangulia. Alithamini maoni ya Watanzania wenzake pamoja na uwezo wa viongozi wachanga wa kuendeleza taifa. Hii ndiyo sababu alitoka uongozini kwa hiari na amani.

Kwa kuhitimisha ujumbe wake kwa kiongozi huyu msifika, mshairi anamwambia hivi:

Mwashi, umetuachia kumbukumbu adimu
Zinazometameta kama vipande vya almasi
Nyoyo zetu zinasema: “Afrika Hoyee!”
Ndipo mshairi anakuita kwa heshima
Uinuke, akuvishe koja la maua ya kuteua
Ewe, chemchemi ya fahari ya Mwafrika!

Sifa ambazo mshairi anamrundika Mwalimu Nyerere katika ubeti huu ni tofauti kabisa na sifa mbovu zilizawatambulisha wanasiasa wenzake katika mashairi yaliyohakikiwa hapo awali. Mshairi huyu anamtaja Mwalimu Nyerere kama chemchemi ya fahari ya Mwafrika. Hii ina maana kuwa kiongozi huyuanastahili kusifiwa na kukumbukwa, sawa na wanasiasa wengine maarufu wa Afrika kama vile Kwame Nkrumah (Ghana), Sekou Toure (Gine), Samora Machel (Msumbiji) na Nelson Mandela (Afrika Kusini).

5.3 Vuguvugu la Vyama Vingi

Katika sehemu hii tunaangazia diwani ya *Chembe cha Moyo* iliyoandikwa na Mazrui (1988). Kimuundo, mashairi yaliyohakikiwa katika sehemu hii ni aina ya mashairi huru. Mashairi tuliyochunguza katika sehemu iliyotangulia, isipokuwa shairi la Mberia (2007) liitwalo ‘Mwashi’ ni yale ya kiarudhi. Kimsingi, utunzi wa aina hii hushikilia kuwa shairi la Kiswahili sharti liwe na vina na mizani. Kazi ya Mazrui (1988), ambayo tunachunguza katika sehemu hii inajumuisha mashairi huru yasiyozingatia vina na mizani. Nadharia ya Ulimbende inasema kuwa kilicho muhimu katika ushairi ni uwasilishaji wa hisia za mshairi kupitia usawiri wa wahusika unaozingatia mazingira wanamopatikana wala sio arudhi. Uzingatiaji wa

aina hii ya mashairi unadhihirisha kuwa usawiri wa wahusika wa kisiasa hauathiriwi kamwe na kuwepo au kutokuwepo kwa arudhi.

Katika tungo zake, Mazrui (1988) alijikita katika kipindi ambacho mataifa ya Afrika yalikuwa yakipigania uanzishwaji wa siasa za vyama vingi. Mshairi huyu alilenga kuuhamasisha umma juu ya dhuluma walizotendewa na viongozi wa kisiasa na vibaraka wao katika kipindi cha siasa za chama kimoja. Sawa na Abdalla (1973), mshairi huyu aliyatunga mashairi yake akiwa mfungwa katika Gereza la Kamiti. Kuwepo kwa kazi za fasihi kama hizi ni ushahidi kuwa maandishi mengi ya kifasihi huchochewa na mazingira ya kisiasa wakati wa utunzi (Waliaula, 2009).

Usawiri wa mwanasiasa wa Afrika katika sehemu hii, sawa na ilivyokuwa katika sehemu ya kwanza ya sura hii, unaendelezwa kijazanda. Katika tungo zake, Mazrui anawaita wanasiasa vinyago, vingingi vikavu, wala njama, majitu manene mazito, mafunza, tabaka dhalimu na wanaharamu. Hebu tuangalie usawiri huu hatua kwa hatua.

5.3.1 Vibaraka

Katika shairi litwalo ‘Vinyago’ (kur. 20-21) mshairi anawakejeli wanasiasa wa kipindi cha udikteta wa chama kimoja. Mtunzi anawasawiri wanasiasa hawa kama watu wanaochechemea na kupepesuka; wasio na mwelekeo. Mshairi anaufungua utungo wake kwa kuzungumza na wasomaji wake akiwataka wafumbuke macho na kuuona udhaifu wa wanasiasa wanaowaongoza. Shairi linaanza hivi:

Waangalieni

Wale wanaotuongoza

wanavyochechemea

wanavyopepesuka

mara huku mara kule

mara hapa mara pale

kila mahali ulimwenguni.

Wale wanaotuongoza

pingu mikononi

pingu miguuni

pingu maningani

Katika vifungu hivi tunawaona viongozi ambao ni vikaragosi wa nchi za kimagharibi. Mshairi anatusawiria uongozi dhaifu ambao viongozi wake ni vinyago wasioweza

kujiamulia chochote bila kupokea maagizo kutoka nchi za nje. Taswira ya vinyago wenye pingu mikononi, miguuni na machoni inaashiria kudhibitiwa kwa hali ya juu. Mtu aliyetiwa pingu mikononi, miguuni na machoni amedhibitiwa kiasi kwamba hawezi kutenda chochote, kutembea popote au hata kujionea chochote bila idhini ya aliyemdhhibiti.

Katika kifungu kinachofuata, mshairi anawasawiri wanasiasa wa Afrika kama watu waliopenda kusifiwa na kutukuzwa. Anasimulia jinsi walivyotawala kwa kuwapumbaza wananchi kiasi cha kuwafanya vinyago vya sarakasi. Inaelekea hapa kuwa baada ya kudhibitiwa na nchi za Magharibi, wanasiasa wa Afrika walitafuta pia mtu wa kumdhhibiti. Bila shaka mtu huyu ni mwananchi. Mshairi analalamika hapa kwa niaba ya umma:

Tumeshindana katika huu mchezo waliotufunza
Tukichezeshwa miili yetu, tukiitambaza kama mafunza
Tukipanua makanwa na midomo
tukitingisa matako na viuno
tukitoa mashuzi na misono
huku haya zote tumezibanza.

Kifungu hiki kinarejelea kipindi cha udikteta wa chama kimoja cha kisiasa ambapo baadhi ya viongozi wa Afrika waliwafanya wananchi vyombo vya kuwatumbuiza na kuwastarehesha. Tunaona hapa jinsi wananchi walivyowaimbia na kuwachezea ngoma wanasiasa bila kujali kujiabisha, bora tu wawafurahishe wakuu wao. Katika kipindi hicho nyimbo za taarab, ambazo ni tungo kamili za kishairi, zilitungwa na kuimbiwa wanasiasa. Sifa walizolimbikiziwa wanasiasa hawa ziliwafanya kujawa na kiburi na kuwadharau wananchi (Mwamzandi, 2002).

Isitoshe, kila walipoenda, wanasiasa hawa walikaribishwa kwa taadhima na wananchi ambao hawakuwa na hiari ila kuwatumikia wakuu. Katika kifungu kifuatacho mshairi anaonyesha jinsi mambo yalivyokuwa:

Haya basi, tupigeni mayowe
tupigeni makofi
ili wakuu wacheke
ili wakuu wafurahike

Haya!
Haya!
Haya!
Hiyo ndiyo kazi yetu
Kwani tu vipofu
Kuliko hao vipofu!

Wazo linalojitokeza hapa ni kuwa wananchi waliokuwa wakiwatumikia wakuu hawa pia walikuwa na dosari. Mshairi anawakosoa hapa kwa kusema kuwa, sawa na viongozi wao walioonekana kama vinyago walipoenda ng'ambo, wananchi pia walikuwa vipofu. Hii inamaanisha kuwa sawa na viongozi wao walioyatii maagizo ya mataifa ya Kimagharibi bila kuyasaili, wananchi pia walikosea kwa kuwatumikia wanasiasa kama watumwa. Ni dhahiri kuwa wananchi hawa hawakuwa na uhuru wa kuwakosoa wanasiasa, kama inavyobainishwa na nadharia ya Baada-Ukoloni.

5.3.2 Wapinga Demokrasia

Kupitia shairi litwalo 'Taji la Wema' (uk. 26) Mazrui (1988) anawasawiri wanasiasa waliopinga demokrasia ya vyama vingi kama vingi vikavu ambavyo sharti vikatwe. Wafuasi wa nadharia ya Uhalisia kama vile Hobbes, Spinoza na Rousseau waliipa nadharia hii mtazamo wa kimaksi ambao unaunga mkono uondolewaji wa viongozi dhalimu kwa kutumia nguvu.

Kwa mujibu wa Mazrui (1988), kuviondoa vingi hivi kunahitaji ushirikiano wa wananchi. Ndiposa mshairi akatoa wito huu kwa wananchi:

Njooni basi, njooni tusafishe njia
Tuteme vingi vikavu vilojikita
Wafuasi vipofu na wafalume pia
leo siku zao zimetimilia

Katika ubeti huu wanasiasa na vibaraka wao wanasawiriwa kama vizingiti vinavyokinza maendeleo. Katika hali ya kawaida, vingi vikavu huwakwaza wanaotembelea eneo vilivyoko na pia kuwazuia kutekeleza wajibu walionuia kuutekeleza. Aidha, vingi vikavu vinaweza kutumiwa kama vifaa vya kuwafungia

wapinzani wanapokandamizwa na wanasiasa dhalimu. Ili kupatikana kwa uhuru wa kujiendeleza bila kukwazwa, mshairi anapendekeza kuwa wanasiasa wa aina hii pamoja na wafuasi wao waondolewe. Hata hivyo, mshairi hatoi pendekezo la jinsi ya kuwaondoa wanasiasa hawa.

5.3.3 Wenye Ubinafsi

Taswira nyingine inayojitokeza kuhusiana na wanasiasa wa kipindi cha baada ya uhuru ni ile ya 'wala njama'. Mazrui (1988) anaeleza jinsi wanasiasa hupanga vikao vya faragha na kupanga jinsi wangewakandamiza wananchi. Katika shairi liitwalo 'Kula Njama' (uk. 44) mshairi analalamika kuhusiana na njama za wanasiasa:

Nimetatizwa na tatizo moja
Hawa mabwana zetu tuishio nao pamoja
hawashushi pumzi kwa mdundo mmoja
kutuona hatuna ngoma,
twatosheka na kungoja?
Na hawa mabwana zetu,
hawakai baraza moja, kwengine na kwetu
wakipika na kupanga
kunyonya kila tone la damu yetu?

Kile anacholalamikia mshairi ni jinsi wanasiasa wetu walivyojaa ubinafsi kiasi cha kupanga kuwaibia wanyonye wanaopaswa kuwatetea. Njama za aina hii huendelezwa na wanasiasa katika vikao mbalimbali likiwemo bunge. Matokeo yake huwa kuwaongeza wananchi mzigo wa ushuru pamoja na kukatwa mishahara kwa lengo la kuwanufaisha wanasiasa. Mshairi anatusawiria jinsi vikao vya aina hii huendelezwa:

Kwani hujaona ile milango ifungwayo,
faragha kubwa itafutwayo
na minong'ono inong'onezwayo?
Dhamira chafu...nakueleza hayo
Yaani, iwapo bado hunayo

Taswira inayojitokeza hapa ni ya watu wadanganyifu wasioujali umma bora tu wajinufaishe. Kwa mujibu wa mshairi, wanasiasa hawa huwa na dhamira chafu, ambayo ni kupora rasilimali ya umma. Hata hivyo, mshairi amewakashifu wanasiasa hawa bila kueleza iwapo mali wanayojilimbikizia huwanufaisha wananchi. Mara nyingi wanasiasa wanapojiongezea mishahara hudai kuwa nyongeza hiyo

ingewasaidia kukimu mahitaji ya wananchi wengi ambao mara kwa mara huwaomba msaada wa kifedha.

Licha ya wanasiasa kuulaumu umma kwa kuwaomba msaada wa kifedha, utafiti huu umetoa ushahidi kuwa nia ya wanasiasa mara nyingi huwa kujilimbikizia mali kote duniani. Katika mistari ifuatayo, mshairi anaifafanua lugha ya wanasiasa, ambao anawaita wala njama:

Lugha yao wala-njama?
Milki na faida, popote duniani!
Bei ya dhahabu ikiwaendea chini
Wenzetu wauawa kule migodini
kule kusini.

Faida ikiwapandia 'fika mbinguni
Sisi twala njaa kwetu mitaani.
Basi ukionacho ndicho ukipatacho!
Au bado hujaamini?

Kwa mujibu wa mistari hii, wanasiasa hujishughulisha tu na kile kitakachowatajirisha wala sio kuufaidi umma. Hawajali kamwe hatari zinazowakabili wananchi wanaofanya kazi zinazohatarisha maisha yao bora tu wanasiasa hawa wajinufaishe. Nia hii ya wanasiasa ya kujitajirisha na kutumia utajiri wao kudumu mamlakani pia inasisitizwa na nadharia ya Baada-Ukoloni ambayo iliongoza utafiti huu. Mfano halisi wa njama za aina hii ni pale wabunge kwenye Bunge la Kumi la Kenya walivyojipatia marupurupu makubwa baada ya kustaafu kwao katika kikao kilichofanyika bungeni usiku (*Daily Nation*, Januari, 11, 2013 uk. 1).

5.3.4 Wanyonyaji

Katika shairi hili la 'Wala Njama' wanasiasa pia wamesawiriwa kama majitu manene mazito na mafunza. Majitu na mafunza haya yanajificha na kuendelea kufurahia mali ya umma unaoendelea kuteseka kwa umaskini. Katika kifungu kifuatacho mshairi anayakejeli majitu na mafunza haya hivi:

Baina ya milki nyingi
na ile milolongo ya wasio-kazi
Baina ya faida nyingi
na vile vyumba vya mateso
vya watoto na wazazi
Kuna *majitu*
manene
mazito
yaliyojificha yakafichika
kama MAFUNZA chini ya mawe.

Katika kifungu hiki mshairi anatusawiria mazingira mawili yanayokinzana; mazingira ya kimaskini na yale ya kitajiri. Tunapata taswira ya matajiri wenye milki na faida nyingi waliozungukwa na maskini wengi wasio na kazi wanaoishi vibandani. Uendelezaji huu wa tabaka, ambao pia umebainishwa na nadharia ya Baada-Ukoloni, ndio mshairi anapinga na kulenga kuwepo kwa jamii isiyo na watu wanaowatumia wanyonge kujinufaisha.

Kwa kuwasawiri wanasiasa kama majitu manene na mazito, mshairi anaonyesha jinsi wanasiasa huendelea kujistawisha kutokana na rasilimali zilizopo na kujitenga mbali na maskini. Usawiri huu unaweza kulinganishwa na ule wa majitu yapatikanayo katika ngano za mazimwi na majitu kwenye fasihi simulizi ya jamii nyingi za Kiafrika. Majitu aghalabu huwa viumbe wa kutisha kwa ukubwa, wenye viungo visivyo vya kawaida kama vile jicho moja kubwa, jinywa lenye meno makali na vitendo viovu. Vitendo hivyo ni pamoja na kuwala mifugo wa wanajamii, kutisha kuiangamiza jamii nzima na wakati mwingine kukimeza kijiji kizima. Ni dhahiri kuwa ulinganishaji wa wanasiasa na majitu haya unawasawiri kama watu walafi, wasio na huruma na waliojaa udhalimu.

Taswira ya mafunza kwa upande mwingine inaashiria unyonyaji wa wanasiasa wa Afrika wakati wa siasa za chama kimoja. Kwa kawaida, mafunza ni vimelea wanaofyonza damu kutoka kwa binadamu kama njia ya kujipatia lishe. Vimelea hawafanyi kazi yoyote ili kujitegemea bali huwategemea wanyama, wadudu au binadamu kwa lishe. Kinaya kilichoko kwenye uhusiano kati ya funza na binadamu ni kuwa funza wanapoendelea kunawirika, binadamu anayewalisha hudhoofika kiafya.

Ulinganishi huu wa wanasiasa na funza ni ishara kuwa wanasiasa hawa waliwanyonya wanyonge waliowazingira na kujilimbikizia utajiri huku wananchi wakiumia kiuchumi na kijamii. Thibitisho la unyonyaji wa aina hii ni hali ilivyokuwa nchini Tanzania kabla ya Azimio la Arusha ambapo unyakuzi uliokithiri wa mali ya umma ulishuhudiwa. (Havnevik na Isinika, 2010). Unyakuzi wa ardhi ni suala ambalo pia lilidhihirika katika utafiti huu.

5.3.5 Wadhalimu

Tabia ya wanasiasa ya kuwatenganisha wananchi na kuwachochea kupigana si ngeni katika eneo la Afrika. Ili kuhakikisha kwamba wanasiasa wanaafikia malengo yao ya kujiendeleza kisiasa na kiuchumi, jamii hugawanywa kitabaka. Hali hii ndiyo inayojadiliwa na Mazrui (1988) katika shairi litwalo ‘Mwapigania kitu gani?’ (kur. 62-63).

Katika shairi hili mshairi anaonyesha jinsi wanasiasa huzua migawanyiko miongoni mwa wananchi na kulitumia kundi moja la wananchi hao kulinyanyasa kundi jingine. Baada ya kuchochewa na wanasiasa, wananchi huchukiana na hatimaye kupigana. Mizozo hii huwapa wanasiasa nafasi ya kupora mali ya umma. Ung’ang’aniaji wa mamlaka na kutaka kujidumisha mamlakani ni masuala muhimu yanayosisitizwa na nadharia ya Baada-Ukoloni. Katika kifungu cha pili wa shairi hili mshairi anashangaa:

Na kwa nini?!
Dunia inatetemeka
bila mavazi
bila malaji;
binadamu akiogelea katika ziwa la damu
ili *watu fulani*... ulimwenguni
wanufaike kwa kipande cha ardhi
... bila thamani.

Baada ya kushangazwa na misukosuko, umaskini na vita vinavyoikumba dunia, mshairi anasema kuwa haya yote hutokea kwa sababu ya *watu fulani*. Watu hawa, ingawa mshairi hawatambulishi moja kwa moja, ni wanasiasa wanaonufaishwa na bughudha wanayozua miongoni mwa wananchi. Mfano wa msukosuko wa aina hii ni ule uliowahi kusababishwa na aliyekuwa Rais wa Uganda, Idi Amin. Matokeo yake

yalikuwa kuzuka vita kati ya majeshi yake na yale ya Tanzania. Athari zilizofuatia zilikuwa pamoja na uharibifu wa mali ya wananchi na mauaji (Wanyande, 1997).

Mshairi anaendelea kutoa ushahidi kuhusiana na uharibifu na wizi wa mali ya umma kwa kufichua jinsi wanasiasa walivyowatenganisha wananchi. Lengo lao lilikuwa kujipatia vipande vya ardhi bila malipo yoyote huku wananchi wakiangamizana. Madai haya yanadhihirika katika kifungu kifuatacho:

Matapo ya watu
yakilia kama mafisi
waikata na kuichoma ngozi ya dunia
ili *watu fulani*
mahali fulani... ulimwenguni
waendeleo kuishi kwa jasho la wenzio
... bila imani

Kifungu hiki kinaendeleza sifa ya tamaa na ubinafsi wa wanasiasa kwa kuwalinganisha na fisi. Katika hurafa nyingi fisi husawiriwa kama mnyama mlafi. Vilevile, mnyama huyu hana ustaarabu wowote kwani huvamia mifupa na mabaki ya mizoga baada ya wanyama kama vile simba na chui kuwinda na kumaliza kula. Kwa kuwasawiri wanasiasa kama fisi, mshairi alilenga kudhihirisha jinsi binadamu hawa walivyo na ulafi wa kinyama.

Dhima ya ushairi kama chombo cha kuuzindua umma inadhihirika katika vifungu vifuatavyo:

Ewe unayejitolea roho yako
Lini utaizindua akili yako
Usimame wima kwa nguvu zako
Uwache kupigana na ndugu zako
... wadhulumiwa wenzako
ili *watu fulani* tu
waendeleo kusarifu unyonyaji
wa watu duniani
bila upinzani?

Ni lini

utaligeukia *tabaka dhalimu*
la taifa lako mahushumu

uliulize:

Nakipigania kitu gani?
Nampigania mtu gani?
Nayapigania maisha gani?

Katika vifungu hivi, mshairi anawakosoa wananchi wanaokubali kuchochewa na wanasiasa na kupigana miongoni mwao. Anawataka wananchi wazinduke na kuacha kuwaangamiza wananchi wenzao. Mshairi anawazindua wananchi ili wagutuke na kulipinga tabaka dhalimu na kulitaka liwaeleze manufaa ya kupigana wao kwa wao.

5.3.6 Watovu wa Maadili

Ili kuonyesha kutokubalika kwa wanasiasa dhalimu wa kipindi cha udikteta wa chama kimoja, Mazrui (1988) anawataja viongozi hawa kama wanaharamu. Katika matumizi ya kawaida, mwanaharamu ni mtoto aliyezaliwa na wazazi ambao hawakufunga ndoa. Pengine mshairi ametumia neno hili kuonyesha hasira yake kutokana na tabia ya wanasiasa hawa ya kutaka kujipatia mali ambayo ni haki ya watu wengine. Ushairi wa Kiswahili umethibitishwa kuwa sanaa iliyotumiwa kwa muda mrefu kutolea hisia mbalimbali ikiwemo ile ya hasira (M'Ngaruthi, 2007).

Kwa kuwasawiri wanasiasa kama wanaharamu, mshairi huyu analichukulia bara la Afrika kama mwanamke aliyetunga mimba kutokana na uhusiano na wakoloni. Matokeo yake ni kuzaliwa kwa kizazi cha viongozi haramu waliopotoka kimaadili kutokana na athari za wakoloni kiasi cha kutojijua. Kizazi hiki cha wanasiasa ndicho kinachozungumziwa na Hamisi (2011) ambacho hakiwajibiki wala kuzingatia maadili kazini bali huingilia vitendo viovu kama vile ufasadi na uzinzi katika afisi za umma. Mshairi anaanza kuisimulia kadhia hii kwa swali lifuatalo:

Hebu nikuulize Mama Afrika,
Kwa nini...
Mimba changa ukajichukulia
Ya haramu sana ilotepetea
Ukazaa wana walo jahilia
Wasiojijua, wala yao njia?

Kifungu hiki kinaashiria kuwa wanasiasa wanaorejelewa walikuwa wamekengeuka na kukiuka maadili ya jamii ya Kiafrika iliyowazaa. Hali hii iliwatia wananchi kiwewe na kuwafanya kukosa imani na viongozi wao. Dhiki iliyowakumba wananchi kutokana na tabia za viongozi hawa haramu inafafanuliwa katika kifungu hiki:

Ah moyo waumia!
Hupigwa na mshangao
Niwafikiriapo
Wale barobaro wanao
Wasaliti wanati walo na vyeo
Walomdhidi mama mzazi wao
Kwa mradi wao.

Mshairi hapa anawaita viongozi ‘wasaliti wanati walio na vyeo’ kwa maana kuwa viongozi hawa hawakuwatumikia wananchi kama walivyotarajiwa. Badala yake waliyadhulumu mataifa yao kwa lengo la kujifaidi wao binafsi.

Licha ya hali ngumu iliyoyakumba mataifa ya Afrika chini ya wanaharamu hawa, kufikia mwishoni mwa shairi hili mshairi anatabiri kwamba siku moja mambo yatabadilika na wanaharamu kuhalalika. Aidha, mshairi anatabiri kuwa siku hiyo itakapowadia dhuluma itakoma, kama inavyofafanuliwa katika kifungu hiki:

Lakini sijali
Sijali kwani najua
Siku moja itawadia
Wana-haramu watajihalalia
Kila cha haramu kukuondolea
Na kukutakasa
...mama wasikia?

Hiyo siku ya siku itakapofika
Kila la dhuluma litajikatika
Na kila mahali utadhihirika
Mwisho wa salata na uharamia
... mama wasikia?

Ni dhahiri kuwa mshairi alikuwa akitabiri juu ya mabadiliko makubwa yaliyotarajiwa katika bara la Afrika kufuatia kuanguka kwa mfumo wa siasa za chama kimoja. Mfumo wa siasa za vyama vingi uliibua matumaini mapya kutokana na kuondolewa kwa udikteta wa chama kimoja.

Katika sehemu inayofuata tutaangalia mawazo ya washairi mbalimbali kuhusiana na sifa za mwanasiasa wa Afrika tangu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi. Utafiti huu ulithibitisha kuwa mabadiliko ya kisiasa kutoka kwa mfumo wa chama kimoja hadi demokrasia ya vyama vingi haukubadilisha tabia za mwanasiasa za Afrika. Kwa

mujibu wa washairi ambao tungo zao zilihakikiwa, mwanasiasa wa Afrika bado hajajitolea kikamilifu kuwatumikia wananchi.

5.4 Kinaya cha Mabadiliko

Mfumo wa siasa za vyama vingi katika mataifa ya Afrika ulitarajiwa kuleta mabadiliko makubwa ya kisiasa na kijamii. Mabadiliko haya yalitarajiwa kusuluhisha matatizo mengi yaliyolikumba eneo hili wakati wa udikteta wa chama kimoja. Aidha, ilitarajiwa kuwa mfumo huu ungemaliza unyakuzi wa mali ya umma na wanasiasa wachache walafi. Licha ya matumaini haya, wanasiasa walianza kuvitumia vyama vya kisiasa walivyovianzisha kama vyombo vipya vya kujitajirisha na pia kuwanyamazisha wapinzani wao (Asingo, 2003).

Ili kudhihirisha sifa za wanasiasa hawa katika kipindi cha siasa za vyama vingi, utafiti huu ulishughulikia mashairi teule kutoka kwa diwani mbili. Diwani hizo ni *Diwani ya Karne Mpya* na *Msimu wa Tisa*. Mashairi yaliyohakikiwa kutoka kwenye *Diwani ya Karne Mpya* ni yale yaliyotungwa na Kyallo Wamitila, Omar Babu (Abu Marjan), Muchai bin Chui, Timothy Arege na Hezron Mogambi. *Msimu wa Tisa* ni mkusanyo wa mashairi yaliyotungwa na Kithaka wa Mberia. Sehemu zifuatazo zinajadili jazanda mbalimbali zilizotumiwa na washairi waliotajwa hapo juu kumfafanua mwanasiasa wa Afrika Mshariki.

5.4.1 Walafi

Kinaya cha mabadiliko ya mwanasiasa wa Afrika baada ya kuanzishwa kwa siasa za vyama vingi kinabainishwa wazi na Babu (2007). Babu anawasawiri wanasiasa hawa kama fisi wasiobadilisha tabia licha ya mpito wa wakati. Shairi lake liitwalo ‘Msitu ni ule ule’ (uk. 29) linaashiria hali ya kukata tamaa kwa mwananchi ambaye alitarajia mabadiliko makubwa baada ya kuangamizwa kwa siasa za chama kimoja. Ubeti wa kwanza unasema hivi:

Hitaraji tuungane, undugu ututawale
Hataka tushikamane, kama pete na kidole
Kumbe bwana nidengene, wakuu wetu wawale!
Msitu ni ule ule, na fisi ni wale wale!

Kupitia maneno haya ya mshairi tunaona kuwa wananchi walitarajia kuwa kungekuwepo na ushirikiano baina yao na viongozi ili kuleta maendeleo. Kinachobainika ni kuwa wananchi walikuwa wamejidanganya. Wanasiasa walibaki wale wale, hawakuwa na tofauti yoyote na madikteta wa siasa za chama kimoja. Sawa na madikteta waliotangulia, kizazi kipya cha wanasiasa hakikushirikiana na umma wala kutilia maanani mahitaji yake.

Katika sehemu iliyopita, tuliona wanasiasa wa kipindi cha siasa za chama kimoja wakilinganishwa na majitu manene mazito na mafunza kutokana na ulafi wao. Katika sehemu hii, mshairi anabainisha jinsi wananchi walivyokatizwa tamaa na kizazi kipya cha wanasiasa anapokariri kuwa ‘msitu ni ule ule, na fisi ni wale wale!’ Hii inamaanisha kuwa mabadiliko ya mfumo wa kisiasa si hakikisho la uongozi bora. Madhumuni ya tatu ya utafiti huu yalikuwa kutathmini mabadiliko ya mwanasiasa wa Afrika baada ya uhuru kwa mujibu wa ushairi wa Kiswahili.

Katika beti zinazofuatia, mshairi anakashifu utovu wa nidhamu, ushindani na unafiki wa wanasiasa wa kipindi cha siasa za vyama vingi. Mshairi anasema hivi:

Vigogo waumbuane, matayo pasi sumile
Na mara watukanane, wapigizane kelele
Eti kisa twondokane, na ya uhasama ndwele!
Bado mwitu ule ule, na fisi ni wale wale!

Kinachodhihirika hapa ni ukosefu wa uadilifu kwa upande wa wanasiasa. Wananchi wanapowashuhudia viongozi wao wakitukanana na kupigiana kelele hadharani hudhani kuwa wamekosana kabisa. Tabia kama hii haitarajiwi kutoka kwa waheshimiwa. Aidha, kwa kiasi kikubwa inachangia katika kuthibitisha kuwepo kwa ushindani wa mara kwa mara miongoni mwa wanasiasa (Mulokozi, 1992).

Licha ya kuzozana hadharani, wanasiasa hawawi maadui wa kudumu. Mshairi anaonyesha jinsi mahasimu hawa husuluhisha tofauti zao na kurejelea maisha yao ya kawaida. Mshairi anaendelea kufafanua:

Sikuye wapapurane, maguvu waamilile
Muda wasisemezane, ja mahasimu wa kale
Wakae wasikizane, warejee pale pale,
Kwani mwitu ule ule, na fisi ni wale wale!

Uwadhani watengane, wadumu hivyo milele
Ghafula waungamane, ubaki kuliya ole!
Maadui wapatane, watakapokaa wale,
Kwani mwitu ule ule, na fisi ni wale wale!

Ufafanuzi huu unadhihirisha kuwa wanasiasa hawajali kuaibika, bora tu watimize matakwa yao. Tunaona kuwa wanapozozana hadharani na kukosa kuzungumziana kwa muda wananchi hushangaa pale wanapopatana tena na kula pamoja. Mizozo hii wakati mwingine huwafanya wafuasi wao kutengana na kuishia kupigana, kuharibiana mali na hata kuuana. Aidha, unafiki huu wa wanasiasa huwafanya wananchi kuzozana na wakati mwingine kuangamizana kwa misingi ya kikabila. Uhasama wa aina hii uliwahi kuzuka nchini Uganda baada ya uhuru na kusababisha hasara kuu (Bigombe, 1993 na Mworio, 2009).

Kutokana na maoni ya mshairi katika utungo huu, inabainika kuwa juhudi kubwa zilizofanywa na wananchi za kuung'oa utawala dhalimu wa chama kimoja hazikuzaa matunda yoyote. Wanasiasa bado ni wale wale – wanaojijali tu nafsi zao huku wakiwatumia wananchi kujinufaisha.

5.4.2 Waharibifu

Utafiti huu ulidhihirisha jinsi wanasiasa wa Afrika wa kipindi cha baada ya uhuru waihusika katika vitendo vya uharibifu bungeni, kiasi cha kuvunja mioyo ya wananchi waliowachagua. Katika shairi liitwalo 'Msimu wa Tisa' (kur. 9-11), Mberia (2007) analalamika kuhusu tabia za wanasiasa ndani ya bunge na kushangaa iwapo maslahi ya wananchi yanashughulikiwa vilivyo. Mshairi anaanza utungo wake kwa kutoa taswira ya ukumbi wa bunge:

Leo ukumbi wa ukumbi umejaa vumbi jeuri
Kimbunga cha ubinafsi, uzembe na kiburi
Kinavuma kama bahari inayoteta na tufani

Katika ubeti huu inadhihirika kuwa bunge la kipindi cha siasa za vyama vingi lilijaa michafuko, huku wanasiasa wakitawaliwa na ubinafsi, uvivu na majivuno. Wanasiasa hawa wanaonekana kushughulishwa na maslahi yao pekee.

Uharibifu wa wanasiasa unathibitishwa katika kifungu kifuatacho ambapo mshairi anawalinganisha na nzige wa jangwa. Mshairi anasema hivi:

Ni nani atakayeimba wimbo wa uzalendo
Katika huu ukumbi wa msimu laanifu wa tisa
Ambamo nyoyo za waliotumwa kujenga taifa
Zinadunda kwa mpigo wa ubinafsi uliokithiri-
Ukumbi ambamo wingu la nzige wa jangwa
Linakula karamu haramu kwenye mti wa jamhuri

Mshairi anashangaa hapa ni nani atakayewatetea wananchi iwapo wanasiasa wanapoenda bungeni hujijali tu nafsi zao. Si ajabu kuwa anawalinganisha wanasiasa hawa na wingu la nzige wa jangwa wanaokula kila kitu katika mti wa jamhuri. Nzige wanaorejelewa hapa ni wadudu hatari ambao husababisha njaa na uharibifu mkubwa wa mazingira wanapovamia nchi na kushambulia kila mmea. Hii ni ithibati kwamba wanasiasa wa kipindi za siasa za vyama vingi hawakuwa na tofauti yoyote na wale wa kipindi cha chama kimoja kwani wao pia walikuwa walafi wakuu. Hawakuwajali kamwe wananchi waliowapeleka bungeni bali walijadili na kupitisha sheria zilizowafaidi wao binafsi.

Mshairi pia anatubainishia tofauti kuu iliyopo kati ya wabunge wenye shibe na wananchi wanaoumia kwa njaa. Anasimulia jinsi wabunge hawa walafi walizurura vijijini baada ya kushiba kutokana na jasho la wananchi. Mshairi anasema hivi:

Zilifuata ziara za kubenua vifua na kuteuka vijijini
Walijinadi kwa akina yahe waliovaa matambara
Walitifua vumbi kwa mabenzi na mapajero mapya
Na kuduwaza watu kwa ujanja wa mlo wa siku moja
Kabla ya kuhama kama mbayuwayu wakati wa kiangazi

Katika kifungu hiki inabainika kuwa wanasiasa hawawatembelei wananchi hawa maskini kwa lengo la kuwasaidia. Lengo lao kuu ni kujijenga kisiasa huku wakiwapumbaza wananchi kwa chakula cha siku moja. Baada ya wananchi kujionea

magari ya kifahari wanasiasa hao hutoweka vijijini na kurejea wakati wa uchaguzi mwingine.

Wanaporejea bungeni baada ya ziara za vijijini, wanasiasa hujiunga pamoja tena kama nzige wa jangwa. Lengo lao huwa kufidia fedha walizotumia katika ziara hizo. Hawajali kamwe sauti za wananchi wanaopinga marupurupu wanayojiwekea, kama inavyobainishwa na mshairi:

Baada ya kupingwa kutunyang'anya mwishoni mwa msimu
Wameshika rungu nzito na kupiga dafirau bajeti ya taifa,
Kwa ubinafsi usiojali walio kwenye minyororo ya ukame
Wamejitwalia marupurupu laanifu eti ya kulipia usafiri
Kama kwamba dawamu wanasafiri hadi kwenye ukingo wa bara

Inabainika hapa kuwa hata baada ya wanasiasa kushambulia mali ya umma kama nzige wa jangwa na kusababisha njaa kali kwa wananchi, ulafi wao haujafika kikomo. Wanakataa kupitisha bajeti ya taifa hadi walipwe marupurupu wanayodai, bila kujali umuhimu wa bajeti hiyo kwa taifa kwa jumla.

5.4.3 Wazembe

Kutokana na uzembe wao kazini, wabunge wa kipindi cha siasa za vyama vingi wamelinganishwa na konokono. Hiki ni kinyama chenye marendarenda yanayokifanya kuteleza na kinachotambaa polepole sana. Mtu anayelinganishwa na konokono huwa mvivu kupindukia, kiasi cha kuwaudhi wenzake.

Kinachowafanya wabunge kulinganishwa na kinyama hiki ni kuwa, hata baada ya kujitwalia marupurupu kwa ulafi wa nzige, baadhi yao hawawajibiki bungeni. Katika kifungu cha saba kwenye shairi liitwalo 'Msimu wa tisa (kur. 9-11) ambalo tumeangalia hapo juu mshairi analalamika:

Jukumu waliloomba kwa kupiga magoti na kutoa ahadi
Tukawapa tukidhani watatusafirisha kutoka bonde la huzuni
Wanalitimiza kwa kujikokota kama konokono au yungiyungi
Wamegeuza ukumbi wa taifa nembo ya uzembe na aibu

Inaonekana wazi kuwa wananchi waliokuwa na matumaini makubwa hapo awali wamejawa na huzuni. Utendakazi wa wabunge wao unakuwa duni na wa kulidunisha

bunge. Unyenyekevu walioigiza walipokuwa wakifanya kampeni unathibitishwa kuwa wa bandia.

Uzembe wa wabunge unabainika zaidi katika kifungu kinachofuatia ambapo baadhi ya vikao vya bunge vinavunjwa kwa kukosa idadi murua ya wabunge. Hata wachache wanaohudhuria hawashiriki kikamilifu kwani baadhi yao husinzia bungeni. Kuhusu tabia hii mshairi anasema:

Vikao vya majadiliano vinavunjwa kwa kukosa idadi murwa
Wanaoitwa kwa jina lenye marashi na kulipwa kwa dhahabu
Hawaji ukumbini wakafika thelathini kutimiza kanuni
Wakija huja wamevaa machovu kama magwada ya chuma
Mambo huwapita usingizini wakidondokwa na udenda

Kutokana na kifungu hiki, ni dhahiri kuwa wanasiasa wa kipindi cha siasa za vyama vingi hawajali wanapokiuka kanuni za kazi waliyowaomba wananchi. Ndiposa wengi wao hukosa vikao vya bunge huku wakijua wazi kuwa kuna idadi maalum inayohitajika ili vikao hivyo viendeleo. Isitoshe, kulala kwao bungeni ni ithibati tosha kuwa hawachelei hata kuonekana na waliowachagua, hasa wakati huu ambapo vikao vya bunge huonyeshwa moja kwa moja kwenye runinga.

Kutowajibika bungeni kunadhihirika zaidi kutokana na utendakazi duni wa kamati za bunge. Hata uteuzi wa kamati hizi ni wa kutiliwa shaka. Mshairi anawaumbua wanakamati hao hivi:

Viongozi wa kamati za kupiga miswada darubini
Wanayumba hawana nguvu za kubeba jukumu adhimu
Hawakupata nyadhifa baada ya kupimwa kwenye ratili
Uchaguzi ulikuwa kazi shaghala-baghala ya waliosinzia

Inabainika katika kifungu hiki kuwa wanakamati hawa hawana ujuzi unaohitajika ili kutimiza wajibu wao kwa ustadi. Aidha, waliteuliwa bila uangalifu kutokana na uzembe wa wabunge waliosinzia kazini.

Ithibati nyingine ya uzembe wa wabunge inayojitokeza katika shairi hili inatokana na jinsi maswali yanavyoulizwa na kujibiwa bungeni. Mshairi anaeleza hali hiyo:

Muda wa swali adimu kwenye ratiba uwadiapo
Muulizaji hayupo kwenye idadi ya wachache ukumbini
Ameketi hoteli akipumbaza vizuu wake kwa vinywaji
Akipanga njama za kunyakua taji la mkuu wa kabila

Mshairi anaeleza kuwa wakati mwingine muda wa kuuliza maswali unapofika mbunge aliyefaa kuuliza swali hapatikani bungeni. Badala ya kuwa bungeni akiwatetea wananchi, mbunge huyu huwa anastarehe hotelini pamoja na wafuasi wake akipanga njama ya kuwa kiongozi wa kabila lake. Hali hii huathiri maendeleo ya taifa kwani miradi muhimu hukosa kujadiliwa na kupitishwa bungeni. Umma huendelea kuumizwa na umaskini na ukosefu wa huduma muhimu ambazo wangepata iwapo wawakilishi wao bungeni wangewajibika.

Sio wanaouliza maswali tu wanaopatikana na dosari. Mawaziri pamoja na manaibu wao pia hawapatikani bungeni kujibu maswali yanapoulizwa. Mshairi anawakashifu hivi:

Swali la pili limeulizwa limechangamsha akili kwa ubora
Bali kiu cha kusikiza jawabu hakitakatika hadi juma lijalo
Waziri hayumo anacheza gofu na majambazi wa kigeni
Badala ya naibu wake kuwapo kujaza pengo la wizara
Yumo kitandani amelemazwa na manofu ya nyama ya jana

Tunaona hapa kuwa wakati mwingine maswali yenye manufaa huulizwa bungeni lakini majibu yake yakacheleweshwa kutokana na kutowajibika kwa mawaziri na manaibu wao. Badala ya kuhudhuria vikao na kujibu maswali yanayoulizwa kuhusiana na wizara zao, baadhi ya mawaziri huenda kucheza gofu na majambazi wa kigeni. Kwa upande mwingine, manaibu wao huwa wamelala kutokana na shibe ya siku iliyotangulia. Hii ni hali ya kusikitisha mno ikizingatiwa kuwa, mbali na kutowajibika, baadhi ya wanasiasa wa kipindi cha siasa za vyama vingi walitumia afisi zao zilizomo katika majengo ya bunge kufanyia vitendo vya uzinzi (Hamisi, 2011).

5.4.4 Waendelezaji wa Tabaka

Suala la utabaka na juhudi za wanasiasa za kuuendeleza limekaririwa mno katika utafiti huu. Wanasiasa hawa, ambao walihodhi na bado wanaendelea kuhodhi nyenzo za kuzalishia mali, walijiweka katika tabaka la juu huku wananchi wengine wakisalia katika tabaka la chini. Ni katika muktadha huu ambapo Wamitila (2007) kupitia shairi

liitwalo ‘Tazama’ (uk. 25) anawasawiri wanasiasa wa kipindi cha siasa za vyama vingi kama waendelezaji wa tabaka.

Katika shairi hili, mshairi anawataka wananchi kufumbuka macho na kujionea jinsi tabaka zilivyoenea. Aidha, mshairi anazungumzia athari za utabaka zinazoendelea kuisakama jamii hata baada ya kuondoa udikteta wa chama kimoja. Mshairi anauhamasisha umma kwa kulinganisha mazingira mawili; yale ya kimaskini na yale ya kitajiri kwa kusema hivi:

Tazama utaona,
Maskini wanaoishi katika dhiki za karne
Fukara wanaodidimia katika kinamasi cha dhuluma
Fakiri wanaogugunwa mili na michonge wa tabaka
Wakiwa wanaokufa njaa kwa kukosa cha kujilia
Maskini wanaoteswa kwa kuililia auni
Umma unaolia kwa kuikosa nafuu,
Kwa kupakosa pa kulala
Kwa kukikosa cha kuvaa
Kwa kuyakosa matibabu
Kwa kuyakosa maisha

Kifungu hiki kinatoa ushahidi kuwa maisha ya mwananchi wa kawaida hayakuimarishwa na mabadiliko ya kisiasa yaliyotokea katika bara la Afrika palipoanzishwa mfumo wa siasa za vyama vingi. Umaskini ulikithiri na wananchi waliendelea kukumbwa na dhiki ya kukosa chakula, matibabu, malazi bora na mavazi.

Kwa upande mwingine, maisha ya wanasiasa yaliendelea kuimarika huku wakiishi maisha ya anasa kama ilivyonakidiwa katika kifungu hiki:

Tazama kisha utaona,
Vitambi vinavyotetemeshwa na uto wa nyama
Shingo zinazoshabihiana na mibuyu ya pwani
Mili iliyonenepeana tamthili ya kiboko
Vinywa vinavyokula na kusaza kwa wingi
Macho yasiyopenda kuuona uhalisi

Taswira tunayoona katika kifungu hiki ni kinyume kamili na ile tuliyoshuhudia katika kifungu kilichotangulia. Mwananchi wa kawaida anapoendelea kukonda na kuumizwa na dhiki ya kukosa kutimiziwa mahitaji muhimu wanasiasa wanaimarika kiafya.

Tunawaona wanasiasa hawa wakiwa na dalili zote za shibe – miili minene iliyo na vitambi vikubwa, shingo nene pamoja na vinywa vinavyokula na kubakisha. Isitoshe, macho yao yanapuuza hali halisi iliyowazunguka – ile ya umma uliojawa na dhiki.

Kinaya kinachojitokeza kuhusiana na tabia za wanasiasa hawa ni kuwa hawaishi kujisifu na pia kusifia maendeleo na sera za nchi zao. Mshairi anaeleza haya katika kifungu hiki:

Tazama tena, kisha utaona
Wanasiasa wanaojisifu kwa maendeleo
Mawaziri wanaorereja sifa za sera za nchi zao
Wanadini wanaoimba kwa kupagawa
Na kiongozi anayejisifia kipaji cha kuona mbele

Kifungu hiki kinaashiria kuwa wakati mwingine umma hushindwa kuwaamini wanasiasa kwani mara nyingine wanachosema sicho wanachoamini na wanachoamini sicho wanachosema. Wanasiasa mara nyingi hujisifu kwa maendeleo na maono yasiyokuwepo. Isitoshe, wanasiasa hao hukosa kusema chochote kuhusiana na dhiki inayowakumba wananchi wanaowaongoza.

Kauli hii inaweza pia kushadidiwa na maoni ya Arege (2007) katika shairi lake liitwalo ‘Tabasamu zao’ (uk. 33). Mshairi anasema kuwa wanasiasa wanapotabasamu yeye hukosa kuziamini tabasamu hizo zilizojaa unafiki, kama anavyokariri katika vifungu hivi:

Wote hawa sioni yao tofauti.
Wote hawa, sawa
Na mwanasiasa mwehu
Ni mtoto wa jicho.
Wanapotabasamu nachelea kuridhia.
Hutabasamu wadhamiriapo mengine.

Tabasamu zao ni ishara ya maangamizi
Wanipangiayo kimoyomoyo, kimyakimya
Wafurahie kutakarika kwangu
Kwenye tanuri hii ya maisha.

Kile mshairi anachosisitiza hapa ni kuwa wananchi wanafaa kuwa macho wanapotangamana na wanasiasa. Hii ni kwa sababu wanasiasa wana sifa mbaya ya kutotabirika; hivyo kutoaminika.

Kutotabirika na kutoaminika huku pia kumedokezwa na Mogambi (2007) katika shairi liitwalo ‘Ndoto mbaya’ (uk. 101) anaposimulia kuhusu jinamizi la uchoyo wa ukuu na unyanyasaji wa wanasiasa. Anasimulia jinsi katika jinamizi hili aliona mazimwi waliokula watu wengi na bado wakiendelea kulalamikia njaa. Mazimwi hawa pia waliwameza waathiriwa wakiwa hai, tena wazimawazima, kama inavyosimuliwa katika kifungu hiki:

Jana niliota
Ndoto mbaya ya hakika
Ndoto ya uchoyo
Uchoyo wa ukuu
Ukuu wa kuwanyanyasa wengi
Ndoto mbaya ya jinamizi
Wanaowala watu wengi wakicheka
Wanaokula wakilalama njaa
Wanawameza wakiwa hai wazimawazima!

Kifungu hiki kinaonyesha kuwa ni vigumu kuwaelewa wanasiasa wa kipindi cha siasa za vyama vingi. Hii inatokana na tabia yao ya ajabu ya kuwaangamiza wananchi huku wakicheka. Aidha, wanasiasa hawa wana tamaa ambayo ni vigumu kuridhishwa. Mshairi anasema kuwa hata wanapokula mali ya umma na kutishia kuwaangamiza wananchi kabisa bado wanataka kula zaidi. Hii ni ithibati kuwa wanasiasa waliorejelewa wamejaa unafiki, kiburi, uongo, uchoyo na ubinafsi (Makillah, 2009).

5.4.5 Wapenda Vyeo na Pesa

Sifa nyingine iliyodhihirishwa na washairi kuhusiana na wanasiasa wa wakati huu ni tamaa ya vyeo, pesa na mali kwa jumla. Muchai bin Chui (2007) kupitia shairi liitwalo ‘Tujenge nti wanati’ (uk. 30) anauhamasisha umma kuhusiana na ulafi wa wanasiasa kwa maneno haya:

Tusikubali wateti, ambao nia ni viti,
Bungeni kwenda manoti, na kunyakua ploti,
Na huku nyuma mauti, kutukamua matiti,
Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati.

Kura iwe ndio cheti, ukabila ni mauti,
Sio kupenda manoti, kuhongwa kati kwa kati,
Ngao iwe ni tikiti, kadi zetu tuzatiti,
Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati

Beti hizi zinaonyesha kuwa baadhi ya wanasiasa wa kipindi cha siasa za vyama huingia uongozini kwa nia ya kujitajirisha wala sio kuwatumikia wananchi. Mshairi anasema hapa kuwa sharti umma uwakatae wanasiasa wanaoingia bungeni kwa nia ya kujipatia mishahara mikubwa na pia kujinyakulia ploti. Tamaa hii ya wanasiasa inaweza kuthibitishwa na tabia ya wanasiasa wa Kenya. Baada ya uchaguzi uliofanyika nchini mnamo Machi 2013, kundi moja la wanasiasa waliochaguliwa lilitisha kuwaondoa wanachama wa Tume ya Mishahara ya Watumishi wa Umma punde tu waingiapo bungeni. Wanasiasa hawa walikuwa wakilalamika, hata kabla hawajaapishwa na kuwa wabunge rasmi, kuhusiana na upunguzwaji wa mishahara ya wabunge uliofanywa na tume hiyo (*Daily Nation* Machi 28, 2013, uk. 72).

Tabia hii ya wanasiasa ya kupenda pesa ina historia ndefu. Wamitila (2007) katika shairi liitwalo 'Chini ya mgunga' (uk. 105) anasimulia jinsi alipokuwa katika shule ya msingi walisomea chini ya mgunga kwa kukosa madarasa. Pesa za kujengea madarasa zilikuwa zimefujwa na wabunge. Mshairi anasimulia:

Nakumbuka kuwa shule haikuwa na pesa
za kujenga madarasa mengine
serikali nayo ilishatobokwa na mifuko
mapeni yakaanguka njiani
kwenye safari ya uhuru
na kuokotwa na mikono
ya mtembezi mwepesi
aliyeelekea bungeni ilikokuwa yake ofisi!

Mgunga ulikuwa kivuli jua kali kutusitiri
Mgunga ulikuwa msitu wa viboko vya mwalimu
Lakini ulikuwa pia ubao wa wanasiasa wa kuwekea
makaratasi manene ambayo hayakuisha
ya baraza la mawaziri.

Kinachojitokeza wazi katika vifungu hivi ni kuwa wanasiasa daima wameweka maslahi yao mbele. Licha ya kufuja pesa za elimu pia waliathiri elimu ya watoto kwa kuweka mabango yao ya siasa pale watoto waliposomea. Aidha, watoto walihitajika kukariri majina ya wanasiasa hawa, jambo ambalo halikuwavutia, kama anavyokiri mshairi:

Huikumbuka vizuri siku moja mwalimu alipoliacha
karatasi moja ubaoni, tulipaswa kuyakariri majina
mengine...

Alipoondoka
Tulichochewa na maembe ya jirani
yaliyoiva na kutualika
Tuliondoka... nyatu nyatu
maneno ya mwalimu
yakitufuata... *Viongozi hawa wanatulinda
na wanaangalia kila kitu nchi hii*
Tulinyatia shamba
La maembe nyatu nyatu
Na kuanza kuyakwepua
Viongozi wakituangalia!

Kitendo hiki cha wanafunzi kuyapuuza maneno ya mwalimu kuhusiana na viongozi wa kisiasa kinaashiria kuwa hata watoto wenyewe hawakuthamini elimu iliyoingizwa siasa. Kinaya kikuu hapa ni kuwa mwalimu anapodai vile viongozi hao waliwalinda na kuangalia kila kitu nchini, viongozi wenyewe hawakuwaona watoto hawa waliponyatia kwenye shamba la jirani na kumwibia maembe! Hii ni ishara ya upofu wa wanasiasa ambao hudai kuilinda nchi ilhali wanajitunza nafsi zao tu.

Upofu huu pia umezungumziwa katika diwani ya *Msimu wa Tisa* ambapo mtunzi analalamika kuhusu dhiki ya njaa inayowakumba maskini wa Afrika. Shairi lake liitwalo 'Minyororo ya njaa' (uk. 1) linatoa taswira ya wananchi wanaokumbwa na njaa kali ilhali viongozi wao hawachukui hatua yoyote ya kuwasaidia. Badala yake, baadhi ya viongozi wanalaumu hali ya anga kwa masaibu yanayowakumba wananchi. Mshairi anawalaumu wanasiasa kwa maneno haya:

Jijini, wimbo ni uleule wa kughasi hisia
Wanasiasa wanalaumu anga kwa janga
Hawaoni kwamba njaa isiyohama nchi
Ni tunda chungu la siasa za pesa-nane
Siasa bila ramani, bila dira, bila kurunzi

Asemaye kwamba ukame ni kudura ya Mungu
Anenaye njaa ni kazi ya uovu wa anga bahili
Ahurumiwe, amezima ubongo wa bongo!

Inaonekana hapa kuwa baada ya kuulaumu udikteta wa chama kimoja kwa miaka mingi kwa karibu kila janga lililokumba bara la Afrika, umma wa eneo hili bado

haujapata afueni. Wanasiasa waliochukua madaraka baadaye wanaendeleza siasa duni huku wakijifanya kutokuwa na suluhu kwa matatizo yanayokumba umma. Badala yake viongozi hawa wanatafuta visingizio, ikiwa ni pamoja na kumlaumu Mungu, kwa kusababisha ukame.

Uongozi huu uliojaa upofu na kutowajibika pia umejadiliwa katika shairi liitwalo ‘Usingizini’ (uk. 3). Katika shairi hili, sawa na lile tuliloangazia hapo juu, wanasiasa wa Afrika wa kipindi cha siasa za vyama vingi wamesawiriwa kama viongozi waliolala na wasio na mipango madhubuti ya kuendeleza eneo hili. Kuhusu kutowajibika huku mshairi anauliza swali hili:

Ni nani anayejua siku adhimu au mwezi azizi
Ambamo wanaokoroma kwenye makochi ya uongozi
Wataamka kutoka usingizi wa siasa bila ramani
Wafikiche macho kwa viganja vya uona-mbali
Waongoze taifa kutoka hili bonde la aibu?

Jambo linalomkera mshairi hapa ni uzembe wa viongozi wa kisiasa. Viongozi hawa hawachukui hatua yoyote ya kuyaondoa mataifa yao katika aibu inayoyakumba raia wake wanapoangamizwa na njaa. Ardhi yenye rutuba haitumiki kikamilifu; hakuna miradi ya kuyazuia maji ya mvua kuteremka hadi mitoni, maziwani na hatimaye baharini. Uharibifu huu unatokea huku viongozi wakilala na kutochukua hatua yoyote ya kuukomesha.

5.4.6 Wanyakuzi wa Ardhi

Mizozo kuhusiana na ardhi pamoja na unyakuzi wake ni masuala sugu ambayo yalijitokeza wazi katika utafiti huu. Iithibitishwa kuwa wanasiasa wengi wa Afrika katika vipindi mbalimbali vya kisiasa walijiingiza katika uovu huu, kama ilivyonakidiwa na watafiti mbalimbali (GoK, 2008, Southall, 2008 na Mworio, 2009).

Mberia (2007) anashadidia maoni ya watafiti hawa kwa kuwasawiri wanasiasa wa kipindi cha siasa za vyama vingi kama wanyakuzi wa ardhi. Katika shairi lake liitwalo ‘Usingizini’ (uk. 3) ambalo tumepitia hapo juu, mshairi anawalaumu wanasiasa kwa unyakuzi wa ardhi ambao unasababisha njaa. Lawama hizi zinatolewa kwa maneno haya:

Wanaonyongwa nyoyo na mafuta ya utajiri
Wamebana mikononi maelfu ya ekari za rutuba
Huku wajukuu wa waliopokonywa urithi kwa mijeledi
Wakiwa hawana vikata vya kukuza vihimili vya maisha!

Katika ubeti huu mshairi anaonyesha athari za unyakuzi wa ardhi kwa umma. Analalamika kuwa wanasiasa wanaendelea kunenepa kwa kuyatumia maelfu ya ekari ya ardhi yenye rutuba waliyonyakua. Kwa upande mwingine, wajukuu wa waliopokonywa ardhi hii wanakufa njaa kwa kukosa pa kulima. Aidha, ardhi iliyotengewa taasisi muhimu kama vile hospitali na shule hunyakuliwa na wanasiasa huku wananchi wakikosa huduma muhimu. Unyakuzi wa msitu wa Mau nchini Kenya ni ithibati tosha ya hasara zinazotokana na unyakuzi wa ardhi ya umma. Eneo linalouzunguka msitu huo lilikosa mvua ya kutosha kutokana na tamaa ya wanasiasa. Hali hii ilisababisha upungufu mkubwa wa maji na chakula kwa wenyeji pamoja na mifugo yao (Miguna, 2012).

5.4.7 Wachochezi na Waenezaji Chuki

Uhalifu kama vile uchochezi na uenezaji wa chuki ni baadhi ya maovu yanayoshuhudiwa katika bara la Afrika na ulimwenguni kwa jumla. Kwa kawaida, wananchi huwategemea viongozi wao kuwalinda na pia kuhakikisha kuwa wametendewa haki wanapodhulumiwa na wahalifu. Imani ya wananchi kwa viongozi wao hupotea iwapo viongozi watageuka na kuwa wavunjaji wa sheria.

Mberia (2007) katika shairi lake litwalo ‘Waharifu Huru’ (uk. 30) anasimulia jinsi wananchi wasio na hatia huumizwa na uchochezi wa wanasiasa. Anaeleza jinsi wanasiasa huwalipa vijana fukara ili kuwatumia kusababisha ghasia. Vijana hawa huwahangaisha watu wanaodaiwa kuwa wageni katika maeneo husika huku wakiwapiga, kuwafukuza na kuchoma mali yao. Mshairi anasimulia:

Bila kutarajiwa, onyo za mashambulizi dhidi ya “wageni”
Zilipaa na kuchafua anga kama harufu ya amonia
Vilifuata vijinga vikipulizwa na pumzi hatari za wanasiasa,
Taya za miako zilitafuna mbao, fenicha, nguo na vyeti
Maghala ya chakula na matumaini ya kesho yenye shibe
Yalifutiliwa mbali na upepo wa wendawazimu wa kupangwa;
Kutoka mikononi mwa fukara walioleweshwa kwa chuki
Mishale ilipiga mbizi katika miili ya wakazi wa makabila mengine
Panga za ghadhabu zilishuka baina ya vichwa na viwiliwili
Vituo vya biashara vilivyonawirishwa kwa maisha na heshima
Vilichimwa na kubakia magofu yenye mwanngwi wa huzuni;
Mashamba yaliyohimili familia na mimea tele na mifugo
Yalivamiwa na kwekwe jeuri na kuminywa afya ya jana
Wajane na mayatima walibaki katika dukuduku la kukata tamaa;
Chemchemi za karo ya watoto zilikauka na kubakia makuo tasa

Kifungu hiki kinaonyesha hasara ambayo husababishwa na uchochezi wa wanasiasa. Baada ya watu kufukuzwa makwao, baadhi yao kuuawa na mali yao kuteketezwa, wajane na mayatima hubaki wakihangaika bila makao, chakula na karo.

Katika kifungu kifuatacho tunaona baadhi ya vijana walioachwa taabani wakipoteza matumaini maishani na kujiingiza katika uhalifu. Mshairi anasema hivi kuwahusu:

Vijana wa kike walifuata njia ya mchanga didimizi wa ukahaba
Wa kiume walikwama kwenye bonde la madawa ya kulevya
Na kisha kutumbukia katika dimbwi la wizi na unyang’anyi;
Bali katika wingu la unafiki wa “amani, upendo na umoja”
Badala ya wahandisi wa wa jakamoyo kutetemeka mahakamani
Badala ya wenye damu viganjani kutupwa korokoroni
Wanaendesha mashagingi yenye bendera za mamlaka
Wanalipwa mishahara minono wakiitwa “viongozi wa taifa”

Jambo la kusikitisha zaidi linalodhihirika katika kifungu hiki ni sura mbili za dunia; ile wanayoishi wanasiasa na ile wanayoishi wahasiriwa. Vijana wanapoendelea kudidimia katika ukahaba, dawa za kulevya, wizi na unyang’anyi, wanasiasa waliowaharibia maisha wanaendelea na maisha yao ya kifahari. Wanaendesha magari makubwa, kulipwa mishahara minono na kuheshimiwa kama viongozi wa taifa. Hakuna hata mmoja wao anayeshtakiwa na kufungwa kwa uhalifu huu.

Ingawa mshairi amewalaumu wanasiasa kwa kusababisha ghasia huku wakiwatumia vijana maskini, umma pia unapaswa kulaumiwa kwa kukubali kutumiwa kutenda

uhalifu. Vikundi vya kidini na mashirika mengineyo yanafaa kuwaelimisha vijana kuhusiana na umuhimu wa kuzingatia sheria za nchi zao. Ni muhimu pia vijana hawa watafutiwe njia bora za kujitafutia riziki ili wasinaswe kwa urahisi na wanasiasa wanaowatumia kutekeleza uhalifu.

5.4.8 Wauaji na Wabakaji

Mbali na kuwachochea wananchi, wanasiasa pia wamesawiriwa katika ushairi wa Kiswahili kama wauaji na wabakaji. Mberia (2007) katika shairi lake liitwalo ‘Kasisi’ (uk. 82) anasimulia jinsi kasisi mmoja alivyoangamizwa na wanasiasa baada ya kushuhudia uchochezi, ubakaji na mauaji waliyotekeleza katika Bonde la Ufa. Mshairi anatoa kumbukumbu ifuatayo:

Ulishuhudia mito ya damu
Ikitirika katika Bonde la Ufa,
Uliona mvua ya machozi
Ikilowesha kambi za wakimbizi,
Ulitazama ndoto za makabwela
Zikiunguzwa na kubakia jivu,
Ulikuwa na bakuri lililojaa habari
Kuhusu manahodha wa njama,
Ulielezwa kisa cha mwanasiasa
Aliyembaka binamu yake ofisini
Ulijua dhiki ya wasichana wachanga
Waliozimwa heshima ya uanamwari

Katika kifungu hiki mshairi anatoa ushahidi na matokeo zaidi ya uchochezi ambao tumejadili hapo juu. Anashuhudia jinsi wanasiasa walivyochochea vita katika Bonde la Ufa nchini Kenya na kusababisha madhara makubwa. Wananchi wengi waliishilia katika kambi za wakimbizi wa ndani baada ya mali yao kuteketezwa na mahasimu wao. Wengine waliuawa katika vita hivyo vilivyothaminiwa na wanasiasa kama inavyoweza kuthibitishwa na vurugu iliyoshuhudiwa nchini Kenya baada ya uchaguzi wa mwaka 2007 (Southall, 2008).

Mshairi pia anagusia kisa cha mwanasiasa aliyembaka binamu yake afisini pamoja na vile vya wasichana wengine wachanga waliowahi kubakwa. Kutokana na visa hivi, wanasiasa wanasawiriwa kama watu waliopotoka kimaadili kiasi cha kutoaminiwa hata na jamaa zao. Kumekuwa na visa ambapo baadhi ya wanasiasa barani Afrika wameshtakiwa kwa madai ya kuhusika katika uchochezi, uhamishaji wa halaiki,

mauaji na ubakaji, sio tu katika mahakama za nchini zao, bali katika Mahakama ya Kimataifa.

5.4.9 Wasaliti na Wajanja

Kuna ithibati zaidi kuwa mwanasiasa wa Afrika hajabadilika hata baada ya kuondoa udikteta wa chama kimoja. Mberia (2007) anafichua jinsi migogoro ya kisiasa ilivyozuka nchini Kenya baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2002. Katika shairi liitwalo ‘Tope la mizozo’ (uk. 6), mshairi huyu anasimulia jinsi matumaini ya Wakenya yalivyodidimizwa na usaliti wa wanasiasa walioingia mamlakani. Wakenya walitamaushwa hasa na uvunjaji wa mikataba ya kisiasa iliyoafikiwa kabla ya uchaguzi. Katika ubeti wa pili mshairi analalamika hivi:

Kabla ya mwangwi wa shangwe zetu kuyeyuka
Tulioshangilia katika bustani pendezi ya matumaini
Walianza kugongana kama vyuma katika kapu
Likivurutwa na watoto katika mchezo usiokoma

Tunaona hapa kuwa viongozi walioingia mamlakani hawakujali maslahi ya wananchi bali walianza kuzozana kati yao. Kwa kuwalinganisha wanasiasa na vyuma vinavyogongana kwenye kapu, mshairi anaashiria kuwa viongozi hawa walikuwa wamekosa mwelekeo kabisa. Isitoshe, kapu hili linavutwa na watoto katika mchezo usiokoma. Hii inamaanisha kuwa viongozi wa kisiasa walikosa uwajibikaji na walichukulia siasa kama mchezo tu.

Katika ubeti wa tatu, mshairi anaeleza kilichosabaisha ukiukaji wa mikataba ya kabla ya uchaguzi. Mshairi anakariri:

Katika ukungu wa werevu bila maarifa
Wenye tamaa kubwa ya kuwapiku wengine
Walitumia ujanja kwenye sinia ya mamlaka
Wakajitwalia minofu na kuwachia wenzao makano
Gundi ya mkataba uliounga pamoja makundi
Ikayeyushwa na moto wa hamaki ya haki

Mshairi anashikilia kuwa mikataba hii ilivunjwa na tamaa na ushindani wa kisiasa. Hili lilisababisha mgawanyiko kati ya makundi mawili ya wanasiasa, kundi moja likinufaika kutokana na uongozi na kulipuuza kundi jingine. Mshairi anaeleza katika

beti zinazofuatia kuwa kuvunjwa kwa mkataba huu kuliendeleza uufisadi. Hali hii ilizua malalamiko makubwa kutoka kwa kundi lililopunjwa katika mkataba.

Uvunjaji wa mikataba ya kisiasa pia unashadidiwa katika shairi litwalo ‘Werevu’ (uk. 8). Katika shairi hili, Mberia (2007) anaeleza jinsi mizozo ya kisiasa ilivyoandama taifa baada ya kiongozi aliyeingia mamlakani kuwasaliti wenzake walioshiriki katika upatikanaji wa demokrasia ya vyama vingi. Mshairi anaeleza usuli wa mizozo hii katika kifungu kifuatacho:

Angalipuuza mashauri ya wajanja waliomzunguka
Na kuthamini maana ya maneno ya wimbo wa taifa,
Angalizingatia kanuni za mkataba wa majemedari
Silaha iliyokomboa taifa kutoka minyororo ya huzuni,
Angalifahamu uaminifu ni akiba inayozaa matunda
Na kukubali usemi: “Werevu mwingi huondoa maarifa”,
Angaligawa mapato kwa ratili iliyopangwa awali
Na kwa kuheshimu kiu cha kambi yake na ya wenza,
Mti wa uelewano ungezidi kuzaa matunda matamu
Leo, kwa furaha, tungalikuwa tukiyala yakiwa mabivu

Kinachodhihirika katika kifungu hiki ni kuwa kiongozi anayerejelewa alipotoshwa na washauri wake wajanja waliomfanya kuwabagua wanasiasa wenzake waliochangia pakubwa katika kuwepo kwake mamlakani. Matokeo ya usaliti huu ni mapendeleo katika ugawaji wa rasilmali za kitaifa huku maeneo yenye wapinzani yakibaguliwa. Ubaguzi huu ulizua kutoaminiana ambapo uelewano, furaha na amani vilikosekana.

Katika kifungu kinachofuatia mshairi anaeleza jinsi wanasiasa waliobaguliwa walijipanga upya ili kukabiliana na waliokuwa mamlakani. Mshairi anasema hivi:

Si ajabu, walioliwa bangu na kuteswa na moto wa majuto
Walijiandaa na kusubiri kwenye medani ya mkataba mkuu
Punde viganja vilikazwa katika kamba ya “Vuta Tuvutane!”
Vidole vya miguu vikajikita katika udongo mzito wa kinamo
Werevu wakaangushwa na kubururwa kwenye tope la aibu

Ubeti huu unatoa ushahidi wa mivutano na mizozo isiyokoma katika mataifa ya Afika katika kipindi cha siasa za vyama vingi. Wanasiasa wa kipindi hiki wanasawiriwa kama wasaliti wanaojali tu maslahi yao na ya wafuasi wao wa karibu. Inaonekana wazi kuwa usaliti huu usipokoma mizozo na mivutano itakithiri.

Mbali na usaliti unaohusisha makundi mawili ya wanasiasa, ushairi wa Kiswahili unafichua aina nyingine ya usaliti. Usaliti huu unahusisha upangaji njama kati ya wanasiasa na wahuni wa kigeni kusababisha vurugu. Katika shairi litwalo ‘Tope la Mizozo’ (kur. 6-7) ambalo tuliangazia baadhi ya vifungu vyake hapo awali, mshairi anasimulia tukio lifuatalo:

Wakitumia genge la wahuni wenye dharau kwa wenyeji
Mamluki wenye lugha inayonuka kama samaki waliooza
Wale tuliopatia wadhifa wa kutulinda pamoja na mali zetu
Wamevamia haki zetu kwa kichaa cha usiku wa manane

Katika ubeti huu mshairi anawashutumu viongozi wa kisiasa kwa kutowalinda raia wa mataifa yao. Badala yake, viongozi hawa wanashirikiana na wavamizi kutoka mataifa ya nje ambao wanawavamia wananchi usiku. Usaliti wa aina hii unaweza kusababisha maafa makubwa kwa mataifa husika, hasa wakati huu ambapo mashambulizi ya kigaidi yanayohusishwa na kundi haramu la Al-Shabaab yametokelezwa katika baadhi ya mataifa ya Afrika.

Ubeti unaofuatia unasimulia jinsi wahuni hawa waliingia nchini kwa mwaliko wa wanasiasa. Mshairi anafichua njama hiyo:

Wahuni wa kigeni wamekaribishwa nchini kwa siri
Na kupewa vyeo vikuu na funguo za milango ya chuma
Wameishi starehe wakijinaki kwa maneno yenye uvumba
Wakitishia polisi kwa mbwa wakali katika kasri zao
Kijeuri, wakichomoa bastola dhidi ya wahudumu wa umma
Wafadhili wao wenye mashagingi yanayopeperusha bendera
Wakiwatetea kwa lugha thabiti dhidi ya raia wa taifa

Taswira inayojitokeza hapa inaonyesha jinsi wanasiasa walijali maslahi yao na kupuuzwa usalama wa taifa. Wanasiasa hawalaumiwi tu kwa kuwaingiza wahuni nchini kisiri. Wahuni hawa wanapewa vyeo vikubwa na starehe kuu. Vyeo hivi vinawafanya hata kuwatisha polisi kwa bastola pamoja na mbwa wakali waliowafuga katika kasri zao. Tunaona hapa kuwa badala ya wanasiasa kuutetea umma pamoja na polisi wanaotishwa wanawatetea wahuni. Tukio la aina hii lilishuhudiwa nchini Kenya wakati wa mavamizi ya mamluki kutoka Armenia waliotambulika kama *Artur Brothers*. Baada ya wahuni hawa kusababisha vurugu katika uwanja wa ndege wa Jomo Kenyatta na kuondoka nchini kwa hali ya kutatanisha, mbunge wa eneo moja

nchini Kenya, alinukuliwa baadaye akiwatetea huku akisema walikuwa marafiki wa binti yake (*SaturdayStandard*, Julai 6, 2013, uk. 1).

Jambo lililodhihirika katika utafiti huu ni kuwa huenda usaliti na ujanja wa wanasiasa ukadumu kwa muda mrefu. Wananchi wanapolitoa uongozini kundi moja la wasaliti huwa na matumaini kuwa kundi jipya wanalolichagua litakuwa na suluhu kwa matatizo yao. Ajabu ni kwamba msimu mmoja wa wasaliti hufuatwa na msimu wa wasaliti wengine, kama inavyobainishwa na Mberia (2007) katika shairi liitwalo ‘Msimu Mwingine wa Wasaliti’ (uk. 12). Mshairi anaueleza msimu huo kama ifuatavyo:

Vitimbakwira watarudi karibuni kutoka karamu haramu
Utazona barakoa za tabasamu kwenye nyuso zao
Watakuja kutugawia peremede zenye sumu ya akili
Watalewesha watu kwa pombe kutoka vibuyu vya maneno
Wataahidi kesho yenye mapipa ya maziwa na mitungi ya asali
Nasi, tukiongozwa na ramani ya tumbo na dira ya ubinafsi
Tutapanga milolongo katika mvua ya Disemba
Tukikaribisha, labda, msimu mwingine wa wasaliti

Ujumbe unaojitokeza katika kifungu hiki ni kuwa huenda wanasiasa wasibadilike hata majira yanapobadilika. Mbinu ya kuwadanganya wananchi kijanja hutumiwa kila msimu wa uchaguzi. Wananchi pia wana fungu lao la lawama. Inaonekana kuwa hawajifunzi kutokana na tabia za wanasiasa wa hapo awali. Baada ya kuhongwa na kuhadaiwa na wanasiasa, wananchi huwapigia kura wajanja hawa na kuliweka mamlakani kundi jingine la wasaliti.

5.4.10 Wanafiki

Kuna ushahidi wa kutosha kutokana na mashairi yaliyohakikiwa katika utafiti huu kuwa baadhi ya wanasiasa wa kipindi cha siasa za vyama vingi ni wanafiki. Kama tulivyoona katika sehemu iliyopita Babu (2007), katika shairi lake liitwalo ‘Msitu ni ule ule’ (uk. 29), anawakashifu wanasiasa kwa unafiki wa kuzozozana hadharani ili kuwafanya wananchi kudhani kuwa walikuwa maadui. Aidha, Mberia (2007) katika shairi lake liitwalo ‘Msimu Mwingine wa Wasaliti’ (uk. 12) amedhihirisha unafiki wa wanasiasa katika muktadha wa kampeni za uchaguzi. Amabainisha kuwa wanasiasa huwahadaa wananchi ili wawapigie kura kwa kuwaahidi mengi mazuri huku wakijua kuwa ahadi zao ni za uongo.

Ushahidi zaidi wa unafiki wa wanasiasa unapatikana katika shairi liitwalo ‘Tume za Rais’ (uk. 31) ambapo mshairi anaonyesha jinsi tume za rais huundwa kwa unafiki mkubwa na kuishia katika matumizi makubwa ya pesa za umma. Mshairi anaanza utungo wake hivi:

Napendekeza tuunde tume ya rais
Tumnunulie kila mwanatume *Hummer*
Ichunguze kama njaa inaweza kuua
Kisha tuunde tume nyingine ya rais
Ihariri taarifa ya tume ya rais

Kinachobainika hapa ni kuwa wakati mwingine tume hizi huundwa kuchunguza mambo ambayo ukweli wake ni dhahiri. Kwa mfano, mshairi anazungumzia kuundwa kwa tume ya rais kuchunguza iwapo njaa inaweza kuua. Isitoshe, wanachama wa tume hizo wanaishi kwa anasa huku wananchi wakimalizwa na njaa ile ile inayodaiwa kuchunguzwa. Huu ni unafiki mkubwa kwani pesa nyingi zinazotumiwa kuwastarehesha wanatume ndizo zingeanzisha miradi ya kumaliza njaa.

Katika vifungu vinavyofuatia mshairi anaonyesha unafiki zaidi wa wanasiasa kwa kufichua ubadhirifu zaidi unaohusishwa na tume hizi. Mshairi anaendelea:

Napendekeza tuunde tume ya rais
Tumjengee kila mwanatume kasri
Ichunguze jina la Rais wa Jamhuri
Kisha tuunde tume nyingine ya rais
Imtangazie Rais jina la Rais

Mshairi analenga kubainisha jinsi wakati mwingine wanasiasa hufuja hazina ya taifa kwa mambo ya kinafiki yanayolengwa kumtukua kiongozi wa taifa husika. Tume ya kuchunguza jina la rais inayotajwa hapa haina manufaa yoyote kwa umma. Wanaonufaika ni wanatume ambao wanajengewa majumba ya kifahari. Wananchi maskini huendelea kuishi katika vibanda licha ya kuwa ndio walipa ushuru unaotumiwa na serikali kuwastarehesha wanatume, ambao aghalabu huwa wanasiasa. Kilele cha unafiki unaohusiana na uundaji wa tume za rais kinafikiwa katika kifungu cha mwisho cha shairi hili. Mshairi anafichua kuwa kutotangazwa kwa matokeo ya uchunguzi unaofanywa na tume mbalimbali huwa ni njama ya wanasiasa wanafiki. Mshairi anasema hivi:

Napendekeza tuunde tume ya rais
Tuilipe kwa mkopo kutoka vitanzi vya Breton Woods
Baada ya miaka mitano ya kumandari na kunywa mvinyo
Wamshauri rais namna ya kuficha taarifa za tume ya rais
Katika sefu za vyumba vya ndani vya mijengo ya rais

Tunaoshuhudia hapa ni wanasiasa wanafiki wanaoongoza kwa hila. Tume inayoundwa inafurahia jasho la wananchi kwa miaka mitano, kipindi kamili ambacho wanasiasa hukaa uongozini, kabla ya uchaguzi mwingine. Hatimaye matumaini ya umma huvunjwa kabisa. Wanafiki hawa wanamshauri rais jinsi ya kuficha ripoti za tume badala ya kuhakikisha kuwa matokeo yake yanatangazwa kwa umma na mapendekezo yake kutekelezwa.

Kwa kuhitimisha sehemu hii, hebu tuangalie muhtasari uliotolewa na Mberia (2007) kuhusiana na unafiki wa mwanasiasa wa Afrika katika shairi liitwalo 'Magenge Matatu' (uk. 32). Mshairihapaanarejelea kipindi cha baada ya uhurukatika awamu tatu kama zilivyobainishwa katika utafiti huu. Awamu hizi ni kipindi cha waliochukua mamlaka kutoka kwa wakoloni, udikteta wa chama kimoja, na hatimaye kipindi cha siasa za vyama vingi. Kuhusiana na wanasiasa wa kipindi cha kwanza mshairi anasema hivi:

Genge la kwanza la mazimwi
Lilituahidi nchi bila minyororo ya kutojua, maradhi na umaskini
Tukanengukanenguka viwanjani kwa shangwe na vigelegele;
Mwongo na nusu wa upepo wa ulafi na ukungu wa ufisadi
Ukazima mwenge wa utaifa na kuangusha uzalendo mtaroni
Harufu ya ukabila ikachafua nchi kama uzushi wa kicheche

Kwa mujibu wa mshairi, punde tu uhuru ulipopatikana, paliingia genge la wanasiasa ambalo lilidhamiria kujinufaisha tu. Wanasiasa hawa waliwaahidi wananchi kuwa wangeangamiza kutojua, magonjwa na umaskini. Wananchi waliwarundika sifa bila kutambua kuwa hawa walikuwa wanafiki waliojaa ulafi na ufisadi. Unafiki huu uliangamiza uzalendo na mahali pake kuchukuliwa na ukabila.

Kipindi kilichofuatia pia kilitawaliwa na kundi la wanafiki waliotumia lugha tamu kuulaghai umma. Mshairi analieleza kundi hili kwa maneno haya:

Genge la pili la mazimwi
Lilituahidi majira maangavu ya amani, upendo na umoja
Tukajijeruhi koo kwa kuimba “Juu! Juu! Juu sana!”
Baada ya miongo miwili viwavi na nzige wakitafuna nchi
Jamhuri ilishuka katika jahanamu ya moto wa AK 47
Zao la umaskini unaovuma kama bahari kwenye miamba

Kwa mujibu wa mshairi, wananchi walidhani kuwa baada ya kundi la kwanza kuondoka maovu yaliyoandamana nalo pia yangeondoka. Kundi hili liliahidi kuwepo kwa taifa jipya lenye amani, upendo na umoja. Ahadi hii iliuchangamsha umma na kuufanya kulisifu hata kuliko kundi la kwanza. Kilichouvunja umma mioyo ni kwamba kundi hili lilijaa ulafi uliotishia kuliangamiza taifa. Umaskini ulibaki kuwa urithi ulioachwa na kundi hili.

Nalo kundi la tatu, ambalo mshairi anaita genge la nusu-mazimwi, lilionekana kuwa afadhali likilinganishwa na magenge mawili ya awali. Ahadi zake za kuondoa utawala mbaya uliokuwepo hapo awali zinajitokeza katika kifungu kifuatacho:

Genge la tatu, nusu-mazimwi
Lilituahidi katiba mpya na dawa kali dhidi ya ufisadi
Tukaamini wimbo “Yote yawezekana bila Mfalme wa Nzige”
Baada ya miaka minne ya hila, tamaa na usingizi ulingoni
Ahadi iliyomwesamwesa kama nyota ya taifa jipya
Imewezwa na wingu la ujanja na harufu ya ufisadi

Unafiki unaobainika hapa ni ule wa wanasiasa wanaoliondoa kundi la awali na kuibadilisha katiba bila kubadilisha nia zao. Licha ya kuahidi mwisho wa ufisadi, kundi hili jipya linaongoza kwa hila, tamaa, ufisadi na kutowajibika, sawa na kundi lililotangulia. Taifa jipya lililoahidiwa bado halijazaliwa.

5.5. Hitimisho

Katika sura hii tumechunguza mabadiliko ambayo mwanasiasa wa Afrika amepitia katika awamu tatu. Awamu ya kwanza ni ile ya wanasiasa waliochukua mamlaka kutoka kwa wakoloni. Tumeona kuwa, punde tu walipochukua mamlaka kutoka kwa wakoloni, wanasiasa hawa walibadilika ghafla na kuwa wakoloni mamboleo. Waliwasaliti wananchi waliokuwa wakiwasifu kwa kuwaondoa wakoloni na kuwaahidi maisha bora baadaye. Demokrasia ambayo wananchi waliahidiwa iliuliwa na mahali pake kuchukuliwa na udikteta wa wanasiasa wasiopenda kukosolewa.

Awamu ya pili ni ile ya kipindi cha uteteaji wa demokrasia ya vyama vingi. Katika awamu hii, paliibuka kundi la wanasiasa waliowaahidi wananchi maisha bora punde tu walipochukua mamlaka kutoka kwa viongozi wa awali waliorithi siasa za kikoloni. Tumeona jinsi kundi hili la wanasiasa lilivyouandama mfumo wa siasa za chama kimoja huku wakigeuka na kuwa wakandamizaji hata kulishinda kundi la kwanza. Kundi hili lilijaa tamaa, ubinafsi, ujanja, ufisadi na unafiki uliotishia kuyaangamiza mataifa husika.

Hatimaye, awamu ya tatu inajumuisha wanasiasa waliojitokeza awali kama watetezi wa demokrasia kamili kupitia uanzishwaji wa mfumo wa siasa za vyama vingi. Utafiti huu umethibitisa kuwa mpito wa wakati pamoja na mabadiliko ya mfumo wa kisiasa havikubadilisha kamwe tabia za mwanasiasa wa Afrika. Kwa mujibu wa washairi ambao kazi zao zilihakikiwa katika utafiti huu, matumaini ambayo wananchi walikuwa nayo katika kundi hili la wanasiasa yalikuwa ya muda tu. Kundi hili lilitawala kwa hila, tamaa na kutowajibika sawa na kundi lililotangulia. Sura ifuatayo inajumuisha muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu.

SURA YA SITA

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

6.1 Muhtasari

Utafiti huu ulichunguza nafasi ya ushairi wa Kiswahili katika uhifadhi wa historia ya mwanasiasa wa Afrika. Tabia na vitendo vya mwanasiasa wa Afrika kabla na baada ya uhuru kwa mujibu wa ushairi wa Kiswahili pia vilibainishwa. Kipindi cha baada ya uhuru kilijumuisha utawala chini ya mfumo wa siasa za chama kimoja na ule wa chini ya siasa za vyama vingi. Ubainishaji huu ulihusisha uhakiki wa kazi mbalimbali za kishairi ambamo mwanasiasa huyu alijitokeza kama mhusika. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Ulimbwende na nadharia ya Baada-Ukoloni.

Nadharia ya Ulimbwende inafafanua umuhimu wa kuzingatia usawiri wa wahusika kiubunifu katika mashairi kwa mujibu wa mazingira wanamopatikana. Nadharia hii pia inashikilia kuwa mshairi anapotunga kazi yake anafaa kuwatumia wahusika kutolea hisia mbalimbali kuhusiana na watu na matukio anayokumbana nayo katika mazingira yake. Aidha, nadharia hii inazingatia kuwa kilicho muhimu katika ushairi si kufungwa na sheria za utunzi bali kujieleza kikamilifu.

Kwa mujibu wa nadharia ya Baada-Ukoloni, athari za kikoloni zilizosalia baada ya kuondoka kwa wabeberu bado zinaliathiri bara la Afrika katika sekta za kisiasa, kijamii na kiuchumi. Baadhi ya athari hizo ni kuibuka kwa tabaka la wanasiasa wanyanyasaji ambao lengo lao kuu ni kujinufaisha kiuchumi. Aidha, baadhi ya wanasiasa hao waliiga utovu wa kimaadili kutoka kwa wakoloni ambao wanaendeleza mpaka sasa.

Mbali na kubainisha tabia za mwanasiasa wa Afrika, utafiti huu ulitambua umuhimu wa ushairi wa Kiswahili katika uhifadhi wa historia ya kijamii. Hii ilitokana na dhana kwamba ushairi wa Kiswahili ndio utanzu wa fasihi ulio na historia ndefu kuliko tanzu nyingine za fasihi. Tanzu nyinginezo ni riwaya, tamthilia na hadithi fupi. Aidha, kuna ithibati kwamba ushairi umetumiwa kwa muda mrefu kama chombo cha kuwasifia na kuwakosoa wanasiasa. Ushairi pia umekuwa, na ungali unatumiwa kutetea pamoja na kuzindua umma dhidi ya ukandamizaji wa wanasiasa dhalimu.

6.2 Hitimisho

Sehemu hii inahitimisha matokeo ya utafiti huu kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti. Madhumuni ya kwanza yalikuwa kuchunguza nafasi ya ushairi wa Kiswahili katika uhifadhi wa historia ya mwanasiasa wa Afrika. Madhumuni ya pili yalikuwa kubainisha sifa za mwanasiasa wa Afrika kabla ya uhuru kwa mujibu wa ushairi ya Kiswahili. Nayo ya tatu yalikuwa kutathmini mabadiliko ya mwanasiasa wa Afrika baada ya uhuru kwa mujibu wa washairi wa Kiswahili.

Ilibainika kuwa ushairi wa Kiswahili una dhima kuu ya kuhifadhi historia ya mwanasiasa wa Afrika. Kupitia usawiri wa mwanasiasa huyu katika vipindi mbalimbali vya kihistoria, ilidhihirika kuwa ushairi wa Kiswahili unaweza kurejelewa kama hazina muhimu na ya kutegemewa. Uhakiki wa mashairi teule uliofanywa katika utafiti huu ulirejelea sifa na tabia za wanasiasa halisi pamoja na matukio yanayoweza kuthibitishwa katika muktadha wa historia.

Utafiti huu pia ulibainisha sifa muhimu za mwanasiasa wa Afrika katika kipindi cha kabla ya uhuru zilizomfanya kupendwa, kuheshimiwa na kutegemewa na umma. Uhakiki wa *Utendi wa Uhuru wa Kenya* ulidhihirisha kuwa mwanasiasa wa kipindi cha kabla ya uhuru alikuwa na sifa kama vile uzalendo, ujasiri na upatanishi. Mzee Kenyatta, ambaye aliwakilisha kundi hili la wanasiasa katika utafiti huu, aliwaunganisha watetezi wengine wa uhuru kutoka kwa mikoa tofauti. Jambo hili liliwafanya kupigania uhuru kutoka kwa mbeberu bila kujali misingi yao ya kikabila, kiumri au kijinsia. Uzalendo huu ndio uliomfanya Mzee Kenyatta na wenzake watano – Karumba, Kaggia, Ngei, Oneko na Kubai kutiwa gerezani kwa miaka saba.

Sifa nyingine iliyojitokeza ni ukakamavu. Hii ni hali ya mtu kuwa na msimamo thabiti usiobadilika kutegemea matukio au hali inayomkabili. Kibao (1972) amemsawiri mwanasiasa wa kipindi cha kabla ya uhuru kama shujaa asiyetishwa na wabeberu wala mateso aliyoyapata gerezani. Mateso haya yalikuwa ni pamoja na kupigwa, kunyimwa chakula na hata kutishiwa kuuawa.

Baada ya uhuru, Mwanasiasa wa Afrika aligeuka ghafla na kuwa mzungu mweusi aliyewadhulumu wananchi. Katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* mshairi anaonyesha jinsi kundi la wanasiasa walioingia mamlakani waligeuka kuwa wanyakuzi wakubwa wa

mali ya umma, ikiwemo ardhi. Hali hii ilisababisha ubaguzi katika ugawanyaji wa rasilimali za kitaifa. Mataifa ya Afrika yaligawanyika katika tabaka mbili kuu; tabaka la matajiri na lile la maskini.

Utafiti huu pia ulibainisha jinsi utawala wa baada ya uhuru ulijihami dhidi ya Upinzani. Wakosoaji wa serikali walitiwa hofu na wanasiasa dhalimu. Ilibainika kuwa wananchi, wakiwemo washairi wa Kiswahili, walilazimika kutumia jazanda walipowarejelea wanasiasa hao. Hii ndiyo sababu katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* wanasiasa hawa wamesawiriwa kama *jipu*, yaani uvimbe wenye uchungu mkali, kwa vile walivyowatesa wananchi. Pia wivu wake unalinganishwa na ule wa *mamba* anayewazuia watu kuteka maji kisimani. Kwa kuwalinganisha na *misumari* mshairi anaashiria haja iliyopo ya kuwaondoa viongozi wabaya ili demokrasia na maendeleo vipatikane. Utumiaji huu wa jazanda ulighubika sifa kama vile ukatili, kiburi, wivu na ujeuri.

Aidha, ilibainika kuwa hali ilizidi kuwa mbaya wakati wa kipindi cha siasa za chama kimoja. Kwa mujibu wa mashairi yaliyohakikiwa kutoka kwa *Chembe cha Moyo*, wanasiasa waliokuwa mamlakani katika kipindi cha siasa za chama kimoja walijaa ubinafsi, tamaa ya mali, ufisadi, usaliti na unafiki. Hawa waliendeleza unyakuzi wa mali ya umma, utabaka na uangamizaji wa demokrasia sawa na watangulizi wao. Uchochezi wa vita vya kikabila, ubakaji na mauaji pia vilitekelezwa na baadhi ya wanasiasa wa kipindi hicho.

Idhihirika pia kuwa mwanasiasa wa Afrika katika kipindi cha siasa za vyama vingi hakubadilika na kuwa bora akilinganishwa na yule wa siasa za chama kimoja. Mashairi yaliyohakikiwa kutoka kwa *Diwani ya Karne Mpya* na *Msimu wa Tisayalidhihirisha* sifa kama vile usaliti, unafiki, ufisadi, tamaa, uongo na ujanja miongoni mwa wanasiasa wa kipindi hicho. Unyakuzi wa ardhi, kujiongezea mishahara licha ya upinzani kutoka kwa umma na uendelezaji wa tabaka pia ulikithiri. Tabia nyingine zilizoshuhudiwa katika kipindi cha siasa za vyama vingi ni pamoja na kutowajibika kazini, kung'ang'ania mamlaka, migawanyiko kwa misingi ya vyama vya kisiasa, uchochezi wa vita vya kikabila, uzinzi, ubakaji na mauaji.

Mwanasiasa wa kipindi cha siasa za vyama vingi, sawa na mwenzake wa kipindi cha siasa za chama kimoja, alikuwa kibaraka cha wageni. Katika diwani ya *Chembe cha Moyo*, wanasiasa wanarejelewa kijazanda kama *vinyago* kwani walifuata matakwa na tabia za waliokuwa wakoloni. Pia walikuwa wakandamizaji wa wapinga demokrasia. Ndiposa wanaitwa *vigingi vikavu* kwa vile wananchi waliwaona kama vikwazo kwa demokrasia na maendeleo ambavyo vilifaa kung'olewa. Kwa kuwarejelea kama *wala njama* Mberia (2007) anaonyesha jinsi wanasiasa walivyosahau tofauti zao za kisiasa na kikabila na kushirikiana walipodhamiria kujinufaisha. Jazanda ya *majitu manene mazito* inaashiria manufaa makubwa ambayo wanasiasa walipata walipowanyanyasa wananchi, kiasi cha miili yao kunenepa kutokana na shibe ya jasho la umma. *Mafunza* ni jazanda inayoashiria unyonyaji wa wanasiasa na jinsi wanavyoutegemea umma kujiendeleza. Kwa kuwaita *wanaharamu*, mshairi anamaanisha kwamba wanasiasa hawa wameiga maovu mengi kutoka kwa wakoloni, kiasi cha kutokubalika katika jamii ya Kiafrika.

Matumizi ya jazanda pia yanapatikana katika *Diwani ya Karne Mpya* ambapo wanasiasa wanatajwa kama *fisi* kutokana na sifa yao ya ulafi. Pia wanalinganishwa na *nzige wa jangwa* kutokana na uharibifu wao unaotishia kuangamiza binadamu wengine. Kwa kuwalinganisha na *konokono*, mtunzi anaashiria uzembe ulioathiri utendakazi wa wanasiasa bungeni.

Kwa jumla, utafiti huu ulibainisha kuwa mwanasiasa wa Afrika katika kipindi cha kabla ya uhuru alijitolea kikamilifu, bila malipo yoyote, kuukomboza na kuuendeleza umma. Hata hivyo, kipindi hicho hakikukosa wanasiasa wenye dosari kitabia na kivitendo. Katika *Utendi wa Uhuru wa Kenya* mshairi amezungumzia jinsi wanasiasa wachache waliojitakia makuu walijaribu kwenda kinyume na juhudi za wazalendo kwa kuhusika katika vitendo vya usaliti na ufisadi.

Ilibainika pia kuwa mabadiliko ya mifumo ya kisiasa hayakubadilisha tabia na vitendo vya wanasiasa. Baadhi ya wanasiasa walioonekana kuwa watetezi wakuu wa umma wakati wa kutetea demokrasia ya vyama vingi hawakuyaimarisha maisha ya umma walipoingia mamlakani. Tabia zao zilibaki sawa na zile za watangulizi wao, wale wa kipindi cha baada ya uhuru, hasa wakati wa udikteta wa chama kimoja.

Ingawa mashairi mengi yaliyohakikiwa yalimsawiri mwanasiasa wa kipindi cha baada ya uhuru kama kiongozi asiyeweza kutegemewa, bara la Afrika limewahi kuwa na wanasiasa vielelezo. Katika diwani ya *Msimu wa Tisa* aliyekuwa rais wa Tanzania marehemu Julius Kambarage Nyerere alisawiriwa kama *mwashi*, yaani mjenzi, aliyejitolea kuhakikisha kuna amani, usawa na demokrasia nchini mwake. Amelinganishwa na wanasiasa wengine maarufu kama vile Kwame Nkrumah (Ghana), Sekou Toure (Gine), Samora Machel (Msumbiji) na Nelson Mandela (Afrika Kusini) ambao wameingia katika kumbukumbu kwa uzalendo wao.

6.3 Mapendekezo

Utafiti huu ulihakiki kazi za kishairi zilizochapishwa kati ya mwaka wa 1972 hadi 2007. Utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusiana na kazi za kishairi zilizotungwa baadaye ili kubainisha iwapo mabadiliko yoyote muhimu ya mwanasiasa wa kipindi cha siasa za vyama vingi yanadhihirika.

Utafiti pia unaweza kufanywa kuhusiana na kazi mpya za kifasihi zinazoangazia mabadiliko ya kisiasa kama vile uanzishwaji wa serikali za kaunti nchini Kenya. Kuibuka kwa wanasiasa kama vile magavana, maseneta, wawakilishi wa wanawake bungeni na wajumbe wa kaunti na mchango wao katika masuala ya uongozi ni dhana inayoweza kuchunguzwa.

Kwa kuwa utafiti huu ulijifunga na utanzu wa ushairi uliotungwa kwa Kiswahili, utafiti wa baadaye unaweza kufanywa kuhusiana na ushairi uliotafsiriwa kutoka kwa lugha na tamaduni nyinginezo ndani na nje ya bara la Afrika. Utafiti pia unaweza kufanywa kuhusiana na usawiri wa mwanasiasa wa Afrika katika tanzu nyingine za fasihi, ikiwemo fasihi simulizi.

MAREJELEO

- Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.
- Abdulaziz, M. (1979). *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Verse*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Akivaga, S. K. (2002). Towards a National Movement for Democratic Change in Kenya. In Kioko, W, Mute, L.M & Akivaga, S.K. (eds). *Building an Open Society: The Politics of Transition in Kenya*. Nairobi: Claripress.
- Ashcroft, B. Griffiths, G. & Tiffin, H. (2007). *Post-Colonial Studies: The Key Concepts*. London: Routledge.
- Asingo, C. O. (2003). The Rise and Fall of The Autocratic State in Kenya. In Oyugi, W. O, Wanyande, P & Mbai, C. O. (eds). *The Politics of Transition in Kenya: From KANU to NARC*. (pp. 15-50). Nairobi: Heinrich Boll Foundation.
- Atieno, O., Ouso, E. S & Williams J. F. M. (1977). *A History of East Africa*. London: Longman Group Ltd.
- Bertoncini, E. Z. (2010). Some Remarks on Kithaka wa Mberia's Poetry. *Swahili Forum 17 (2010): 91-103*.
- Bigombe, B. O. (1993). Uganda Government Approach to Conflicts in the North and North Eastern Uganda. *Nordic Journal of African Studies 2(2):109-117*.
- Chacha, N. C. (1980). *Ushairi wa Abdilatif Abdalla. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa*. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Chacha, N. C. (1992). *Ushairi wa Abdilatif Abdalla: Sauti ya Utetezi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Childs, P., Williams, R. J. P. (1997). *An Introduction to Post-Colonial Theory*. London: Prentice Hall.
- Dumila, F. (1971). *Wasifu wa Kenyatta*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Emaittah, G. (2007). *Modern Play in Kiswahili: A Study of Its Development in Kenya, 1953-1975. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa*. Pretoria: University of South Africa.
- Foakes, R. A. (1968). *Romantic Criticism*. London: Edward Arnold.
- Frolova, N. (2003). Euphrase Kezilahabi: The Renewal of Kiswahili Poetry. *Kiswahili*, 66. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar-es-Salaam.
- Gachukia, D. (2005). Government by Tribe or Government by Political Parties? In Wanjohi, G. J. & Wanjohi, G. W. (Eds.). *Social and Religious Concerns of East Africa*. (pp. 101-107). Nairobi: Wajibu

- Government of Kenya. (2007). Report on Tharaka, Tigania Conflict by Njuri Ncheke Boundary Arbitration Committee.
- Hamisi, J. (2011). *The Politics of Betrayal: Diary of a Kenyan Legislator*. New Trafford: Trafford Publishing.
- Havnevik, K. & Isinika, A. K. (2010). *Tanzania in Transition: From Nyerere to Mkapa*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
- Hill, J. S. (1977). *The Romantic Imagination*. London: Macmillan Press Ltd.
- Jordan, J. E. (1976). *Why the Lyrical Ballads?* Berkeley: University of California Press.
- Kanyinga, K., Long, J. D, & Ndi, D. (2008). Report on Fraud. <http://www.africog.org/reports/KPTJ-submission-to-the-Kriegler-Commission.pdf>, accessed 4-4-2012.
- Kazungu, K. (1984). Utangulizi. Katika Mohamed, S. A. *Kina cha Maisha*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Kelly, R. M. (2014). Corruption in Africa: Cultural, Economic and Political Factors Which Impact Corruption and Potential Solutions. Unpublished MA thesis. New Jersey: The State University of New Jersey.
- KENFAD, (1997). *Civic Education for Grassroot Community Empowerment and Democratisation of Social Institutions*. Nairobi: KENFAD.
- Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinemann.
- Kezilahabi, E. (1976). *Ushairi wa Shaaban Robert*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Kezilahabi, E. (1983). Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili. *Fasihi, Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. TUKI. S. 223-238 (B. 8.16.13) 144163.
- Khatibu, M. S. (1975). *Utenzi wa Ukombozi wa Zanzibar*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Kibao, S. A. (1972). *Utenzi wa Uhuru wa Kenya*. Nairobi: Oxford University Press.
- Kibwana, K. (1996). Mustakabali wa Mabadiliko ya Katiba Nchini Kenya. Katika Kibwana, K., Kimondo, G. K., & Gathii, J. T., (Wah.). *Mwananchi na Katiba*. (kur. 44-46). Nairobi: Claripress.
- Kimondo, G. K. (1996). Kuanzisha Tena Kwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. Katika Kibwana, K., Kimondo, G. K., & Gathii, J. T., (Wah.). *Mwananchi na Katiba*. (kur. 44-46). Nairobi: Claripress.
- King'ei, G. K. (1999). *Miale ya Uzalendo*. Nairobi: Phoenix Publishers.

- King'ei, G. K & Kemoli, A. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.
- Kinyatti, M. (1992). *Mau Mau: A Revolution Betrayed*. London: Vita Books.
- Kipsang, S., Chepkuto P. K. (2011). Reflections on Political and Governance Systems in Kenya. *International Journal of Current Research*. Vol. 3,8, pp.163-167, August, 3011.
- LeVan, A. C. (2011). Power Sharing and Inclusive Politics in Africa's Uncertain Democracies. *Governance: An International Journal of Policy, Administration and Institutions*. Vol. 2, Issue 1, pp. 31-53, January, 2011.
- Maitaria, J. N. (2012). Uainishaji wa Ushairi wa Kiswahili: Dhima ya Methali. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Makillah, S. (2009, Oktoba 10). Vikwazo kwa Demokrasia Nchini. *Mwananchi*. Kupitia: www.nation.co.ke.
- Masinde, E. W. (2002). Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Massamba, D. P. B. (2003). Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili. *Fasihi: Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. TUKI. TUKI. S. 55-95 (B. 8.16.13).
- Mazrui, A. (1988). *Chembe cha Moyo*, Nairobi: Heinemann
- Mazrui, A. M & Syambo, B. K. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers
- Mberia, K. (2007). *Msimu wa Tisa*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.
- Mboya, T. (1970). *The Challenge of Nationhood: A Collection of Speeches and Writings*. London: Deutsch.
- Mbugua, B. (1988). Democracy Takes a Step Down. *Beyond*, 2.
- Miguna, M. (2012). *Peeling Back the Mask: A Quest for Justice in Kenya*. London: Gilgamesh Africa.
- M'Ngaruthi, T. K. (2007). Usawiri wa Wahusika katika *Dafina ya Umalenga* (H. M. Mbega) na *Jicho la Ndani* (S. A. Mohamed). Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- M'Ngaruthi, T. K. (2012). *Miale ya Mashariki: Mashairi na Mwongozo wa Uchambuzi*. Ontario: Nsemia Inc. Publishers.

- Mohamed, S. A. (1967). *Utenzi wa Uhuru wa Tanganyika*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mohamed, S. A. (2002). *Jicho la Ndani*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Momanyi, C. (1998). Usawiri wa Mwanamke Mwislamu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Morgenthau, H. J. (1978). Fifth Edition. *Politics Among Nations: The Struggle for Power and Peace*. New York: Alfred A. Knopf.
- Mrikaria, S. E. (2010). Kejeli na Fasihi ya Kiswahili – Tanzania. *Swahili Forum 17 (2010): 104-125*.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers
- Muindi, B. (2012, April 10). Arms race hots up in East Africa. *Daily Nation*, p.56.
- Mulokozi, M. (1982). Protest and Resistance in Swahili Poetry. *Kiswahili 49/1:25-54*.
- Mulokozi, M. (1992). Kalevala and Africa. *Nordic Journal of African Studies 1(2):71-80*. www.njas.helsinki.fi/pdf-files/vol1num2/mulokozi.pdf, accessed 15-6-2011.
- Mulokozi, M. (2000). *History of Kiswahili Poetry: A.D 1000-2000*. Dar es Salaam: TUKI.
- Munene G. M. (2005). Leadership: Kenyatta and Nkrumah. In Wanjohi, G.J. & Wanjohi, G.W. (Eds.) *Social and Religious Concerns of East Africa*. (pp. 85-100). Nairobi: Wajibu.
- Mvungi, T. (1982). *Raha Karaha*. Dar es Salaam: Continental Publishers.
- Mwamzandi, I. Y. (1996). Mbinu za Kimaigizo katika Tungo za Abdilatif Abdalla. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Njoro: Chuo Kikuu cha Egerton.
- Mwamzandi, I. Y. (2002). Usemezano katika Umalenga wa Kiswahili: Mfano wa Taarab. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Njoro: Chuo Kikuu cha Egerton.
- Mworia, L. K. (2009). An Evaluation of Continuous Conflict Between Related Communities: A Case of Tharaka and Tigania Communities. Unpublished MA Project Report. Nairobi: University of Nairobi.
- Nabhany, A. S. (1987). Utangulizi. Katika Chiraghdin, S. *Malenga wa Karne Moja*. Nairobi: Longhorn Kenya.

- Ndungo, C. M. (1985). *Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria*. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijchapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi
- Njogu, K. (2004). *Reading Poetry as Dialogue*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustana College.
- Ousby, I. (1996). *Guide to Literature in English*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Ruo, K. R. (1983). Suala la Ushairi wa Kiswahili; Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: *Fasihi (1983):127-143*.
- Senkoro, F. E. M. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Simala, K. I. (2004). Swahili Poetic Text and African Historiography. *Sudanic Africa, Vol. 15*. Pp. 17-38. <http://www.jstor.org/stable/25653411>, accessed 23-08-2011.
- Skinner, E. P. (2010). African Political Cultures and the Problems of Government. <http://www.africa.ufl.edu/asq/v2/v2i3a3.pdf>, accessed 24-08-2011.
- Southall, R. (2008). Democracy and Power; Africa and Democracy. <http://www.africa.ufl.edu/>, accessed 10-10-2009.
- Thiong'o, N. (1981). *Writers in Politics*. Nairobi: Heinemann Kenya Ltd.
- Topan, F. (1974). Utangulizi. Katika Kezilahabi, E. *Kichomi*. Nairobi: Heinemann.
- Wafula, R. M. & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Waliaula, K. A. (2009). The Incarcerated Self: Narratives of Political Confinement in Kenya. Unpublished PhD Dissertation. Ohio: Ohio State University.
- Walibora, K. (mh.) (2007). *Diwani ya Karne Mpya*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, K. W. (2002). Utangulizi. Katika Mohamed, S.A. *Jicho la Ndani*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, K. W. (2006). *Kamusi ya Ushairi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.
- Wamitila, K. W. (2010). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers

Wanyande, P. (1997). *State Driven Conflict in the Greater Horn of Africa*.
www.pdfbe.com/pe/peter-horn-book.pdf , accessed 20-5- 2011,

Wellek, R. & Warren, A. (1985). *Theory of Literature*. Hamorndsworth: Penguin.

Wordsworth, W. (1925). *Lyrical Ballads with A Few Other Poems*, London: Bristol.

KIAMBATISHO 1: SAUTI YA DHIKI (ABDALLA, 1973)

N'shishiyelo Ni Lilo

1

Napulikiza ndu yangu, ninenayo usikiye
Yaliyo moyoni mwangu, ningependa nikwambiye
Ujuwe imani yangu, ambayo niishishiye
Siiwati ingawaje, ambayo niishishiye

2

Walineni walimwengu, wa zama zilopisiye
Kwamba kweli i utungu, kwa yule aambiwaye
Nami haya ndugu yangu, sasa niyaaminiye
Asojuwa nasikiye, apeleleze ajuwe

3

Kweli nnaifahamu, haipendwi aswilani
Kwa mja hiyo ni sumu, mbaya iso kifani
Mwenye kuitakalamu, hapendezi katwaani
Sasa nshayaamini, ni kweli haya ni kweli

4

Kweli imenitongeya, kwa kuinena mwendani
Wale nalowaambiya, wamenitiya dhikini
Wameniona mbaya, kumshinda Firauni
Kweli, sasa naamini, si wangi waipendao

5

Kweli naliwaambiya, wakuu w anti hini
Haeleza moya moya, kwa wanati wa ntini
Kuhusu walofanyiya, upande wa upinzani
Sasa kuwamo tabuni, nalipwa kwa hiyo kweli

6

Kweli ilipowatoma, kama dasturi yake
Wao wakaona vyema, afadhali wanishike
Wanishike hima hima, hima ndani waniweke
Ngomeni n'adhibike, nijute kusema kweli

7

Kweli yanipasha tabu, ndugu yangu niamini
Na nyingi mno adhabu, za moyoni na mwilini
Yote haya ni sababu, ya kunena kweli hini
Ndipo sasa haamini, kweli i utungu kweli

8

Kweli menibaidisha, na huko kwetu mjini
Pia menitenganisha, na walo wangu nyumbani
Kuja kuniadhibisha, kwa kunnileta ngomeni
Yote sababu ni nini? Ni kwamba mesema kweli

9

Kweli menifunga ndani, ya chumba nde sitoki
Kutwa kucha ni chumbani, juwa kuota ni dhiki
Na mlinzi mlangoni, yu hapo kattu ha'ndoki
Nilindwavyo bilhaki, ni kama samba marara

10

Kweli yanilaza tini, ilo na baridi kali
Ningawa burangetini, natetema kweli kweli
Na maumivu mwilini, daima ni yangu hali
Shauri ya idhilali, ya kulazwa simitini

11

Kweli japo ni ngomeni, kwenye kuta ndefu nene
Kabisa sitangamani, na mahabusu wingine
Na lengo kubwa nadhani, ni: nilonalo 'sinene
Hazua mambo mingine, kwa kuambukiza watu

12

Kweli pia meninyima, haki zilizo ngomeni
Wangu kuja nitizama, hilo haliwezekani
Haya nnayoyasema, ndivyo yalivyo yakini
Baruwa sitakikani, kwandika wala kwetewa

13

Sendi mbele tasimama, sikupi kwa tafswili
Kusudi nirudi nyuma, kwa ubeti wa awali
Ili nipate kusema, imani yangu kamili
Ujuwe kwa jambo hili, mtima wangu ulivyo

14

Nilipoenua kimo, kutaka niseme kweli
Nilidhani yaliyomo, hinena sina aili
Kanama wangu mdomo, waja fungika kauli
Nisiseme bilkuli, kuwaeleza wanati

15

Mno wanganiadhibu, adhabu kila namna
Na mangi yanganiswibu, ya usiku na mtana

Hayatakuwa sababu, ya kuniasa kunena
Kweli nitapoiyona, tanena siinyamai

16

Mateso yao yangawa, nda kuumiza mtima
Hayatakuwa ni dawa, ya kutonipa kusema
Ni bure wajisumbuwa, nilipo nnasimama
Si 'mi wa kurudi nyuma, kweli ilipo 'tasonga

17

Ama hakika mwendani, kwa mwenye moyo wa sawa
Mateso ya duniani, wakati kijaaliwa
Hushukuru Rahamani, kajikaza kutukuwa
Name yangawa yakuwa, hikaza moyo si hila

18

Mateso humabadili, aso na moyo thabiti
Apawapo idhilali, japo ingawa katiti
Huona ni afadhali, awate yakwe ya dhata
Ela langu siliwati, n'shishiyelo ni lilo

19

Wangi washasumbuliwa, waneni wa kweli hiyo
Na wangi washauliwa, kwa kutobadili moyo
Na mimi nimeradhiwa, ku'yandama sera hiyo
'Tafuwata zao nyayo, n'shishiyelo ni lilo

20

Atwambizile Rasuli, kipenzi cha Bwana Mn'gu
Ya kwamba tuseme kweli, japokuwa i utungu
Na mimi siibadili, na yiyo imani yangu
Nililoamini tangu, na lilo hilo sil'ati

21

Kweli naitiya tamma, nikuage ndugu yangu
Kweli si mwenye kukoma, kuwambiya walimwengu
Kweli si'yati kusema, katika uhai wangu
Name kwa upande wangu, hi'yambiwa 'takubali

Jipu

1

Towa taka masikiyo, upulikize uneni
Haya upulikizayo, uyatiye akilini
Kwani ni muhimu hayo, wendani utabaini
Kwa hivyo fanya makini, upate kuyasikiya

2

Moyoni furaha sina, ningaitaka sinayo
Si usiku si mtana, ni mamoja kwangu hayo
Mateso nnayoona, yaujuwa wangu moyo
Si mwako na wayowayo, uliyonifikiliya!

3

Nna jipu lintunza, linipalo tabu mno
Tangu liliponianza, kamwe sipati usono
Kwamba ni mara ya kwanza, kuuguwa ndwezi hino
Latoma kama sindano, utunguwe nakwambiya

4

Si jana wala si juzi, liliponianza tangu
Ni mingi mno miezi, nnadhofu hali yangu
Nnakonda kama uzi, kwa kushitadi utungu
Kubwa tumaini langu, ni mwishowe nangojeya

5

Hitaka keti siwezi, kwamba li makaliyoni
Kutwa huwa yangu kazi, kusimama; ntendeni?
Na usiku usingizi, siupati aswilani
Kucha nakesha mwendani, kwa utungu kuzidiya

6

Kili kipele mwilini, ndiyo mwanzo wake kuwa
Sikujuwa aswilani, kuwa jipu chaja kuwa
Ningekijuwa zamani, ningekitangiya dawa
Na kwamba sikutambuwa, ndipo hakiwatiliya

7

Jambo nilingojevalo, ni kutimu yake siku
Ningojevalo ni hilo, tena kwa kubwa shauku
Itimupo ndimi nalo, ja mwewe na mwana kuku
Ni furaha hiyo siku, kwangu na wenzangu piya

8

Siku ya kuiva kwake, hiyo ndiyo siku kweli
Huo ndiwo mwisho wake, na mwisho wa idhilali
Idhilali in'ondoke, mimi nayo tuwe mbali
Siku hiyo ni mawili, kuteka au kuliya

9

'Taliminya litumbuke, lisinisumbuwe tena
Usaha wote utoke, utoke nikiuona

Midamu itiririke, kama ng'ombe alonona
Jipu hili mwana lana, Mn'gu mbwalipa hizaya

10

Jasho jembamba litoke, ndia mbili likitona
Na hapo nitetemeke, si kwa baridi kuona
Bali kwa utungu wake, utakaozidi sana
Hapo ndipo nitasona, na moyo ufurahike

11

Baada ya yote haya, jaraha niliuguze
Kwa madawa kulitiya, ili kwamba yanipoze
Irudi yangu afiya, na zaidi niongeze
Nirukeruke niteze, kwa furaha kuningiya

Kalamu sasa natuwa, kaditamati lisani
 Nadhani nilotongowa, 'mekungiya akilini
 Jipu nitalitumbuwa, libaki kovu mwilini
 Suala kuu ni: lini? Ni siku ikitimiya

Mamba

Namba nawe, niwe kama waambao
 Niupambe, upendeze wasomao
 Niufumbe, wafumbuwe wawezao

Kuna mamba, mtoni metakabari
 Ajigamba, na kujiona hodari
 Yuwaamba, kwamba 'taishi dahari

Memughuri, ghururi za kipumbavu
 Afikiri, hataishiwa na nguvu
 Takaburi, hakika ni maangavu

Akumbuke, siku yake ikifika
 Roho yake, ajuwe itamtoka
 Nguvu zake, kikomoche zitafika

Afahamu, mtu hajui la kesho
 Hatadumu, angatumia vitisho
 Maadamu, lenye mwanzo lina mwisho

Mnazi Vuta N'kuvute

ALII

Ndugu ulo mnazini, wanitafuta balaa
 Nakwambia shuka tini, katakata wakataa
 Wafanya ni masikani, mustarehe 'mekaa
 Utashuka au la?

BADI

Ndugu tini ya mnazi, nilo juu nakujibu
 Haya ni ya upuuzi, unambiyayo swahibu
 Kushuka tini siwezi, pasi kuuwa sababu
 Hiyo ni yangu jawabu

ALII

Sababu ya kukwambiya, ya kwamba ushuke tini
 Ni kuwa nataka kweya, huko juu mnazini
 Kwa ajili nami piya, nitunde nazi mwendani
 N'shakweleza kwa nini

BADI

Hayo ni ya kutekesha, unambiyayo ndu yangu
Wataka niteremsha, juu ya mnazi wangu?
Wanistaajabisha, kuniamuru kwa changu
Una kishaa mwenzangu

ALII

Sina kishaa sinani, akili yangu kamili
Ni wewe usobaini, pale ulipo ukweli
Mnazi ni tangu lini, ukawa ni yako mali?
Sinitendee feeli

BADI

Wabobojekwa maneno, yasokuwa na maana
Ni ya kipumbavu mno, hayo uliyoyanena
Iwapo mnazi huno, si wangu; mbwa nani bwana?
Seme ni juwe bayana

ALII

Mnazi ni wa shirika, mimi na wewe mwendani
Unshakuwa wataka, kunitowa shirikani?
Hilo halitatendeka, wala haliwezekani
Sikubali abadani

Takupa habari yake, kama wewe hufahamu
Kutokeya mwanzo wake, hata leo ikatimu
'Takweleza utosheke, kwa maelezo timamu
Ujuwe sina wazimu

Mnazi yake aswili, uli mbwa wazazi wetu
Mbwa baba zetu wawili, pasi kungiya wa tatu
Mali yao ya halali, hawakunyang'anya watu
Sasa wafile ni wetu

BADI

'Takukatiza kauli, niwia radhi mwenzangu
Hapa ninayo suali, ikerayo moyo wangu
Katika hawa wawili, pasi kungiya wa tatu
Yupi mwenye kubwa fungu?

ALII

Siwe na pupa tuliya, tuwa ndugu yangu tuwa
Tama nyingi ni mbaya, mlimwengu humuuwa
Nisikiza nakwambiya, kusudi upate juwa
Wali na mafungu sawa

Walipoaga duniya, kwenenda zao kuzimu
Mnazi walit'watiya, baba zetu wadhamu
Tuurithi sote piya, ili tusiwalaumu
Je, unshafahamu?

BADI

Tuseme ndivyo yalivyo, hivyo unenavyo wewe
Na hata kama ni hivyo, bado 'tavutana nawe
Sijaridhika vilivyo, na maelezo yakowe
N'eleze hili nijuwe

Nataka kukuuliza, suala nyingine kaka
Hivi punde 'me'neleza, mnazi ni wa shirika
Kwa nini kunihimiza, upesi nipate shuka
Na hali ni wa shirika?

ALII

Sababu ya kukwambiya, ushuke tini haraka
Mke na wanangu piya, wana ndaa mewashika
Nami nataka kukweya, nitunde nazi hakika
'Kauze wapate pika

BADI

Jambo hilo ndugu yangu, kitambo nilikwambiya
Ya kwamba chako na changu, tutanganye kwa umoya
Kisha tupige mafungu, atwaye kila mmoja
Wake kuwapelekeya

Uliyakubali haya, kuwa tushirikiyane
Muda mfupi kusiya, ukayazuwa mingine
Ukashika yako ndiya, name hashika nyingine
Ikabidi tutengane

Ndipo kunipiga vita, visivyojuwa mwanzowe
Ulotafuta 'mepata, hasara ni kwako wewe
Mpiga ngumi ukuta, huumiza mkonowe
Wapigiyani mayowe?

ALII

Bure wajipambaniza, na kwingi kujimamasa
Maneno wayageuza, kusudi si kwa kukosa
Hivyo ulivoy'eleza, ukweli hukuugusa
Wafita yako makosa

Kushirikiyana nawe, ni kweli nilikubali
Bali ulianza wewe, ya kwenenda ndiya mbali
Kutengana mimi nawe, haona ni afadhali
Kuliko kuwa wawili

Pamoja tulipokuwa, vyetu tukivitanganya
Jambo moja hagunduwa, ulokuwa ukifanya
Hukuwa kinipa sawa, wakati wa kugawanya
Changu ukinipokonya

Mwerevu ulijidai, fungu kubwa ukitwaa
Wanayo wala miyai, na vyakula vya kufaa
Wala hata hukinai, kwa mitumbo kuwajaa
Na nguo njema wavaa

Hali kuwa wangu wana, wadhii mno kwa ndaa
Ndiyani ukiwaona, ni mitambara 'mevaa
Ni kwa kuwa kitu sina, kuwapa nilowazaa
Kwa wewe changu kutwaa

BADI

Wanambiya nilikuwa, kilo kichache hikupa
Nami kingi hitukuwa, wanangu henda kiwapa
Ndiyo sababu wakawa, wanangu wamenenepa
Na nguo njema kuwapa

Makosa haya si yangu, ya wanayo kudhikika
Lau hilo dogo fungu, kwalo ungaliridhika
Watoto wako ndu yangu, wasingelitaabika
Bali hili hukutaka

Uliona ni vizuri, kichache kutokubali
Ukafanya nyingi ari, ya kukiwata kalili
Ni heri nusu ya shari, kuliko shari kamili
Au hufahamu hili?

ALII

Fungu ulo ukinipa, wakati unapogawa
Sababu iliyonipa, hakataa kutukuwa
Ulikuwa kinikopa, ukinipa kama dawa
Hali tuna haki sawa

Lau kama ningekuwa, 'meliridhi jambo hili
Ingeonesha ya kuwa, hiyo ni moja dalili
Ya kwamba kudhulumiwa, mwenyewe nimekubali
Na hali hili si kweli

Pili ni kuwa nyumbani, mke na wana hakika
Wangekuwa wakidhani, pesa nusu nafundika
Wao wasingeamini, kwamba wewe wanipoka
Dhalimu usotosheka

Tatu ningelaumiwa, na watu kila mahali
Wao wangeona kuwa, watu wangu nawadhili
Jina baya ningepawa, kwamba mimi ni bakhili
Na hali hili si kweli

Kwani ningelidhaniwa, napata kilo adhimu
Kwamba hilo litakuwa, ni pato litalodumu
Wasingejuwa ya kuwa, dhalimu wanidhulumu
Na kunyonya yangu damu

Ndipo haona ni vyema, nijitowe shirikani
Wajuwe wanaadama, na watu wangu nyumbani
Chombo kitakapozama, na kuzama walo ndani
Nisiwemo lawamani

BADI

Ghadhabu zalokushika, na khera za kijuhula
Zilikupa kun'epuka, kwamba waucha muhula
Ulokwishita kitapika, warudiyani kukila?
Hebu sema lahaua

ALII

Kwa kuwa ni haki yangu, sitahayari kudai
'Tatumiya nguvu zangu, madhali ningali hai
Nilipate fungu langu, japo kwa ya ghali bei
Nawe hapo uwe hoi

Wewe ni mbobokwaji, maneno mangi kanwani
Ambaye ni mtendaji, alilo nalo haneni
Hutuliyana kama maji, yaliyomo mtungini
'Kangoja siku ya zani

ALII

Ni ya waoga tabiya, hiyo usemayo wewe
Shujaa humuambiya, mvita wake ajuwe
Henendi kumuoteya, ja kifaranga na mwewe
Kama usemavyo wewe

BADI

Kama kweli una niya, ya kutenda usemalo
Kipi kilokuzuwiya, kunitimiziya hilo?
Au haujawadiya, wakati wa kutendalo?
Lipi ulingojevalo?

ALII

Wanangu tangu kitambo, wangukuwa washafanya
Kila mtu yake fimbo, wali washajikusanya
Kuja kukuonya mambo, kwa changu kuninyang'anya
Lakini nikawakanya

Na sasa nalirudiya, nilokwambiya mwanzoni
Jambo nalolikwambiya, ni kwamba ushuke tini
Iwapo hutasikiya, shauri yako mwendani
Ukijafikwa ni shani

BADI

Mjinga usinifanye, wala usinishituwe
Wala usijidanganye, na orongo 'siambiwe
Alobwiya ndiye mwenye, alowata azuzuwe
Hili kaa ulijuwe

ALII

Kabla sijenda zangu, machache nataka sema
Umeninyang'anya changu, kwa kutumiya dhuluma
Pasi na shaka utungu, nitauwona lazima
Sitasahau daima

Nilitakalo ni kuwa, waja wapate yaona
Wajuwe 'medhulumiwa, kwa muda mrefu sana
Siku 'kitwaa hatuwa, pamoja na wangu wana
Pasiwepo wa kunena

Ijapokuwa nataka, kukustahamiliya
Iko siku nitachoka, zaidi kuvumiliya
Hapo litalokufika, zaidi kuvumiliya
Hilino nakuapiya

Ningenda zangu kumbuka, yote niliyoyanena
Siyatwae kidhihaka, 'kiketi yawaze sana
Iko siku itafika, haitakawiya tena
Kujulikane bayana

KIAMBATISHO 2: CHEMBE CHA MOYO (MAZRUI, 1988)

Vinyago

Waangalieni

Wale wanaotuongoza

wanavyochechemea

wanavyopepesuka

mara huku mara kule

mara hapa mara pale

kila mahali ulimwenguni

Wale wanaotuongoza

pingu mikononi

pingu miguuni

pingu maningani

Na bado wakatufanya vinyago vya sarakasi

Wametuchezesha watumwa:

Nyuso chafu kama kilabu

Tumecheka tukilia bila sababu

Mikono tukiipepea kama madubu

mpaka...

tumekuwa mabingwa wa mchezo wa utumwa

katika hili jukwaa la dunia.

Tumeshindana katika huu mchezo waliotufunza

Tukichezesha miili yetu, tukiitambaza kama mafunza

Tukipanua makanwa na midomo

tukitingisa matako na viuno

tukitoa mashuzi na misono

huku haya zote tumezibanza.

Haya basi, tupigeni mayowe

Tupigeni makofi

ili wakuu wacheke

ili wakuu wafurahike

Haya!

Haya!

Haya!

Hiyo ndiyo kazi yetu

Kwani tu vipofu

Kuliko hao vipofu!

Taji la Wema

Kilele na taji la wema
Nyota ya maisha daima... ni ujamaa
Wenye kuirudishia dunia
 heba ya kale ilofifia
 Na nyuso mwanga kuzitupia
 kuzipa nadhari ya kufurahia
Naapa! mpaka kuwasili kwake watu ni watumwa
Wanaodidimia katika vumbi la kaburi...
 bila tamaa.

Njoooni basi, njoooni tusafishe njia
Tuteme vigingi vikavu vilojikita
Wafuasi vipofu na wafalume pia
 leo siku zao zimetimilia

Tamaa yetu ni juhudi yetu
Tamaa yetu ni nafusi zetu
 zilizochaguliwa na wakati
 kujenga dunia ilo thabiti
Basi upisheni ujamaa
Upisheni huu utu.

Kula Njama

KULA
NJAMA
Kwa pumzi moja yakiungana
Kwa shauri moja yakioana
Imefahamika maana?

Nimetatizwa na tatizo moja
Hawa mabwana zetu tuishio nao pamoja
hawashushi pumzi kwa mdundo mmoja
kutuona hatuna ngoma,
 twatosheka na kungoja?

Na hawa mabwana zetu,
hawakai baraza moja, kwengine na kwetu
wakipika na kupanga
 kunyonya kila tone la damu yetu?

Na wakatupikia
Na wakatupangia
Adabu gani ya kututia
iwapo chambo walichotutulia
kimeshaindwa kutunasa kihisia
katika wavu wa lile wazo:

Kwamba mwenyewe Mngu Mwenyezi
amepanga na yake mapenzi
iwe vivi ilivyo, katika yake enzi?
Mwenye kupata apate
Mwenye kupatwa apatwe?

KULA- NJAMA

Maneno mawili yanayotisha kama kiama
yalijoojua uvunjifu wa maisha ya salama
...maisha ya waliwa njama,
yaliyoshikana kama mume na mke
katika ndoa ya daima
Au bado hujatazama?

Kwani hujaona ile milango ifungwayo,
faragha kubwa itafutwayo
na minong'ono inong'onezwayo?
Dhamira chafu...nakueleza hayo
Yaani, iwapo bado hunayo

Haiwezekani unaniambia?!
Usiiwache hadaa yako ikule njama!
Risasi ile iliyokutoboa mwili mzima
tulipangiwa mimi na wewe,
tangu mwanzo wa mfumo huu.

Na ule mshahara uliokatiwa
mkato wa ndani-kwa-ndani
uliopasua mifuko yote surualeni?
Mkato ule pia naamini
tulipangiwa mimi na wewe yakini
kwa mantiki batini
ya mfumo huu.

Tuna haja ya shaka, dada zangu?
Shaka hatuna haja nayo.
Tuna haja ya utafiti, ndugu zangu?
Utafiti hatuna haja nao
Kwani tulichokiona tumejionea:
michuruziko ya damu yetu imeenea
na yote kule kule imeelekea
kwenye nyayo za wala-njama.

Lugha yao wala-njama?
Milki na faida, popote duniani!
Bei ya dhahabu ikiwaendea chini
Wenzetu wauawa kule migodini
kule kusini.

Faida ikiwapandia ‘fika mbinguni
Sisi twala njaa kwetu mitaani.
Basi ukionacho ndicho ukipatacho!
Au bado hujaamini?

Tuseme hujajua
milki haibebi bunduki?
Au tuseme hujajua
faida haina fataki
ya kutuua kwa malaki
katika Mathare za dunia?

Si yale manoti
wala si mahundi
yapelekayo mawindoni
mikono migumu
iliyorowa kwa madamu
kuwinda nyama-mtu Salvador na Msumbiji
kuwinda nyama-mtu Nicaragua na Azania
ili kupandishia wala-njama
faida iliyowashukia.

Baina ya milki nyingi
na ile milolongo ya wasio-kazi
Baina ya faida nyingi
na vile vyumba vya mateso
vya watoto na wazazi
Kuna majitu
manene
mazito
yaliyojificha yakafichika
kama MAFUNZA chini ya mawe.

Mafunza!
Kama wahujaji waliorukwa na subira
wakaacha makasri yao yaliyo imara
Kuja kukusanyika
katika Maka za mauaji yao
Washington, London, Geneva,
Ambako njama huliwa
zikatema cheche za hofu
pande zote duniani
Hakuna njama waniambia?
Basi ni tamko gani la kueleza
haya yaliyokaa kama miujiza?
Waweza kuwaza?

Watu kukutana kwa hiari
kuongeza asili-mia mia kwa siri
itakayowaondolea mamilioni

chakula chao mezani.
Itakayowawekea kitandani
moto wa njozi zisizo kifani
za mwisho wa maisha yao
hapa ulimwenguni.

Njoo basi, sogea kidogo
Tuimbe nyimbo zetu,
zile nyimbo za unyago
Bwana Kula-Njama katuletea muhogo.

Kwa sababu,
maadamu kuna majitu
ikaayo na kupangia watu
kutumalizia maisha yetu
hakuna hila yoyote duniani
iliyofinyangwa kwa hii lisani
itakayoniondolea hili ninaloamini
kwamba haya majitu
daima
yala njama
kula watu nyama!

Mwapigania Kitu Gani?

Yadunda na kupwitapwita, ngoma kuu ya vita
Ikitaka nyama iliyo hai
itokomezwe, chumani ikijikita
ikitaka mtumwa baada ya mtumwa
wa kila nchi, ulimwenguni mzima
ashike chuma cha kifo-cha-mwenziwe
kifo cha utumwa.

Na kwa nini?!
Dunia inatetemeka
bila mavazi
bila malaji;
binadamu akiogelea katika ziwa la damu
ili watu fulani... ulimwenguni
wanufaike kwa kipande cha ardhi
... bila thamani.

Matapo ya watu
yakilia kama mafisi
waikata na kuichoma ngozi ya dunia
ili watu fulani
mahali fulani... ulimwenguni
waendeleo kuishi kwa jasho la wenzio
... bila imani
Na nani aliye juu ya mbingu
Ya vita hivi vya uchungu?

Mungu?
Uhuru?
Miliki?

Ewe unayejitolea roho yako
Lini utaizindua akili yako
Usimamame wima kwa nguvu zako
Uwache kupigana na ndugu zako
... wadhulumiwa wenzako
ili watu fulani tu
waendeleo kusarifu unyonyaji
wa watu duniani
bila upinzani?

Ni lini
 utaligeukia tabaka dhalimu
 la taifa lako mahushumu
uliulize:
 Nakipigania kitu gani?
 Nampigania mtu gani?
 Nayapigania maisha gani?

Wana-haramu

Hebu nikuulize Mama Afrika,
Kwa nini...
Mimba changa ukajichukulia
Ya haramu sana ilotepetea
Ukazaa wana walo jahilia
Wasiojijua, wala yao njia?

Kuzurura ukamalizikia
Bila muruwa, heba kukupotea
Ukawa ganda la kupitia njia
Usiwe maoni ya kuonelea?

Kwa nini...
Ukazaa kizazi kilo kiwete
Kilohasirika kwa wakati wote
Kilopagawa kwa kingi kite
Hata utu wake ukakipotea?

Ah moyo waumia!
Hupigwa na mshangao
 Niwafikiriapo
Wale barobaro wanao
Wasaliti wanati walo na vyeo
Walomdhidi mama mzazi wao
 Kwa mradi wao.

Lakini sijali
Sijali kwani najua
Siku moja itawadia
Wana-haramu watajihalalia
Kila cha haramu kukuondolea
Na kukutakasa
...mama wasikia?

Hiyo siku ya siku itakapofika
Kila la dhuluma litajikatika
Na kila mahali utadhihirika
Mwisho wa salata na uharamia
... mama wasikia?

KIAMBATISHO 3: DIWANI YA KARNE MPYA (WALIBORA, MH. 2007)

Tazama

K.W. Wamitila

Tazama utaona,

Maskini wanaoishi katika dhiki za karne
Fukara wanaodidimia katika kinamasi cha dhuluma
Fakiri wanaogugunwa mili na michonge wa tabaka
Wakiwa wanaokufa njaa kwa kukosa cha kujilia
Maskini wanaoteswa kwa kuililia auni
Umma unaolia kwa kuikosa nafuu,
Kwa kupakosa pa kulala
Kwa kukikosa cha kuvaa
Kwa kuyakosa matibabu
Kwa kuyakosa maisha

Tazama kisha utaona,

Vitambi vinavyotetemeshwa na uto wa nyama
Shingo zinazoshabihiana na mibuyu ya pwani
Mili iliyonenepena tamthili ya kiboko
Vinywa vinavyokula na kusaza kwa wingi
Macho yasiyopenda kuuona uhalisi

Tazama tena, kisha utaona

Wanasiasa wanaojisifu kwa maendeleo
Mawaziri wanaorereja sifa za sera za nchi zao
Wanadini wanaoimba kwa kupagawa
Na kiongozi anayejisifia kipaji cha kuona mbele

Msitu Ni Ule Ule

Omar Babu (Abu Marjan)

Hitaraji tuungane, undugu ututawale
Hataka tushikamane, kama pete na kidole
Kumbe bwana nidengene, wakuu wetu wawale!
Msitu ni ule ule, na fisi ni wale wale!

Waimbe waonekane, kwamba wajali watule
Siku nenda wambizane, ujima waulekele
Hoja tuheshimiane, na amani teletele
Ela mwitu ule ule, na fisi ni wale wale

Vigogo waumbuane, matayo pasi sumile
Na mara watukanane, wapigizane kelele
Eti kisa twondokane, na ya uhasama ndwele!
Bado mwitu ule ule, na fisi ni wale wale!
Sikuye wapapurane, maguvu waamilile
Muda wasisemezane, ja mahasimu wa kale
Wakae wasikizane, warejee pale pale,

Kwani mwitu ule ule, na fisi ni wale wale!

Uwadhani watengane, wadumu hivyo milele
Ghafula waungamane, ubaki kuliya ole!
Maadui wapatane, watakapokaa wale,
Kwani mwitu ule ule, na fisi ni wale wale!

Tujenge Nti Wanati

Muchai bin Chui

Mimi naunga mkono, naunga wazo thabiti,
Umoja wetu wanati, katika kujenga nti,
Ndilo jambo madhubuti, linalofaa wanati,
Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati.

Kila raia wa nti, anayo haki ya nti,
Kutoa wazo thabiti, kushiriki harakati,
Ili msingi wa nti, upate kujithibiti,
Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati.

Mzalendo madhubuti, ni yule mpenda nti,
Akakataa unyeti, serikali kusaliti,
Asikubali katiti, kutoa siri za nti,
Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati.

Haya shime wananti, tujumuike umati,
Tusirefushe uteti, viama kuweka kati,
Msingi wetu ni hati, tufanye kazi kwa dhati,
Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati.

Tusikubali wateti, ambao nia ni viti,
Bungeni kwenda manoti, na kunyakua ploti,
Na huku nyuma mauti, kutukamua matiti,
Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati.

Kura iwe ndio cheti, ukabila ni mauti,
Sio kupenda manoti, kuhongwa kati kwa kati,
Ngao iwe ni tikiti, kadi zetu tuzatiti,
Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati.
Rasilmali za nti, mbuga za pori na miti,
Vifaru, ndovu na nyati, utamaduni mufiti,
Tukazie harakati, raha yetu wananti,
Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati.
Uwe Jaluo Hakati, au Mkamba Kaiti,
Mnandi Eldoreti, au Kikuyu wa kati,
Umoja wetu wanati, ndio msingi thabiti
Mjenga nti mwanati, mvunda nti mwanati.

Tabasamu Zao

Timothy Arege

Nitafakaripo kwa tuo
Moyo hunitweta na mtetemo kunivaa
Wanijiapo na tabasamu
Ambazo hulinyonga tumaini langu
Ninahuzunika.

Wanisalimiapo kwa mikono miwili
Na chini kuniinamia
Wakiyakoleza yao matamshi
“Mzee... ndugu... Salama! Salama!”

Nachukia zao nyendo.
Wanadai kwa mihemko
“Lazima tungo kutetea wanyonge”
Lakini nitazamapo, wenyewe hawasiti
Mnyonge mkononi kumtia
Na kwa maguvu kumfikicha
Haki yake kumhini
Mtetezi kufaidi.

Wote hawa sioni yao tofauti.
Wote hawa, sawa
Na mwanasiasa mwehu
Ni mtoto wa jicho.
Wanapotabasamu nachelea kuridhia.
Hutabasamu wadhamiriapo mengine.

Tabasamu zao ni ishara ya maangamizi
Wanipangiayo kimoyomoyo, kimyakimya
Wafurahie kutakarika kwangu
Kwenye tanuri hii ya maisha.

Ndoto Mbaya

Hezron Mogambi

Jana niliota
Ndoto mbaya ya hakika
Ndoto ya uchoyo
Uchoyo wa ukuu
Ukuu wa kuwanyanyasa wengi
Ndoto mbaya ya jinamizi
Wanaowala watu wengi wakicheka
Wanaokula wakilalama njaa
Wanawameza wakiwa hai wazimawazima!

Juzi niliota ndoto mbaya pia
Ndoto yenye mazingaombwe
Wanaowala wakiwacheka na kuwapigia makofi
Makofi ya kuwasifu wale wanaowatafuna
Kusifu kwa uchungu wa kutojua kufahamu
Makali yanayozima uhai wa wengi

Leo naota ndoto
Ndoto ya mchana
Mchana wenye giza
Ndoto mbaya iliyojaa mazimwi
Mazimwi wenye kuhangaisha wengi
Kwa ahadi za uongo zisizokwisha

Usiku naogopa kuota tena
Ndoto mbaya za 'kaa vivyo hivyo'
Ndoto yenye kujaa giza mbele
Giza linalotisha maisha ya kizazi!

Je, kesho nitaota?
Ndoto yenye uhai wa kifo
Ndoto ya matumaini yanayoyeyuka
Kuyeyushwa kwa jua la mchana
Mchana wenye giza totoro?
Nauliza!

Chini ya Mgunga

K.W. Wamitila

Hutokea siku nikaketi na kuwaza
Hukumbuka mgunga mnene
 ulioliinamia shamba la jirani
 tulikoketi na kuimba kwa
 sauti herufi zote
 tulikofunzwa jinsi ya kuandika
 juu ya mchanga tifutifu
 tulikoandika kwa madole gumba
 ya viguu vyetu vya kitoto...
 tulikotimua vumbi tukiendesha
magari ya majani ya mkonge
na kuigiza sauti kwa matumaini.

Nakumbuka kuwa shule haikuwa na pesa
za kujenga madarasa mengine
 serikali nayo ilishatobokwa na mifuko
 mapeni yakaanguka njiani
 kwenye safari ya uhuru
 na kuokotwa na mikono ya mtembezi mwepesi
 aliyeelekea bungeni ilikokuwa yake ofisi!

Mgunga ulikuwa kivuli jua kali kutusitiri
Mgunga ulikuwa msitu wa viboko vya mwalimu
Lakini ulikuwa pia ubao wa wanasiasa wa kuwekea
makaratasi manene ambayo hayakuisha
ya baraza la mawaziri.

Huikumbuka vizuri siku moja mwalimu alipoliacha
karatasi moja ubaoni, tulipaswa kuyakariri majina
mengine...

Alipoondoka
Tulichochewa na maembe ya jirani
yaliyoiva na kutualika
Tuliondoka... nyatu nyatu
maneno ya mwalimu
yakitufuata... *Viongozi hawa wanatulinda
na wanaangalia kila kitu nchi hii*
Tulinyatia shamba
La maembe nyatu nyatu
Na kuanza kuyakwepua
Viongozi wakituangalia!

KIAMBATISHO 4: MSIMU WA TISA (KITHAKA WA MBERIA, 2007)

Minyororo ya Njaa

Tumerudi kwenye dimbwi la huzuni
Kana kwamba kamba isiyoonekana
Inatuvuta kila baada ya miaka mitano
Kuturejesha kwenye bonde la machozi

Kurasa za magazeti na viwambo vya runinga
Vinaonyesha tena picha zinazoshtua hisia:
Watoto waliomumunywa na kinywa cha njaa
Wakabakia na macho yanayodondoka dhiki
Na vipande vya mianzi mikavu badala ya miguu

Mzee anayekemewa na tumbo inayolalamika
Amekalia gogo huku ukungu wa kukata tamaa
Umezidisha idadi ya miaka usoni mwake
Mbavu zake zimechomoza kama fito zilizopinda
Katika ukuta wa udongo uliovammiwa na mvua

Kwenye kijiji cha mikakaya, minga na vumbi
Jamaa na majirani waliovaa huzuni kama veli
Wanaaga udongo wa fusi la kaburi ya tano
Wametoa kwaheri zenye moto wa uchungu
Kwa mtoto aliyeshikwa mkono na njaa
Akaambiwa: Njoo nikupeleke kuzimu!

Kwenye kijiji ng'ambo ya mto usiokauka
Mama asiyethubutu kukata tamaa liwe liwalo
Anachemsha matunda-mwitu machungu
Kushawishi kokwa jeuri zilainike chunguni
Kuokoa watoto wenye miguu ya vunjajungu

Jijini, wimbo ni uleule wa kughasi hisia
Wanasiasa wanalaumu anga kwa janga
Hawaoni kwamba njaa isiyohama nchi
Ni tunda chungu la siasa za pesa-nane
Siasa bila ramani, bila dira, bila kurunzi

Asemaye kwamba ukame ni kudura ya Mungu
Anenaye njaa ni kazi ya uovu wa anga bahili
Ahurumiwe, amezima ubongo wa bongo!

Anga la nchi si mgeni ni jirani wa miaka na mikaka
Udongo tunaolima hauna mafumbo yasiyofumbulika:
Unapokabwa koo na kiu hausikii mwito wa wakulima!
Linalotabiriwa wazi kama kuchomoza jua asubuhi
Litaitwaje ajali na mwongo anayehitaji dawa
Au binadamu mwenye ubongo wa kongoni!

Usingizini

Ardhi yenye siha na uchangamfu wa rutuba
Imelala usingizi katika kitanda cha maumbile
Tukinong'onezana: "Anga linaonea nchi!"
Tambarare zenye uwezo wa kuhimili mamilioni
Zimeachiwa nguchiro, panya, mchwa na nyenze
Katika taifa linalotapatapa katika dimbwi la njaa

Daima dawa ya thamani inatiririka katika mito
Inatupita na kumezwa ovyo na bahari na maziwa
Katika taifa linalonyongwa na mikono ya njaa

Majira yanapofungua mlango mkuu angani
Ba dawa kuteremka kutoka maghubari ya neema
Tunasimama tukitabasamu huku akili zimefunga
Na kuacha tiba ipotee katika mito, bahari na maziwa
Na kuacha taifa likisinzia hadi lishtuliwe njaa

Ni lini reli na barabara za lami na changarawe
Zitizingia katika vijiji vya mikakaya na vikwata
Ili ukame unapoanza vita dhidi ya wafugaji
Masoko ya nyama na ngozi yawe kimbilio
Kabla ya mifugo kuwa karamu kwa nderi?

Kwa nini wenye nyoyo za kusaka riziki kwa juhudi
Hawana stima ya kuzungumza na chuma na mbao
Katika viwanda chini ya mitini na miembe
Kuunda miavuli ya kujikinga kutokana na njaa?

Wanaonyongwa nyoyo na mafuta ya utajiri
Wamebana mikononi maelfu ya ekari za rutuba
Huku wajukuu wa waliopokonywa urithi kwa mijeledi
Wakiwa hawana vikata vya kukuza vihimili vya maisha!

Kwa nini tunajifanya nyumbu wa Maasai-Mara
Ambao bila kuchukua hatua, miaka na mikaka
Hupigwa dafirau na hasira nyekundu ya Mto Mara
Na kuwa karamu murua kwa mamba na nderi
Bila nyumbu asemaye: "Hayatakuwa tena!"

Ni lini tutaimarisha urafiki na teknolojia ya kilimo
Tufue tupa kama mataifa yanayokula bila aibu
Tukate hii minyororo dhalilishi ya msiba wa njaa
Ambayo imetufunga kwenye chuma ya huzuni?
Ni nani anayejua siku adhimu au mwezi azizi
Ambamo wanaokoroma kwenye makochi ya uongozi
Wataamka kutoka usingizi wa siasa bila ramani
Wafikiche macho kwa viganja vya uona-mbali
Waongoze taifa kutoka hili bonde la aibu?

Tope la Mizozo

Serikali iliyoingia ikibeba vibuyu vya ahadi za asali
Ikivaa gwada pendezi lenye rangi za upinde-wa-mvua
Ni kama binadamu aliyekula kiapo
“Naapa, kamwe sitafuata barabara ya lami na uhasama
Daima nitapita kwenye njia ya tope zito la mizozo
Ewe Mungu usiniondoe kwenye dimbwi la huzuni!”

Kabla ya mwangwi wa shangwe zetu kuyeyuka
Tulioshangillia katika bustani pendezi ya matumaini
Walianza kugongana kama vyuma katika kapu
Likivurutwa na watoto katika mchezo usiokoma

Katika ukungu wa werevu bila maarifa
Wenye tamaa kubwa ya kuwapiku wengine
Walitumia ujanja kwenye sinia ya mamlaka
Wakajitwalia minofu na kuwachia wenzao makano
Gundi ya mkataba uliouna pamoja makundi
Ikayeyushwa na moto wa hamaki ya haki

Punde harufu ya kidonda-ndugu cha ufisadi
Ilishambulia pua ya taifa kama wingu zito la ammonia
Na kuanzisha mieleka ya miguno, jasho na vumbi
Baina ya waliojuwa wenza katika vita dhidi ya uoza

Wendao kwa magari yakipeperusha bendera za jaha
Wameburura sheria za nchi kwenye mtaro mchafu:
Wakitumia ujanja kupigia debe mkataba wa umma
Wamehonga kwa mbuga za wanyama na vyeti vya ardhi

Wakitumia genge la wahuni wenye dharau kwa wenyeji
Mamluki wenye lugha inayonuka kama samaki waliooza
Wale tuliopatia wadhifa wa kutulinda pamoja na mali zetu
Wamevamia haki zetu kwa kichaa cha usiku wa manane
Wahuni wa kigeni wamekaribishwa nchini kwa siri

Na kupewa vyeo vikuu na funguo za milango ya chuma
Wameishi starehe wakijinaki kwa maneno yenye uvumba
Wakitishia polisi kwa mbwa wakali katika kasri zao
Kijeuri, wakichomoa bastola dhidi ya wahudumu wa umma
Wafadhili wao wenye mashagingi yanayopeperusha bendera
Wakiwatetea kwa lugha thabiti dhidi ya raia wa taifa

Misukumo inavuma kama bahari yenye hasira
Ukitafuta mwamuzi humwoni akijaribu kuzima moto
Haneni neno la kukwamua muungano topeni
Miguu ya taifa inataaliwa na tope zito la mizozo

Werevu

Angalipuuza mashauri ya wajanja waliomzunguka
Na kuthamini maana ya maneno ya wimbo wa taifa,
Angalizingatia kanuni za mkataba wa majemedari
Silaha iliyokomboa taifa kutoka minyororo ya huzuni,
Angalifahamu uaminifu ni akiba inayozaa matunda
Na kukubali usemi: “Werevu mwingi huondoa maarifa”,
Angaligawa mapato kwa ratili iliyopangwa awali
Na kwa kuheshimu kiu cha kambi yake na ya wenza,
Mti wa uelewano ungezidi kuzaa matunda matamu
Leo, kwa furaha, tungalikuwa tukiyala yakiwa mabivu

Badala ya kuongozwa na ndoto ya taifa angavu
Mgavi alizingatia sauti laini za genge la walafi
Akawapakulia thuluthi mbili za sinia la ngawira
Na kuwapunja samba waliopigana kwa meno na kucha

Si ajabu, walioliwa bangu na kuteswa na moto wa majuto
Walijiandaa na kusubiri kwenye medani ya mkataba mkuu
Punde viganja vilikazwa katika kamba ya “Vuta Tuvutane!”
Vidole vya miguu vikajikita katika udongo mzito wa kinamo
Werevu wakaangushwa na kubururwa kwenye tope la aibu

Gari la siasa likaacha barabara ya lami
Na kujitosa kwenye ujia wenye udongo chepechepe
Mwendo wa kasi tuliotarajia utufikishe kwenye ufanisi
Ukawa safari ya kusukuma na kuvuta matopeni
Kusudi mgavi asukumiwe gari lipite kinamo lovulovu

Kwa kugopa kutereza na kukwama kwenye mitaro
Amelainisha makabila kwa mabenzi yenye bendera
Na kkuongeza idadi ya wanaokamua nchi kwa fujo
Kinyume na ahadi iliyong’aa jana kama nyota

Msimu wa Tisa

Leo ukumbi wa ukumbi umejaa vumbi jeuri
Kimbunga cha ubinafsi, uzembe na kiburi
Kinavuma kama bahari inayoteta na tufani
Ni nani atakayeimba wimbo wa uzalendo
Katika huu ukumbi wa msimu laanifu wa tisa
Ambamo nyoyo za waliotumwa kujenga taifa
Zinadunda kwa mpigo wa ubinafsi uliokithiri-
Ukumbi ambamo wingu la nzige wa jangwa
Linakula karamu haramu kwenye mti wa jamhuri

Punde walipokula kiapo cha uaminifu kwa nchi
Bila kujali vinywa vinavyopiga miayo ya njaa
Walivamia ghala la taifa kwa tamaa inayovuma

Waliovishwa makoja katika mabaraza ya walaji wapya
Walipeperusha bendera kwenye mabenzi ya bei duwazi
Kinyume na ahadi zenye ubani katika majukwaa ya jana
Ambamo tuliahidiwa majira ya nidhamu inayong'aa

Zilifuata ziara za kubenua vifua na kuteuka vijijini
Walijinadi kwa akina yahe waliovaa matambara
Walitifua vumbi kwa mabenzi na mapajero mapya
Na kuduwaza watu kwa ujanja wa mlo wa siku moja
Kabla ya kuhama kama mbayuwayu wakati wa kiangazi

Baada ya kupingwa kutunyang'anya mwishoni mwa msimu
Wameshika rungu nzito na kupiga dafirau bajeti ya taifa,
Kwa ubinafsi usiojali walio kwenye minyororo ya ukame
Wamejitwalia marupurupu laanifu eti ya kulipia usafiri
Kama kwamba dawamu wanasafiri hadi kwenye ukingo wa bara

Jukumu waliloomba kwa kupiga magoti na kutoa ahadi
Tukawapa tukidhani watatusafirisha kutoka bonde la huzuni
Wanalitimiza kwa kujikokota kama konokono au yungiyungi
Wamegeuza ukumbi wa taifa nembo ya uzembe na aibu

Vikao vya majadiliano vinavunjwa kwa kukosa idadi murwa
Wanaoitwa kwa jina lenye marashi na kulipwa kwa dhahabu
Hawaji ukumbini wakafika thelathini kutimiza kanuni
Wakija huja wamevaa machovu kama magwada ya chuma
Mambo huwapita usingizini wakidondokwa na udenda

Viongozi wa kamati za kupiga miswada darubini
Wanayumba hawana nguvu za kubeba jukumu adhimu
Hawakupata nyadhifa baada ya kupimwa kwenye ratili
Uchaguzi ulikuwa kazi shaghala-baghala ya waliosinzia

Muda wa swali adimu kwenye ratiba uwadiapo
Muulizaji hayupo kwenye idadi ya wachache ukumbini
Ameketi hoteli akipumbaza vizuu wake kwa vinywaji
Akipanga njama za kunyakua taji la mkuu wa kabila

Swali la pili limeulizwa limechangamsha akili kwa ubora
Bali kiu cha kusikiza jawabu hakitakatika hadi juma lijalo
Waziri hayumo anacheza gofu na majambazi wa kigeni
Badala ya naibu wake kuwapo kujaza pengo la wizara
Yumo kitandani amelemazwa na manofu ya nyama ya jana

Karaha ya upungufu kwenye ukumbi wa *waheshimiwa!*
Inapoendelea kughasi hisia siku zisizofikia mwisho
Wachache wanaopiga miayo kwa ulemavu wa machuvu
Wanakata kaulil ya kuzunguza ufunguo wa sefu ya taifa
Mabilioni yanatolewa kwa matumizi bila kumulikwa kwa kurunzi

Vitabu vya historia vitakapomulika msimu wa tisa
Vitatesa pua kwa harufu kali kama uzushi wa kicheche-
Mnuko wa wasaliti waliovishwa magwada ya heshima
Na kulishwa mayai, maziwa, asali na nyama ya nundu
Kwa miaka mitano ya usaliti unaonguruma kama radi

Msimu Mwingine wa Wasaliti

Vitimbakwira watarudi karibuni kutoka karamu haramu
Utazona barakoa za tabasamu kwenye nyuso zao
Watakuja kutugawia peremedede zenye sumu ya akili
Watalewesha watu kwa pombe kutoka vibuyu vya maneno
Wataahidi kesho yenye mapipa ya maziwa na mitungi ya asali
Nasi, tukiongozwa na ramani ya tumbo na dira ya ubinafsi
Tutapanga milolongo katika mvua ya Disemba
Tukikaribisha, labda, msimu mwingine wa wasaliti

Kitini

Tulipoguna kwa maumivu makali kwenye misuli
Juhudi za kizalendo zilipopamba moto yakini
Tulipotokwa na michirizi ya jasho tukitaka utu
Tulipopambana na dhiki ya giza la miongo miwili
Waziri aliyeridhika, alitushauri kwa ulimi wa kinaya
 Juhudi zenu zenye nia ya kung'oa chama
 Ni sawa na ubwege wa kutaka kukata mtini
 Kwa wembe ulionyolea tena na tena!

Alipotanabahi kuwa chombo chake kilikuwa taabani
Ukweli wa siasa mbaya ya kutumia na kutupa jaani
Ulipommulika machoni kwa mwangaza wa ufahamu
Alijibambua ngozi kuukuu kama nyoka mjanja
Akaingia uwanjani kwa mwili uliometameta
Akapiga pembe adimu ya mkombozi wa umma

Baada ya umma uliochoshwa na kiu cha haki
Kumiminika shambani wakiimba kwa umoja
Na kung'oa mikalatusi iliyonyima umma maji
Waliotukejeli kwa tashbihi za mtini na wembe
Sasa, wameketi kwenye kiti cha bembea cha taifa
Wakila matunda ya mti uliopandwa na waliosahaulika

Waharifu Huru

Bila kutarajiwa, onyo za mashambulizi dhidi ya “wageni”
Zilipaa na kuchafua anga kama harufu ya amonia
Vilifuata vijinga vikipulizwa na pumzi hatari za wanasiasa,
Taya za miako zilitafuna mbao, fenicha, nguo na vyeti
Maghala ya chakula na matumaini ya kesho yenye shibe
Yalifutiliwa mbali na upepo wa wendawazimu wa kupangwa;
Kutoka mikononi mwa fukara walioleweshwa kwa chuki
Mishale ilipiga mbizi katika miili ya wakazi wa makabila mengine
Panga za ghadhabu zilishuka baina ya vichwa na viwiliwili

Vituo vya biashara vilivyonawirishwa kwa maisha na heshima
Vilichimwa na kubakia magofu yenye mwanangwi wa huzuni;
Mashamba yaliyohimili familia na mimea tele na mifugo
Yalivamiwa na kwewe jeuri na kuminywa afya ya jana
Wajane na mayatima walibaki katika dukuduku la kukata tamaa;
Chemchemi za karo ya watoto zilika na kubakia makuo tasa

Vijana wa kike walifuata njia ya mchanga didimizi wa ukahaba
Wa kiume walikwama kwenye bonde la madawa ya kulevya
Na kisha kutumbukia katika dimbwi la wizi na unyang'anyi;
Bali katika wingu la unafiki wa "amani, upendo na umoja"
Badala ya wahandisi wa wa jakamoyo kutetemeka mahakamani
Badala ya wenye damu viganjani kutupwa korokoroni
Wanaendesha mashagingi yenye bendera za mamlaka
Wanalipwa mishahara minono wakiitwa "viongozi wa taifa"

Tume za Rais

Napendekeza tuunde tume ya rais
Tumnunulie kila mwanatume *Hummer*
Ichunguze kama njaa inaweza kuua
Kisha tuunde tume nyingine ya rais
Ihariri taarifa ya tume ya rais
Napendekeza tuunde tume ya rais
Tumjengee kila mwanatume kasri
Ichunguze jina la Rais wa Jamhuri
Kisha tuunde tume nyingine ya rais
Imtangazie Rais jina la Rais
Napendekeza tuunde tume ya rais
Tuitengee nusu ya akiba ya Banki Kuu
Ichunguze kama rais ni rais bila tume za rais
Kisha tuunde tume nyingine ya rais
Imshauri rais kuhusu rais na tume za rais

Napendekeza tuunde tume ya rais
Tuilipe kwa mkopo kutoka vitanzi vya Breton Woods
Baada ya miaka mitano ya kumandari na kunywa mvinyo
Wamshauri rais namna ya kuficha taarifa za tume ya rais
Katika sefu za vyumba vya ndani vya mijengo ya rais

Magenge Matatu

Genge la kwanza la mazimwi
Lilituahidi nchi bila minyororo ya kutojua, maradhi na umaskini
Tukanengukanenguka viwanjani kwa shangwe na vigelegele;
Mwongo na nusu wa upepo wa ulafi na ukungu wa ufisadi
Ukazima mwenge wa utaifa na kuangusha uzalendo mtaroni
Harufu ya ukabila ikachafua nchi kama uzushi wa kicheche

Genge la pili la mazimwi
Lilituahidi majira maangavu ya amani, upendo na umoja
Tukajijeruhi koo kwa kuimba "Juu! Juu! Juu sana!"

Baada ya miongo miwili viwavi na nzige wakitafuna nchi
Jamhuri ilishuka katika jahanamu ya moto wa AK 47
Zao la umaskini unaovuma kama bahari kwenye miamba

Genge la tatu nusu-mazimwi
Lilituahidi katiba mpya na dawa kali dhidi ya ufisadi
Tukaamini wimbo “Yote yawezekana bila Mfalme wa Nzige”
Baada ya miaka minne ya hila, tamaa na usingizi ulingoni
Ahadi iliyomwesamwesa kama nyota ya taifa jipya
Imewezwa na wingu la ujanja na harufu ya ufisadi

Mwashi

Mwalimu, kuwemo ndani ya udongo
Hakutazuia kuinuka kutoka pumziko
Na kupanda jukwaa la mar mar na mvuli
Kupokea hili koja la mawaridi adimu
Kutoka kitalu cha maua moyoni mwangu

Mwalimu, mikono azizi ya wazazi
Iitumia vyema udingo wa malezi
Kufinyangia mwafrika mheshimika
Mzalendo mwenye ndoto angavu
Kiongozi mwongoza kwa vitendo

Ulikuwa mwashi aliyekolea ujuzi:
Kiswahili na usawa wa makabila
Ulizifanya mawe adimu ya ujenzi
Matamshi yaliyochujua kwa kichungi
Na maisha yaliyometameta maadili
Yaliyokuwa saruji ya chapa ya kutajika
Sasa tuna msingi imara wa taifa

Leo, labda, uchumi wa ukanda
Ungelikuwa imara kama kigongo
Kama ndoto yako ya kuvuta pamoja
Haingeliuliwa na wauaji wa Nairobi-
Ole wao wazungu weusi kama makaa
Na suti zao za milia na mikufu ya saa
Mazuu walioachwa nyuma na malkia
Viumbe vya kuhurumiwa kwa huzuni
Wagonjwa wenye virusi vya akili!

Ulichukia minyororo mizito ya ukoloni
Ilikuumiza akili, moyo, damu na uboho
Ulitambua uchangamfu wa miguu huru
Na furaha ya shingo bila mikatale,
Kwa hiari, ulijitolea kwa hali na mali
Kusaidia kung’oa vigingi vya ulowezi
Vilivyojikita kusini mwa Zambezi,
Pumzi za miayo ya njaa nyumbani

Hazikuyumbisha undugu thabiti
Ulisimama kwa ukakamavu mwingi
Ukachangia kukatakata seng'enge jeuri
Ambayo kwa miongo mingi ya giza
Iliwatenga watu weusi na mwangaza
Kusini mwa mto Limpopo

Hapa na pale, sauti zinaniambia
“Muinui anapopumzika kaburi
Atoke, umtie mahakamani
Kisha umnyonge kitaaluma
Kwa hii kamba ya chuma
Kwa kufungia maisha ya umma
Katika kasha la ndoto mbichi”
Hapa na pale, vihunzi vya uhalisia
Vilitia mashaka na shaka safarini:
Ndoto ya kung'arisha Mji Mkuu
Kwa kukwangura mitaa ya mabanda
Ilivunja miamba na kuvunja vigae
Kama jahazi la mwanagenzi baharini;
Kilimo cha mashamba ya jembe la umma
Hakikutia mbelewele na kuzaa matunda
Miche ilinyauka ikiwa bado michanga
Kwani kulima kwa miuo na visagalima
Si kazi ya kulisha mamilioni yenye njaa;
Lakini wenye kusema tunasema
“Mambo hayakwenda, yalienda mrama
Bali malengo yalikuwa maangavu
Kama kivulli cha mwenge wa uzalendo

Tofauti na wenzako waliolewa chakari
Kwa kunywa pombe haramu ya ujeuri
Wakabakia kubwakia kama mbwa hatari
Kulinda mapochopocho yasiponyoke,
Kinyume na wanaojiinua kwa ngazi ya tamaa
Na kujiweka kwenye vilele vya miparamuzi
Tayari kuvamia wapinzani kutoka angani,
Tofauti na wanaotesa pua za wananchi
Wanaogandama ikulu kama dondandugu,
Ulipogundua ukuukuu katika damu yako
Hukusema “Nchi hii ni mimi!”
Uliinuka bila mieleka na mikwaruzano
Na kuacha usukani mikononi mipya

Mwashi, umetuachia kumbukumbu adimu
Zinazometameta kama vipande vya almasi
Nyoyo zetu zinasema: “Afrika Hoyee!”
Ndipo mshairi anakuita kwa heshima
Uinuke, akuvishe koja la maua ya kuteua
Ewe, chemchemi ya fahari ya Mwafrika!

Kasisi

Ulishuhudia mito ya damu
Ikitirika katika Bonde la Ufa,
Uliona mvua ya machozi
Ikilowesha kambi za wakimbizi,
Ulitazama ndoto za makabwela
Zikiunguzwa na kubakia jivu,
Ulikuwa na bakuri lililojaa habari
Kuhusu manahodha wa njama,
Ulielezwa kisa cha mwanasiasa
Aliyembaka binamu yake ofisini
Ulijua dhiki ya wasichana wachanga
Waliozimwa heshima ya uanamwari

Ulikuwa na hamu ya thamani
Kusimama wima mahakamani
Na kwa silaha madhubuti ya ulimi
Kuwa jemedari hodari uwanjani
Katika vita vya kutetea utu
Dhidi ya genge la wahuni

Leo tumekukuta chini ya mnga
Mwilil uliotengwa na walio hai
Kwa radi ya risasi kichwani

Wanasema ulijitungua mwenyewe
Bali sisi si wageni katika nchi
Tunakumbuka ya juzi na jana;
Si muhali walikushona midomo
Ili kimya chako kiwe ngao kwao.